# USAWIRI WA MWONOULIMWENGU KATIKA NGANO ZA WANDIA

**FELIX NJINE MWAI**

**Tasnifu iliyowasilishwa Katika Shule ya Mafuzu kwa Minajili ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Kutuzwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili Katika Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**

**OKTOBA, 2024**

**UNGAMO NA IDHINI**

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya shahada au stashahada katika Chuo Kikuu kingine.

Sahihi: ______________ Tarehe: 22/10/2024

Felix Njine Mwai
AM12/11705/13

**Idhini**

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu.

Sahihi: ______________ Tarehe: 22/10/2024

Prof. John M. Kobia
Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihi: ______________ Tarehe: 22/10/2024

Dkt. Allan Mugambi
Chuo Kikuu cha Chuka

**HATILINZI**

©2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuchapisha, kuhifadhi kwa mfumo wowote au kutoa sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mke wangu mpendwa Bi. Joyce Nyambura Njine pamoja na binti yetu Faith Nyakio Njine kwa mapenzi yao ya dhati na kwa kuwa mihimili muhimu katika maisha yangu. Aidha, kwa marehemu babangu Geoffrey Mwai Njine na marehemu mamangu Cecilia Kabuci Mwai, Mungu azilaze nyoyo zenu pema peponi.

## SHUKRANI

Kwanza ninamshukuru Mola kwa kunipa afya njema na nguvu za kuendeleza kazi hii tangu mwanzo hadi mwisho. Shukrani za dhati ni kwa wahadhiri na wasimamizi wangu Prof. John M. Kobia na Dkt. Allan Mugambi kwa ushauri na uelekezi wa kupigiwa mfano, ambao umeufanikisha utafiti huu. Mola awe nanyi siku zote za maisha yenu. Shukrani zangu za dhati zimwendee Prof. Zachary Njogu Waita kwa kunifaa kwa ushauri, vitabu na machapisho mbalimbali yaliyofanikisha utafiti huu. Vilevile, nawashukuru kwa njia ya kipekee wahadhiri wote katika Idara ya insia katika Chuo Kikuu cha Chuka hasa Bw. Enoch S. Matundura na Dkt. Onesmus G. Ntiba kwa mchango wao katika masomo na utafiti huu. Ninawapa shukrani za dhati wanauzamili wenzagu hasa Damaris Gakii Mutabari, Purity Wambui, Bi. Asumpta Mwangi na Bi. Esther W. Maina, kwa kunichochea, kunihimiza na kunikosoa katika utafiti huu.

Vilevile ningependa kuwashukuru walimu wa Idara ya Kiswahili katika Shule ya Upili ya Mirichu kwa kunihimiza na kushirikiana nami nilipokuwa nikifanya utafiti wangu. Siwezi kumsahau Bw. John Akal ambaye alinitia shime na kunifaa kwa kuipiga msasa kazi hii. Mke wangu mpendwa, Bi. Joyce Nyambura Njine anastahiki shukrani za pekee kwa kunifadhili kwa hali na mali licha ya majukumu mengi yaliyomkabili kazini. Ningependa kumshukuru binti yangu Faith Nyakio Njine kwa kunitia shime katika utafiti wangu huu kila nilipokosa matumaini. Shukrani za dhati ziwaendee Esther Mbutha, Faith Njeri Wambui na Josphat Mburu Njoroge kwa mchango wao katika kupiga chapa kazi hii.

Ningependa kumshukuru kwa njia ya kipekee, fanani Wanjira wa Rukenya kwa kufanikisha usimulizi wa ngano tano teule na kuelezea baadhi ya maneno magumu. Aidha, shukrani zangu za dhati ziwaendee, Danson Kariuki, James Gichira, Irene Wamuyu na Luckstar Wachira kwa kuwa hadhira wakati wa ukusanyaji wa data. Shukrani za kipekee zimwendee Irene Wamuyu kwa mchango wake katika unukuzi wa ngano kumi teule kwa Kindia. Shukrani za dhati ziwaendee dada zangu Elizabeth Njeri, Nicella Njoki na shemeji yangu Lucy Nyaguthiĩ kwa kunitia shime kuendelea na masomo yangu. Ningependa kutoa shukrani za dhati kwa wote walionifaa kwa namna moja au nyingine katika masomo na utafiti huu. Wote nawaombea baraka za Mwenyezi Mungu.

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule. Ngano zilizoteuliwa ni Kabindura, Wacuka, Kamwagirwa na Kibuyu cha baba, Muya na dada yake Cinji, Thigiti na Kanyonyo, Mkutano wa Wanyama wa porini na ndovu na fisi. Malengo ya utafiti yalikuwa kudhihirisha jinsi mwonoulimwengu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa ulivyojitokeza katika ngano za Wandia na kutathmini jinsi sauti ya simulizi na mtazamo zilivyotumiwa kusimulia mwonoulimwengu katika ngano teule za Wandia. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya naratorojia iliyoasisiwa na Plato (428-348kk) na kundelezwa na Propp (1928),Tondorov (1969),Genette(1980) na Bal (1999). Nadharia ya naratolojia hutumika katika hadithi, mfuatano wa matukio kiusababishi, kutambua njia mbalimbali za usimulizi wa hadithi na kipengele cha wahusika. Mihimili ya nadharia ya naratojia ilisaidia utafiti huu katika kuhakiki mwonoulimwengu wa Wandia kwa kubainisha mbinu za usimulizi, nafasi ya wakala wa simulizi na mtazamo wa Fanani. Utafiti ulijikita nyanjani ambapo Wanjira wa Rukenya alitamba ngano kumi. Mbinu ya sampuli ya kimaksudi ilitumika katika uteuzi wa ngano sita zilizotumika katika utafiti huu. Ukusanyaji wa data ulitokana na usimulizi wa ngano teule uliotekelezwa na Fanani Wanjira wa Rukenya, unukuzi kwa lahaja ya Kindia na kutafsiri matini kwa Kiswahili Sanifu. Mafungu yaliyoonyesha vipengele vya mwonoulimwengu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa yalinukuliwa kwa njia ya maelezo kulingana na malengo ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa utunzi wa ngano teule ulikitwa kwenye tajriba ya Wandia ambayo ndiyo msingi wa fasiri wa mwonoulimwengu wao. Aidha, watunzi wa ngano teule walidhihirisha misimamo yao kiitikadi kuhusu suala la mwonoulimwengu wa Wandia. Utafiti utafaidi jamii ya wasomi kuelewa zaidi dhana ya mwonoulimwengu na nafasi yake katika utambulisho wa upekee wa jamii. Utafiti utaonyesha njia nyingine ya kuzichanganua ngano kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Walimu wa Kiswahili katika shule za upili na vyuo vikuu watanufaika kwa kutumia tafsiri ya ngano hizi kufundishia fasihi simulizi. Aidha, hekima inayotokana na utafiti huu itakuwa nyongeza ya mchango kwa dafina ya maarifa ya fasihi simulizi ya Kiafrika. Utafiti ulipendekeza tafiti zaidi zifanywe ili kubainisha mwonoulimwengu katika vipera vingine vya fasihi simulizi. Hali kadhalika mwonoulimwengu unaweza kutafitiwa kwa kutumia nadharia zingine tofauti na naratolojia.

## ABSTRACT

This research aimed to investigate the worldview of the Ndia people as portrayed in their oral narratives. The selected oral narratives used in this research were Kabindura, Wacuka, Kamwagirwa and The Fathers Gourd, Muya and his sister Cinji, Thigiti and Kanyonyo, The meeting of the Wild Animals and The Elephant and The Hyena. The objectives of the study focuses on showing how social, economic and political worldview are depicted in Ndia oral narratives and to assess how the narrative voice and focalization were used in narration of worldview in Ndia oral narratives. The study was guided by the theory of narratology whose proponent is Plato (428-348BC) and developed by Propp (1928), Tondorov (1969), Genette (1980) and Bal (1999). The theory of narratology deals with the story, causative sequence of events, ways and means of narrating a story and the aspect of characterization. The tenets of narratology used in this research were to recognize different ways of narrating a story, the causative sequence of events, the narrative agent and the narrators ideology. The study was carried out in the field whereby narrator Wanjira wa Rukenya narrated ten oral narratives. Purposeful sampling method was used to obtain a sample of six oral narratives used in this research. Data was obtained through narration of selected oral narratives by Wanjira wa Rukenya, transcription in Kindia dialect and translation to Standard Swahili. Sentences that portayed aspects of social, economic and political worldviews were selected from the text. Data was analysed and presented through discourse according to the research objectives. The research findings confirmed that composition of the selected narratives was based on the experiences of the Ndia people which laid the basis for depiction of their worldview. On the other hand, composers of selected oral narratives revealed their ideological perspectives about the worldview of the Ndia people.The research will benefit researchers to understand better the concept of worldview and its place in identification and speciality of a community. The study shows another way of analyzing narratives using the theory of narratology. Kiswahili teachers in secondary schools and teachers in universities will benefit by using the selected oral narratives in teaching of oral narratives. The findings of this research will be an addition of contribution to knowledge of African Literature.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** ....... ii
**HATILINZI** ....... iii
**TABARUKU** ....... iv
**SHUKRANI** ....... v
**IKISIRI** ....... vi
**ABSTRACT** ....... vii
**YALIYOMO** ....... viii
**VIFUPISHO NA ISHARA** ....... xii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ....... 1
1.1 Usuli wa Mada ....... 1
1.2 Suala la Utafiti ....... 4
1.3 Malengo ya Utafiti ....... 4
1.4 Maswali ya Utafiti ....... 5
1.5 Umuhimu wa Utafiti ....... 5
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ....... 5
1.7 Machukulio ....... 6
1.8 Maelezo ya Istilahi ....... 7

**SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI NA MSINGI WA KINADHARIA.** ....... 9
2.1 Dhana ya Mwonoulimwengu ....... 9
2.2 Sauti ya Simulizi ....... 13
2.3 Mtazamo ....... 14
2.4 Historia Fupi ya Wandia ....... 15
2.5 Ngano ....... 16
2.6 Ngano za Wandia ....... 18
2.7 Mfumo wa Maisha wa Jamii ya Wandia ....... 19
2.8 Utamaduni wa Wandia ....... 21
2.9 Historia Fupi ya Fanani Wanjira Wa Rukenya ....... 22
2.10 Usawiri wa Wahusika Katika Ngano ....... 24
2.11 Msingi wa Kinadharia ....... 25

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI .................................................................29**
3.1 Mahali pa Utafiti ........................................................................................29
3.2 Mpangilio wa Utafiti ....................................................................................29
3.3 Uteuzi wa Sampuli .......................................................................................29
3.4 Vifaa vya Utafiti...........................................................................................30
3.5 Ukusanyaji wa Data .....................................................................................30
3.6 Uchanganuzi wa Data...................................................................................32
3.7 Uwasilishaji wa Data....................................................................................32
3.8 Maadili ya Utafiti .........................................................................................32

**SURA YA NNE: USAWIRI WA MWONOULIMWENGU WA KIJAMII, KIUCHUMI NA KISIASA KATIKA NGANO ZA WANDIA .................................................................34**
4.1 Utangulizi ....................................................................................................34
4.2 Usawiri Wa Mwonoulimwengu Wa Kijamii Wa Wandia ................................34
4.2.1 Mivutano ya Kijinsia ..................................................................................34
4.2.2 Uchumba......................................................................................................39
4.2.3 Ndoa.............................................................................................................41
4.2.4 Malezi ..........................................................................................................43
4.2.5 Kudhibiti Nafsi ............................................................................................46
4.2.6 Maadili.........................................................................................................52
4.2.7 Haki Ya Kijamii...........................................................................................56
4.2.8 Tabaka .........................................................................................................60
4.3 Mwonoulimwengu wa Kiuchumi wa Wandia..................................................62
4.3.1 Kilimo..........................................................................................................62
4.3.2 Ufugaji .........................................................................................................65
4.3.3 Biashara .......................................................................................................68
4.3.4 Kibarua ........................................................................................................69
4.4 Mwonoulimwengu wa Kisiasa wa Wandia.....................................................71
4.4.1 Usuluhishi wa Migogoro .............................................................................71
4.4.2 Uongozi .......................................................................................................78
4.4.3 Haki .............................................................................................................81
4.6 Hitimisho........................................................................................................84

**SURA YA TANO: JINSI SAUTI YA SIMULIZI NA MTAZAMO ZINAVYOCHANGIA MWONOULIMWENGU WA KIJAMII, KIUCHUMI NA KISIASA KATIKA NGANO ZA WANDIA ......... 86**

5.1 Utangulizi ......... 86

5.2 Jinsi Sauti ya Simulizi na Mtazamo Zinavyochangia Usawiri wa Mwonoulimwengu wa Kijamii wa Wandia ......... 87

5.2.1 Mivutano ya Kijinsia ......... 87

5.2.2 Uchumba ......... 90

5.2.3 Ndoa ......... 93

5.2.4 Maadili ......... 97

5.2.5 Haki ya Kijamii ......... 101

5.2.6 Tabaka ......... 105

5.3 Jinsi Sauti ya Simulizi na Mtazamo Zinavyochangia Mwonoulimwengu wa Kiuchumi wa Wandia ......... 106

5.3.1 Kilimo ......... 107

5.3.2 Ufugaji ......... 108

5.3.3 Biashara ......... 111

5.4 Jinsi Sauti ya Simulizi na Mtazamo Zinavyochangia Usawiri wa Mwonwoulimwengu wa Kisiasa Katika Ngano Teule ......... 111

5.4.1 Usuluhishi wa Migogoro ......... 111

5.4.2 Uongozi ......... 117

5.4.3 Haki ......... 120

5.5 Hitimisho ......... 125

**SURA YA SITA126: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ...... 126**

6.1 Muhtasari ......... 126

6.2 Hitimisho ......... 127

6.3 Mapendekezo ......... 128

**MAREJELEO ......... 129**

**VIAMBATISHO ......... 134**

Kiambatisho 1: Sampuli ya Ngano za Wandia zilizotumika Katika Utafiti ......... 134

Kiambatisho 2: Orodha ya Ukaguzi ya Masuala Makuu Katika Usawiri Wa Mwonoulimwengu Wa Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa Wa Wandia Katika Ngano Teule ..................................................................... 158

Kiambatisho 3: Orodha ya Ukaguzi ya Jinsi Sauti ya Simulizi na Mtazamo Zinavyochangia Usawiri wa Mwonoulimwengu wa Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa katika Ngano Teule ................................... 161

Kiambatisho 4: Ramani inayoonyesha Maeneo ya Kiutawala na Kisiasa ya Kaunti ya Kirinyaga ..................................................................... 166

Kiambatisho 5: Picha Zilizochukuliwa Wakati wa Utambaji wa Ngano Teule Wanjira wa Rukenya (Kwanza kutoka kushoto) akitamba hadithi ya Kabindura ..................................................................... 167

Kiambatisho 6: Barua ya Uthibitisho wa kuomba kibali cha kufanya utafiti ........ 169

Kiambatisho 7: Kibali cha Utafiti ........................................................................ 170

## VIFUPISHO NA ISHARA

| | |
|---|---|
| kk | kabla ya Kristo |
| k.m- | kwa mfano. |
| k.v- | kama vile. |
| n.k- | Na kadhalika. |
| N1 | Kabindura. |
| N2 | Wacuka,Kamwagirwa na Kibuyu cha Baba. |
| N3 | Muya na Dada yake Cinji. |
| N4 | Thigiti na Kanyonyo. |
| N5 | Mkutano wa Wanyama wa Porini. |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Lugha ya fasihi ya Kiafrika ina sifa mbili ambazo ni kuwa chombo cha mawasiliano na utamaduni ambao umesheheni thamani zinazotumika kufasiri maana ya maisha na; kutambua nafasi ya binadamu katika ulimwengu (Wa Thiong`o, 1981). Mtaalamu huyu anasema kuwa utamaduni ndio kioo kinachotumiwa na binadamu kujitazama na kutambua nafasi yake katika ulimwengu. Dhana ya maana ya maisha inayorejelewa na Wa Thiong'o (mtaje) ni mwonoulimwengu wa jamii. Hivyo basi maoni ya mtaalamu huyu yalichochea utafiti huu kwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya lugha ya fasihi ya Kiafrika na utamaduni. Utafiti huu ulichukulia kuwa lugha ya fasihi simulizi ya Wandia inabeba utamaduni wa Wandia ambao ni chombo cha fasiri ya mwonoulimwengu wao.

Kwa mujibu wa Akivaga na Odaga (1982), fasihi simulizi ni sanaa iliyo hai kutokana na uwasilishaji na upokezaji kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Dhana inayojitokeza hapa ni kuwa, fasihi simulizi inasemekana kuwa hai kwa kuzingatia kigezo cha uwasilishaji ambacho ndicho msingi wa kupokezana sanaa kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Mantiki ya sanaa hai katika utafiti huu ilichochea haja ya kutafitia mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao ili kuufahamu upekee wao na kuendeleza uhai wa sanaa yao. Wataalamu hawa wanashikilia kuwa njia ya pekee ya kuelezea fasiri ya watu kuhusu ulimwengu, thamani na matamanio yao ni kufanya utafiti wa fasihi simulizi ambao unatazamisha jamii na mazingira yake. Kauli hii ilizua haja ya kutafitia ngano za Wandia kwa lengo la kutazamisha jamii ya Wandia na mazingira yake ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Mchakato huu wa kiutafiti ulinuiwa kuibua mwonoulimwengu wa Wandia kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Kwa mujibu wa Vansina (1985: 133), mwonoulimwengu ni uwakilisho wa msingi wa uhalisia katika vigezo vinavyoonekana na visivyoonekana. Katika muktadha huu, Vansina (mtaje) ameonyesha kuwa mwonoulimwengu unajumulisha maoni kuhusu viumbe vilivyomo na uainisho wake katika mpangilio na uamilifu wake. Kazi hii ilichochea haja ya kuchunguza mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule kulingana na malengo ya utafiti.

Fasihi simulizi humulika maisha ya watu na huakisi utamaduni wa watu. Mchakato mzima wa kuakisi utamaduni huu hubainisha mwonoulimwengu wa jamii inayohusika (Chimerah, 1990). Kutokana na mawazo ya Chimerah (mtaje) ni bayana kuwa mwonoulimwengu umekitwa kwenye utamaduni wa jamii. Maoni haya yalichochea haja ya kutafitia ngano za Wandia ambazo ni sehemu ya utamaduni wao ili kuelewa jinsi wanavyofasiri mwonoulimwengu wao.

Fasiri ya mwonoulimwengu wa jamii inaeleweka vyema kwa kuihusisha na maadili ya jamii yaliyokitwa kwenye utamaduni kwa sababu yanahusisha mahusiano kati ya Mungu, binadamu na maumbile kwa upande mmoja na fasiri ya wema na uovu kwa upande mwingine (Magesa, 1998). Mhimili wa maadili unashurutisha mwoano kati ya mwono wa binadamu wa ulimwengu unaoonekana na usioonekana. Maadili ni kipengele kinachodumisha uhusiano huu ( mtaje ). Fasiri hii ya mwonoulimwengu kwa mujibu wa Magesa (mtaje), ilitumika kama msingi wa fasiri ya mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao na kuchochea haja ya kujaza pengo lilipo la utafiti.

Kwa mujibu wa Kraft (1999), mwonoulimwengu ni msingi wa dhana ambazo huwezesha binadamu kupambana na maisha katika utamaduni fulani. Hivyo basi, mwonoulimwengu ndio msingi wa fasiri yetu ya ulimwengu. Kazi hii ilichochea haja ya kuchunguza mwonoulimwengu wa Wandia katika muktadha wa utamaduni wao. Lengo lilikuwa kuchunguza tajriba ya Wandia ambayo ndiyo msingi wa utunzi wa ngano za Wandia ili kubaini jinsi wanavyopambana na maisha katika muktadha wa utamaduni wao.

Ngano ni chombo kinachowezesha binadamu kufahamu ulimwengu na kwamba watu hawaoni ulimwengu uliopo mbele ya macho yao hadi uwekwe kwenye muundo wa ngano. Hivyo basi ngano ni chombo muhimu cha kufafanulia mwonoulimwengu wa watu (Abbott, 2002). Maoni haya yalidhihirisha umuhimu wa kuchunguza mwonoulimwengu wa Wandia kama unavyojitokeza katika ngano zao. Utafiti ulichukulia kwamba ngano za Wandia zinatekeleza dhima ya kuwawezesha kuelewa mwonoulimwengu wao katika mchakato wa kutafuta fasiri ya maana ya maisha.

Mionoulimwengu ni vyombo vinavyovutia uchunguzi wa kisayansi kwa sababu ina uwezo wa kuunda athari, utambuzi na tabia. (Koltiko - Rivera, 2004). Kazi ya mtaalamu huyu ilichochea haja ya kutafitia mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao ili kubaini jinsi unavyoathiri Maisha yao kwa jumla, kubainisha utambuzi wa upekee wao pamoja na kuratibu tabia zao.

Mwonoulimwengu ni jumla ya machukulio na dhana ambazo hushikiliwa na watu kuhusu jinsi wanavyofasiri ulimwengu (Kurka, 2004). Mtaalamu huyu ameonyesha kuwa mwonoulimwengu hujenga msingi thabiti wa tabia, mawazo na machukulio ambayo hutawala jinsi tunavyoishi. Kazi hii iliujengea utafiti huu msingi thabiti na kuchochea haja ya kuchunguza mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano ili kubainisha machukulio na dhana zinazoongoza fasiri ya mwonoulimwengu wao.

Kwa mujibu wa Nyonje (2006), mwonoulimwengu ni fasiri ya uhalisia wa maisha uliokitwa kwenye utamaduni wa watu fulani. Nyonje (mtaje) anaeleza kuwa utamaduni una dhima ya utambulisho wa upekee wa watu fulani na ndicho kibainishi cha mwonoulimwengu wao. Utafiti wa Nyonje (Mtaje) ulizua haja ya utafiti wa usawiri wa mwonoulimwengu katika ngano teule kwa kuwa ngano za Wandia ni msimbo wa uwasilisho wa utamaduni wa Wandia. Hivyo basi, utafiti ulichukulia kuwa utamaduni wa Wandia ni kipengele muhimu cha utambulisho wa upekee wao.

Mwonoulimwengu una uhusiano wa karibu na masuala ya kijamii kwa sababu umekitwa kwenye tajriba ya jamii (Webster na Mertova, 2007). Ngano haziibuki kutokana na ombwe tupu bali ni matokeo ya tajriba za watu katika jamii (Webster na Mertova, Mtaje). Hivyo basi tajriba inayorejelewa na wataalamu hawa ni uzoefu wa kutenda mambo na kutokana na uzoefu huu ngano zinaibuka. Kauli hii ilibainisha kwamba ngano za Wandia zilichangiwa pakubwa na tajriba ya maisha yao. Tajriba hii ya Wandia ndiyo kigezo mwafaka cha kufafanulia mwonoulimwengu wao. Hivyo basi, ngano za Wandia zilizokitwa kwenye utamaduni wa Wandia ndizo zilitumika kama msimbo wa kusawiri mwonoulimwengu wao. Hali hii ilizua haja ya kutafitia ngano za Wandia ili kubainisha mwonoulimwengu wao kwa lengo la kujaza pengo lililopo la utafiti.

Musungu (2016) amedokeza kuwa mwonoulimwengu ni dhana inayorejelea fasiri ya jamii kuhusu uhalisia wa maisha, suala ambalo huelekeza mtazamo na mahusiano ya kijamii, kiuchumi, kidini na kisiasa. Utafiti wa Musungu (mtaje) ulichochea haja ya kuchunguza mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano ili kubaini uhalisia wa fasiri ya mwonoulimwengu wao na mtazamo wao kuhusu masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Wandia, kama ilivyo jamii yoyote ile, wana utamaduni wao ambao huelezwa kwa vipera vya fasihi simulizi kama vile ngano, nyimbo, maigizo na mazungumzo. Ngano ni mojawapo wa vipera ambavyo kwavyo utamaduni wa Wandia pamoja na mwonoulimwengu wao hufafanuliwa. Hivyo basi, kulikuwa na haja ya kutafitia suala la usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia na utambulisho wa upekee wao. Suala hili limeshughulikiwa katika sehemu inayofuata.

### 1.2 Suala la Utafiti

Mwonoulimwengu ni kipengele muhimu kinachotumika kusawiria upekee wa jamii. Aidha, mwonoulimwengu wa jamii yoyote ile hutekeleza dhima ya kutoa mwongozo wa maisha ya jamii kwa ujumla wake. Kimsingi, mwonoulimwengu ni kitambulisho cha jamii na kibainishi cha mustakabali wake kwa kutoa fasiri ya maisha kwa jumla. Ngano ni mojawapo wa vipera vya fasihi simulizi vinavyobeba mwonoulimwengu wa jamii kwa kiasi kikubwa kwa sababu zinaibuka kutokana na tajriba ya jamii inayohusika. Hivyo basi, utafiti wa ngano kwa lengo la kubainisha mwonoulimwengu wa jamii ni msingi wa utambulisho wa jamii. Japo ngano za Wandia zilifanyiwa utafiti, tafiti nyingi ziliegemezwa kwenye masuala ya kijamii ambayo ni sehemu ya mwonoulimwengu wa Wandia bila kuibua taswira kamili ya mwonoulimwengu wao na kudhihirisha upekee wao. Utafiti huu ulilenga kujaza pengo hili kwa kutafitia usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa katika ngano zao ili kubainisha fasiri yao ya maisha na upekee wao kama jamii mahuluti.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

i. Kueleza jinsi mwonoulimwengu wa Wandia unavyojitokeza katika masimulizi yao.

ii. Kutathmini jinsi sauti ya simulizi na mtazamo zilivyotumiwa kufanikisha usimulizi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao.

**1.4 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo;

i. Je, mwonoulimwengu wa Wandia unabainika vipi katika ngano zao?
ii. Je, sauti ya simulizi na mtazamo zilitumika vipi kufanikisha mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao?

**1.5 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu ulinuiwa kumsaidia msomaji kuuelewa muundo wa ngano za Kiafrika kwa kuzingatia kipengele cha sauti ya simulizi na mtazamo. Utafiti utafaidi jamii ya wasomi kuelewa jamii nyingi za Kiafrika na kuongeza maarifa kuhusu fasihi simulizi ya Kiafrika. Utafiti ulinuiwa kuonyesha jinsi nyingine ya kuzichanganua ngano kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Tafsiri ya ngano teule kwa Kiswahili sanifu ilinuiwa kuwafaa walimu na wanafunzi katika viwango vya Sekondari na vyuoni kufundishia fasihi simulizi hususan mada ya ngano.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulinuiwa kushughulikia usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule. Fasihi simulizi ni uwanja mpana ambao unahusisha vipera kama vile semi, nahau, methali, nyimbo, maigizo na mazungumzo. Utafiti huu ulikitwa katika ngano kwa sababu kama walivyosema Webster na Mertova (2007), ngano ni chombo cha kufafanulia mwonoulimwengu wa jamii kwa sababu zinatokana na tajriba ya jamii. Ngano hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa sababu uchunguzi wa mtafiti wa awali ulibainisha kuwa maudhui makuu katika ngano hizi ni masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Japo kuna nadharia nyingi za uhakiki wa ngano, utafiti ulitumia nadharia ya naratolojia kwa sababu inahusisha hadithi na diskosi, yaani kile kinachosimuliwa na jinsi hadithi inavyowasilishwa. Hivyo basi hadithi katika utafiti huu ni mwonoulimwengu wa Wandia na diskosi ni nyenzo ambazo zilitumiwa kusimulia mwonoulimwengu. Nyenzo hizi ni sauti ya simulizi na mtazamo.

## 1.7 Machukulio

Ilichukuliwa kwamba ngano tano zilizoteuliwa zilikuwa na data ya kutosha kuhusu suala la mwonoulimwengu kwa jumla kwa sababu zilisheheni masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Aidha, ilichukuliwa kwamba fanani Wanjira wa Rukenya ni kiwakilishi tosha cha tajiriba ya Wandia na sauti ya simulizi ya kutoka nje katika usimulizi wa mwonoulimwengu wa Wandia. Vilevile, ilichukuliwa kwamba ngano teule zilikuwa kiwakilishi mwafaka cha mtazamo wa watunzi wa ngano za Wandia kuhusu suala la mwonoulimwengu wa jamii.

### 1.8 Maelezo ya Istilahi

**Daigesia:** Ni uwasilishaji wa usemi au matendo katika kazi ya fasihi kwa kuyaigiza. Ni istilahi iliyotumika kusimulia mwonoulimwengu katika ngano teule kwa kutumia mtindo wa maigizo. Mfano, katika nyimbo na maigizo baina ya wahusika.

**Fanani:** Neno hili linamaanisha mtu au sauti katika simulizi ambapo anawasilisha hadithi. Istilahi hii ilitumiwa kumrejelea fanani Wanjira wa Rukenya ambaye alitumiwa kuwasilisha ngano teule au sauti ya simulizi ya mwonoulimwengu wa Wandia.

**Mimesia:** Istilahi inayomaanisha namna ya uwasilishaji wa usemi au matendo katika kazi ya fasihi inayosisitiza maelezo ama kusimulia. Ni istilahi iliyotumika kusimulia mwonoulimwengu katika ngano teule.

**Msuko:** Mfuatano wa kimantiki wa visa na matukio katika ngano ambao huzingatia uhusiano wa kiusababishi. Neno hili lilitumika kuchunguza mfuatano wa visa na matukio kiusababishi katika usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia kutokana na ngano teule.

**Mwonoulimwengu:** Istilahi inayomaanisha fasiri ya uhalisia wa maisha uliokitwa kwenye utamaduni wa Wandia. Ni istilahi iliyotumiwa kuchunguza jinsi utamaduni wa Wandia unavyowawezesha kupata fasiri ya maana ya maisha kwa kuzingatia vigezo vya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

**Naratolojia:** Ni nadharia inayohusika na sifa na muundo wa ngano. Ni nadharia iliyotumika kuchunguza usimulizi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule.

**Ngano:** Ni maelezo ya mfuatano wa matukio kiusababishi. Aghalabu mfuatano huu huzingatia mpangilio wa kiwendo. Ni neno lililotumiwa kutoa maelezo ya msuko wa vitushi katika kila ngano teule hususan katika uchunguzi wa usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule.

**Uura:** Isitilahi ya lahaja ya kindia inayoashiria maji yenye utamu kama asali yaliyojitiririsha kutoka mtini. Uura uliliwa na

nguchiro. Hii ndiyo sababu ukaitwa uura wa nguchiro. Ulaji wa 'uura' ulinasibishwa na mikosi. Istilahi 'Uura' ilitumika katika utafiti huu kuchunguza dhana ya kutodhibiti nafsi pamoja na matokeo yake.

**Wandia:** Katika utafiti huu, istilahi Wandia ilimaanisha jamii ndogo ya kabila la Agikuyu wanoishi katika kaunti dogo ya Kirinyaga Magharibi na wanaozungumza lahaja ya Kindia. Istilahi hii ilitumiwa kuchunguza tajriba ya Wandia ambayo ndiyo chanzo hasa cha ngano teule zilizotumiwa katika uchanganuzi wa mwonoulimwengu wa Wandia.

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI NA MSINGI WA KINADHARIA.

## 2.1 Dhana ya Mwonoulimwengu

Kwa mujibu wa Kabira (1983), msanii ndiye chombo kinachotumiwa kuwasilisha thamani na falsafa za jamii inayohusika. Mtaalamu huyu amesisitiza umuhimu wa kumchunguza msanii katika muktadha wa jamii yake ili kuelewa falsafa ya jamii. Kazi ya mtaalamu huyu iliufaa utafiti huu kuelewa thamani za jamii ya Wandia ambazo ndizo chanzo cha ngano zao na falsafa ya maisha yao. Aidha, uchunguzi wa fanani Wanjira wa Rukenya katika muktadha wa jamii yake ya Wandia uliwezesha ufahamu wa mwonoulimwengu wa Wandia. Kwa upande mwingine, kazi ya Kabira (mtaje) ilitofautiana na utafiti huu kwa msingi kuwa Kabira (mtaje), alishughulikia usimulizi wa fanani Kabebe kutoka jamii ya Agikuyu kutoka Kanunga ilhali utafiti huu ulihusisha usimulizi wa fanani Wanjira wa Rukenya kutoka jamii ya Wandia.

Uchunguzi wa fasihi simulizi ni njia inayotumiwa na jamii kuelezea falsafa na thamani za jamii. Aidha ngano zinaweza kueleweka katika muktadha wa kijamii na uwasilishaji (Kabira na Mutahi, 1988). Wataalamu hawa wanaendelea kuelezea kuwa muktadha huu ndicho kigezo ambacho huibua mwonoulimwengu wa jamii iliyozizaa. Hapa ngano zinatumika kama msimbo wa elimu: Ufafanuzi wa elimu inayorejelewa na wasomi hawa ni mwonoulimwengu wa jamii ambao ni kiini cha utafiti huu. Japo wataalamu hawa wameshughulikia muktadha wa jamii na uwasilishaji, utafiti huu ulishughulikia mwonoulimwengu wa jamii ya Wandia kwa kuzingatia vigezo vya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Utamaduni wa watu ni kigezo muhimu katika ufahamu wa mwonoulimwengu wa jamii. Sababu ni kuwa watu wanaoshiriki utamaduni fulani ndio huelewa na kufasiri misimbo, falsafa na mifumo ya maisha ya jamii husika (Nyonje 2006). Mtafiti huyu ameelezea kuwa utamaduni una dhima ya utambulisho wa upekee wa watu fulani na ndicho kibainishi cha mwonoulimwengu wao. Utafiti wa Nyonje (mtaje) ulisaidia utafiti huu kuangazia elementi za utamaduni wa Wandia ambazo zinasawiri utambulisho wa Wandia miongoni mwa jamii zingine. Hata hivyo, tofauti kati ya utafiti wa Nyonje (mtaje) na huu ni kuwa utafiti wake ulihusisha utamaduni wa waswahili ilhali utafiti huu umehusisha utamaduni wa Wandia.

Masimulizi hujumuisha mwonoulimwengu wa watu. Webster na Mertova (2007) wameeleza kuwa sifa muhimu inayofanya ngano kuwa chombo muhimu cha kufafanulia mwonoulimwengu wa jamii ni kuwa ngano zinaibuka kutokana na tajriba ya jamii ambayo ni sehemu ya utamaduni wao. Aidha masimulizi ndiyo msimbo unaotumiwa na jamii kufafanulia ulimwengu wao. Wataalamu hawa wanashikilia kuwa mwonoulimwengu una uhusiano wa karibu na masuala ya kibinadamu wakati wowote wa matukio na tajiriba ya binadamu. Maoni ya wataalamu hawa yaliufaidi utafiti huu katika kubaini jinsi tajriba ya Wandia inavyoibua mwonoulimwengu wao. Kazi ya wataalamu hawa inatofautiana na hii kwa misingi kuwa walishughulikia stadi ya usimulizi ambayo inatumika kuibua mwonoulimwengu wa jamii ilhali utafiti huu ulitumia ngano kama njia ya kufafanulia mwonoulimwengu wa Wandia.

Uhusiano uliopo baina ya fasihi na urejelezi ni msisitizo kuwa fasihi sharti irejelee muktadha wake, yaani iliandikwa na mtunzi anayepatikana katika mazingira fulani ya kijamii, kitamaduni, kiuchumi, kisiasa, kijiografia na kihistoria. Aidha suala muhimu katika uhakiki wa ngano ni uchunguzi wa jinsi ulimwengu halisi unavyoakisiwa na kazi ya fasihi ( Wamitila, 2008). Mtaalamu huyu anaendelea kuelezea kuwa nguzo muhimu katika upangaji na utekelezaji wa sera na mikakati ya kuendeleza jamii ni ufahamu fika wa mwonoulimwengu wa jamii hiyo. Sababu ni kuwa mielekeo ya wanajamii kuhusu masuala mbalimbali yanaweza kudhihirika katika ngano zao kwa kuwa ngano huakisi utamaduni, mazingira na tajriba ya jamii husika. Kazi hii ilitumika kama dira ya kuangazia utafiti huu katika ubainisho wa jinsi ulimwengu halisi wa Wandia unavyoakisiwa na fasihi kwa kuzingatia ngano zao. Kazi ya Wamitila (mtaje) inahitilafiana na utafiti huu kwa sababu ilishughulikia uhusiano uliopo baina ya fasihi na urejelezi kwa jumla ilhali utafiti huu umeshughulikia kipera cha ngano za Wandia na urejelezi wa muktadha wa kijamii kwa lengo la kubainisha mwonoulimwengu wao.

Msanjila (1992), ametambua mojawapo ya njia za uhakiki wa ngano kuwa njia ya uhakiki wa kiujumi. Hii ni njia ambayo inachunguza ngano ili kubaini jinsi inavyotosheleza mahitaji ya kijamii, kitamaduni na kiroho. Msanjila (mtaje) amesisitiza kuwa uhakiki wa kiujumi unahakiki ngano kwa kuchunguza utendakazi wake katika muundo wa kijamii. Kazi ya mtaalamu huyu ilionyesha kuwa uhakiki wa ngano kwa kuzingatia misingi ya kiuamilifu una lengo la kuonyesha jinsi zinavyotekeleza matakwa

ya jamii. Mwonoulimwengu ni mojawapo ya mahitaji haya kwa kuwa ni falsafa inayotoa fasiri ya maisha kwa jumla na kuelezea utambuzi wa upekee wa jamii.

Kwa mujibu wa Chesaina (1994), fasihi simulizi ndio moyo wa njia ya maisha ya watu na roho ya utamaduni wao. Aidha, fasihi simulizi kwa kuwa ni hifadhi ya maadili ya watu inafafanua mwonoulimwengu wa jamii husika. Maoni ya mtaalamu huyu yalichochea haja ya kutafitia mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao kwa kuwa ngano hizi ni hifadhi ya maadili ambayo ni mojawapo wa vibainishi vya mwonoulimwengu wao. Hivyo basi, pana haja ya kutafitia mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao.

Kabira na Waita (2010) walishughulikia fasihi simulizi ya Wandia na kuandika kusanyiko la ngano ishirini na tatu zilizosimuliwa na fanani Wanjira Wa Rukenya. Katika kusanyiko hili, wataalamu hawa wameelezea kwa kifupi baadhi ya masuala kama vile; Wasifu wa fanani Wanjira Wa Rukenya, msanii na jamii, mitazamo ya kijinsia pamoja na mbinu na tamathali za lugha. Baadhi ya masuala haya ni sehemu ya fasiri ya mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia. Aidha mbinu na tamathali za lugha ni nyenzo zinazotumiwa kuwasilisha masuala haya. Kazi ya Kabira na Waita (mtaje) haijashughulikia masuala yote yanayohusishwa na fasiri ya mwonoulimwengu wa Wandia kwa jumla na hivyo basi kudhihirisha pengo la utafiti. Utafiti huu ulinuia kujaza pengo hili kwa kushiriki usimulizi wa ngano teule ambazo zilisimuliwa na Wanjira wa Rukenya ili kugundua usimulizi wa mwonoulimwengu wa Wandia. Aidha, uchanganuzi wa ngano hizi kwa misingi ya nadharia ya naratolojia uliwezesha kubainisha sauti ya simulizi na mtazamo, vigezo ambavyo vilidhamiriwa kufanikisha usimulizi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule.

Musungu (2016) alitambua jukumu muhimu linalotekelezwa na ngano za Wabukusu katika fasiri ya mwonoulimwengu wao. Aidha, mwasilishaji wa ngano za Wabukusu huathiriwa na kushawishiwa kwa kiwango kikubwa na utamaduni wake pamoja na hali za kijamii, kiuchumi, kijiografia na kihistoria. Musungu (mtaje) anaendelea kueleza kuwa ngano huumbwa kutokana na uoni wa msimulizi pamoja na utathmini wa mazingira yake ya kitamaduni, suala ambalo linazifanya ngano kuwa kioo cha uhalisia wa kijamii. Ngano za Wabukusu ni chombo ambacho kinatumiwa na Wabukusu katika

uumbaji wa mtazamo na mwonoulimwengu kuhusu uhalisia wa maisha. Utafiti wa Musungu (mtaje) ulisaidia utafiti huu kutathmini nafasi ya utamaduni wa Wandia katika kushawishi uwasilishaji wa ngano teule na Wanjira wa Rukenya. Aidha, utambuzi wa mazingira ya utunzi uliwezesha utafiti huu kuchukulia ngano za Wandia kuwa kioo cha jamii ambacho kinatumiwa kufasiria uhalisia wa kijamii pamoja na mwonoulimwengu wake. Hata hivyo, utafiti huu ulitofautiana na ule wa Musungu (mtaje) kutokana na misingi kuwa ngano za Wandia zinaibuka kutokana na tajriba na utamaduni wa Wandia, suala ambalo ni tofauti na utamaduni na tajriba ya Wabukusu.

Miriti (2016), alitafitia mwonoulimwengu wa Wamuthambi kwa kutumia kipera cha methali zao. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa methali za Wamuthambi ni chombo kinachotumiwa na jamii hii kufafanulia mwonoulimwengu wao. Utafiti wa mtafiti huyu ulitoa mchango kwa utafiti huu kwa kuwa ngano na methali ni vipera vya fasihi simulizi vinavyoibuka kutokana na tajriba ya jamii inayohusika. Hata hivyo utafiti wa Miriti (mtaje) unahitilifiana na huu kwa kuwa uwasilishaji wa methali ni tofauti na uwasilishaji wa ngano.

Muundo wa ngano za kiafrika unazingatia kaida ya kifreudia inayojihusisha na anasa dhidi ya uhalisia. Sheria hii inasawiri ukinzani kati ya anasa dhidi ya uhalisia, (Waita, 2019a). Uchunguzi wa Waita (mtaje) ulisaidia utafiti huu kuwezesha utambuzi wa dhana ya anasa na uhalisia; vigezo ambavyo ni msingi wa fasiri ya mwonoulimwengu wa watu katika jamii. Hivyo basi utafiti wa mtaalamu huyu ulichangia pakubwa usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao. Kazi ya Waita, (mtaje) inahitilafiana na utafiti huu kwa kuwa Waita (mtaje) aliongozwa na mtazamo wa kifreudia ilhali utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi mwonoulimwengu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa unavyobainika katika ngano za Wandia kwa kuzingatia shughuli mahususi, sauti ya simulizi na mtazamo katika ngano za Wandia.

Mgogoro wa kijinsia katika ngano za Akikuyu ni suala muhimu linaloongoza uhakiki wa mwonoulimwengu wa kijamii kwa misingi ya kijinsia, Waita (2019b). Mtaalamu huyu amebainisha kuwa ngano za jamii ya Agikuyu zilimsawiri mwanamume kwa baadhi ya taswira hasi kama vile; zimwi, kielelezo asili cha uovu na mtu mwenye uwezo wa kudhulumu wasichana na mlafi anayeweza kuangamiza jamii. Waita (mtaje),

aliegemeza kazi yake kwenye uhusiano wa nguvu za kijinsia na kupalilia itikadi ya kijinsia kwa mtazamo wa kike kinyume na itikadi ya kutawaliwa kwa wanawake na wanaume katika mawanda yote ya maisha. Utafiti wa mtaalamu huyu uliufaa utafiti huu kwa kuzingatia kigezo cha mkinzano wa kijinsia ambacho ni mojawapo wa vigezo vinavyotumika kufafanulia mwonoulimwengu wa jamii. Kazi ya Waita (mtaje) inahitilafiana na utafiti huu kwa misingi kuwa ilishughulikia kipengele cha taswira za mwanamume wa jamii ya Agikuyu ambacho ni kipengele kimoja tu cha fasiri ya mwonoulimwengu wa jamii ya Agikuyu ilhali utafiti huu ulilenga kubainisha mwonoulimwengu wa Wandia kwa kuzingatia vipengele vya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Mwauo wa maandishi kuhusu dhana ya mwonoulimwengu umebainisha kuwa mwonoulimwengu ni kigezo muhimu ambacho kinatumika kufafanulia maana ya maisha ya jamii kwa jumla. Aidha, mwonoulimwengu wa jamii unabainisha upekee wa jamii inayohusika. Ufahamu wa mwonoulimwengu ni dira ambayo ilitumika kuongoza uchunguzi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao.

## 2.2 Sauti ya Simulizi

Kimsingi sauti ya simulizi inarejelea fanani ama wakala wa simulizi anayejibu swali la je ni nani anayeongea? (Abbot,2002). Abbot (mtaje) amehoji kuwa, umuhimu wa kutambua anayechukua nafasi ya fanani ni kuwezesha hadhira kujua jinsi anavyoingiza kwa usimulizi matakwa na matarajio yake pamoja na udhaifu wake ili kuweza kuamini habari wanazopata kutoka kwake. Kwa mujibu wa Genette (1980: 186), sauti ya simulizi ni msemaji au sauti ya diskosi ya simulizi. Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kuwa sauti ya simulizi ndicho chombo kinachodumisha mtagusano wa kimawasiliano na hadhira kwa kuwa msimulizi ndiye huamua kitakachosimuliwa, jinsi kitakavyosimuliwa na kwa mtazamo upi. Iwapo sauti ya simulizi huamua jinsi ngano fulani itakavyowasilishwa, ina maana kuwa sauti ya simulizi inaweza kuamua mtazamo wa uwasilishaji wa ngano (Wafula, 2013: 58). Istilahi sauti ya simulizi inatekeleza dhima ya kubainisha wazi kwamba ni sauti ya fanani ama wakala wa simulizi anayeongea na sio sauti nyingine inayotekeleza wajibu wa kuongea katika usimulizi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule.

Uainisho wa sauti ya simulizi unategemea muundo wao wa kisarufi na mahali alipo fanani kuhusiana na hadithi. Muundo wa kisarufi unazua aina tatu za sauti ya simulizi, yaani sauti simulizi ya nafsi ya kwanza, pili na ya tatu (Cohan na Linda, 1988:90). Wataalamu hawa wametambua aina za sauti ya simulizi kama vile; sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ambayo inatumia nafsi ya kwanza ambapo fanani pia ni mhusika katika hadithi inayosimuliwa; sauti ya simulizi ya nafsi ya pili inayobainishwa kwa matumizi ya kiwakilishi cha nafsi "wewe" na; sauti simulizi ya nafsi ya tatu inayohusisha usimulizi wa nafsi ya tatu.

Uainisho wa pili wa sauti ya simulizi unahusu mahali alipo fanani kuhusiana na hadithi inayosimuliwa, mathalan, sauti ya simulizi ya ushiriki inayohusu msimulizi ambaye anapewa nafasi ya kusimulia hadithi ambapo yeye pia ni mhusika, yaani msimulizi anayeshiriki katika ulimwengu wa hadithi (Arege, 2012:139). Jahn (2005), ametumia istilahi ya usimulizi wa kindani na kuonyesha kuwa kibainishi cha usimulizi wa aina hii ni matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza; sentensi zinazoonyesha kuwa msimulizi angaa alishuhudia matukio yanayosawiriwa. Suala muhimu ni ufahamu kuwa msimulizi wa kindani pia ni mhusika katika simulizi hiyo (Wafula, 2013:65). Sauti ya simulizi ya kutoka nje inahusishwa na hadithi kusimuliwa na msimulizi kutoka nje ya ulimwengu wa hadithi, yaani msimulizi asiyepatikana kama mhusika katika hadithi na sentensi zote katika hadithi ni za nafsi ya tatu (Arege, 2012).

Sauti ya simulizi ni uumbaji ambao ulitumika katika utafiti huu kuelezea mwonoulimwengu kama sehemu ya elementi ya simulizi katika ngano za Wandia ili kubaini mwonoulimwengu wao. Hata hivyo, sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na ya tatu ndizo sauti za simulizi ambazo zilitawala usimulizi wa mwonoulimwengu katika ngano teule na zilitumiwa kusimulia mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao.

## 2.3 Mtazamo

Mtazamo ni dhana inayotumiwa kuelezea jinsi msimulizi anavyotazama hadithi yake pamoja na mahali anakotazamia hadithi hiyo, (Abbott, 2002). Mtazamo ndiyo miwani ambayo kwayo hadhira huona wahusika na matukio katika ngano. Fanani ndiye mtazamaji mkuu na hadhira huona tendo lenyewe kupitia kwa macho yake (Abbott, 2002:66). Jukumu la kimsingi la mhusika katika usimulizi ni kuchukua nafasi ya kuwa

kiakisi cha mtazamo ( Keen, 2003). Hapa mtazamo umepewa kipaumbele katika mchakato wa ufahamu wa yaliyomo katika simulizi. Maelezo haya yaliufaa utafiti kwa kuwa yalitoa mwanga zaidi kuhusu mtazamo wa fanani ambao ulinuiwa kufanikisha usadikishaji wa habari kuhusu mwonoulimwengu wa Wandia.

Wakala wa simulizi ana uwezo wa kuongea na kuona ama kufanya mambo yote mawili wakati mmoja (Rimmon-Kenan, 2002). Uoni huu ndio unaorejelewa kuwa mtazamo. Kimsingi, kuna mitazamo miwili; mtazamo wa ndani unaohusishwa na msimulizi wa nafsi ya kwanza ama msimulizi ambaye pia ni mhusika na; mtazamo wa nje unaohusishwa na msimulizi ambaye hashiriki katika hadithi fulani, (Wamitila, 2003; Rimmon-Kenan, 2002). Kituo cha mtazamo wa ndani kimo ndani ya matukio yanayowakilishwa ilhali mtazamo wa nje unategemea mwono wa msimulizi, Rimmon-Kenan (mtaje).

Kulingana na Rimmon- Kenan (2002), Mtazamo umegawika katika sura nne kama vile utambuzi, akili, hisia na itikadi. Sura ya utambuzi inahusisha kuona, kusikia na kunusa, masuala ambayo yanatawaliwa na nafasi na wakati. Nafasi inahusu mahali alipo mtazamaji mwenye mtazamo wa ndani au nje huku kipengele cha wakati kikihusishwa na mtazamo wa ndani unaohusu habari zinazodhibitiwa na mtazamaji mwenye mtazamo wa nje. Mtaalamu huyu anaendelea kusema kuwa, sehemu ya akili inahusu maarifa, utambuzi, imani na kumbukumbu. Kimsingi mtazamaji mwenye mtazamo wa nje anajua kila kitu kuhusu ulimwengu unaowakilishwa. Maarifa ya mwenye mtazamo wa ndani ni finyu kwa sababu yeye ni sehemu ya ulimwengu unaowakilishwa na hawezi kujua kila kitu kuuhusu, (Rimmon-Kenan, mtaje). Sehemu ya hisia ilikitwa katika mabadiliko ya kihisia. Hatimaye, kuna sehemu ya kiitikadi inayojihusisha na mfumo wa kijumla wa kutazama ulimwengu na kuufasiri. Itikadi ya mtazamo wa Fanani ina mamlaka kuliko itikadi zingine katika hadithi na zinatathminiwa kutokana na nafasi hii ya juu. Mitazamo ya msimulizi na ya wahusika ilitumika katika utafiti huu kufafanulia mwonoulimwengu wa jamii ya Wandia katika ngano zao.

### 2.4 Historia Fupi ya Wandia

Fasihi simulizi kuhusu asili na historia ya Wandia ilikitwa kwenye mitazamo miwili ambayo ni mtazamo wa kisasili cha Gikúyú na Mumbi na ule wa msambao. Mtazamo

wa kwanza unaoendelezwa na Leakey (1977a), unashikilia kuwa jamii ya Agíkúyú ikiwemo jamii ndogo ya Wandia ilianzishwa na mwanamume mmoja (Gikúyú) na mwanamke mmoja (Múúmbi), walioumbwa na mwenyezi Mungu na kuwekwa katika Múkúrwe wa Nyagathanga, sehemu iliyopo kaunti ya Murang`a kaskazini mwa Mto Chania. Mtazamo wa pili unaelezea kuwa asili ya Agikuyu ni msambao wa Agikuyu kuelekea kaskazini mwa Metumi na Kusini mwa Gaki katika karne ya kumi na saba.

Chanzo cha msambao huu kilikuwa ugomvi wa ndani uliosababisha uvamizi wa kiwango kikubwa (Muriuki, 1974). Wahamiaji wa kiasili walikongamana Sagana sehemu iliyoko katika eneo bunge la Ndia. Kisha walizagaa katika sehemu mbalimbali za mlima Kenya. Wahamiaji wa kiasili waliosalia hapo sagana walizaana na kisha kuenea katika sehemu zingine za Ndia na kuunda jamii ya Wandia wanaotambulishwa kwa lahaja ya Kindia na upekee wa mwonoulimwengu wao kuhusu maisha uliokitwa kwenye utamaduni wao (mtaje). Ngano ni mojawapo wa misimbo ya fasihi simulizi unaotumiwa kufafanulia mwonoulimwengu wa Wandia. Uelewa wa Wandia, utamaduni pamoja na Ngano za Wandia ambazo ni sehemu ya utamaduni wao uliufaa utafiti huu kuchanganua mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao.

**2.5 Ngano**

Istilahi ngano inatokana na neno la kisanskriti ya zamani `*gna*` lenye mzizi unaomaanisha `kujua` na kwamba inatufikia kupitia kwa istilahi ya kilatini `*gnarus*` yenye maana ya kufahamu na kuambia (*naro*). Etimolojia hii inaafiki pande zote mbili za ngano, yaani kusimulia ukiwa na lengo la kufahamisha (White, 1987 ). Kwa mujibu wa White (mtaje), ngano husimulia mfuatano wa matukio ambayo ni muhimu kwa msimulizi pamoja na hadhira yake. Hii ina maana kuwa usimulizi hukitwa kwenye muktadha wa kijamii (Wertsch, 1981).

Ngano haziwezi kuchukuliwa kama miundo ya kidhahania iliyojitenga na miktadha ya kitamaduni. Lazima zionekane kama kwamba zilikitwa katika jamii na kama tajriba ambayo inawasilishwa na watu katika miktadha ya kitamaduni (Bruner, 1984). Kwa mujibu wa Miruka (1994), ngano ni maelezo ya kinathari kuhusu watu, matukio, mahali n.k. ambayo yanaweza kuwa ya kweli au ya kubuni na hupitishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya mdomo. Fasiri hii ya Miruka (mtaje) iliegemezwa kwenye

kipengele cha tajriba ya jamii na jinsi ya uwasilishaji. Abbott (2002), ametoa fasiri ya ngano kwa kutumia misingi ya vigezo viwili, yaani, uwakilisho wa matukio unaohusisha hadithi na diskosi na uwasilishaji au utambaji wa ngano. Mawazo ya Abbott (mtaje) yalisisitiza dhima ya tajriba ya jamii pamoja na uwasilishaji kwa njia ya mdomo.

Baadhi ya ngano hugusa mifumo ya imani ya watu, mielekeo kuhusu maisha na utafutaji wa maana ya maisha (Odaga, 1984). Mawazo ya Odaga (mtaje) yalichangia uchanganuzi wa mwonoulimwengu katika ngano teule kwa kuwa imani, mielekeo na maana ya maisha ni vipengele vya kimsingi katika usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia kutokana na ngano teule. Ngano haziibuki kutokana na ombwe tupu bali ni zao la tajriba ya jamii (Webster na Mertova, 2007). Mawazo ya wataalam hawa yaliwezesha utambuzi wa kuwa ngano teule ni zao la tajriba ya Wandia. Wakichangia suala la tajriba, Kabira na Mutahi (1988) Walibainisha kuwa uchunguzi wa ngano ambao umekitwa kwenye muktadha wa kijamiii na uwasilishaji unaibua mwonoulimwengu wa jamii iliyozizaa. Hapa muktadha wa kijamii ulilenga tajriba hasa ya jamii lengwa ya Wandia. Ngano ni mojawapo ya njia ambayo kwayo tunafahamu ulimwengu katika wakati hivi kwamba ufahamu huu umekitwa katika jinsi tunavyouona (Abbott, 2002). Maoni haya yalisaidia utafiti kuchunguza mwonoulimwengu wa Wandia kwa kuuweka katika muundo wa ngano na kuzingatia tajriba yao ya maisha.

Vansina (1985) amehusisha ngano na dhana mbili: Mchakato na matokeo; yaani uwasilishaji wa ujumbe kwa njia ya mdomo na kuwa na matokeo ya ujumbe wa mdomo. Vansina (mtaje) ameendelea kueleza kuwa ujumbe wowote ni zao la jamii na hutumika katika usuluhishaji wa migogoro, matumizi ya kiitikadi na udhanishaji. Maoni haya yalisaidia kuchunguza mwonoulimwengu wa Wandia kwa misingi ya usuluhishi wa migogoro, itikadi na udhanishaji. Ngano zinapaswa kuchukuliwa kama sehemu ya miktadha ya kijamii ambayo iliziumba ili kufahamu uamilifu wa ngano katika miktadha ya kijamii.

## 2.6 Ngano za Wandia

Ngano za Wandia ni hadithi za kubuni ambazo zilitungwa na watunzi wa jamii ya Wandia kwa lengo la kuburudisha, kuelimisha na kuadilisha. Ngano hazitokani na ombwe tupu bali ni zao la tajriba ya jamii iliyozizaa (Webster na Mertova 2007). Kwa kuongozwa na mantiki hii, ilibainika kuwa ngano za Wandia ni zao la tajriba ya Wandia inayojumlisha mwonoulimwengu, mwenendo, Imani, thamani, maadili, n.k. Ngano ni mali ya jamii na haziwezi kumilikiwa na mtu binafsi. (Akivaga na Odaga, 1982). Hivyo basi, ngano za Wandia ni mirathi ya Wandia na sio mali ya mtu binafsi.

Kabira na Waita (2010), walinasibisha kusanyiko la ngano ishirini na tatu na fanani Wanjira wa Rukenya. Utambulisho huu ulitokana na stadi pamoja na tajriba ya kutamba ngano. Hata hivyo Waita (2003) alitambua kuwepo kwa fanani wengine katika jamii ya Wandia kama vile Jecinta Wangithi na Irene Wanjiru. Wanjira alipokezwa ngano na mama yake pamoja na *nyanya* yake ambao walikuwa na kipawa cha utambaji wa ngano (Kabira na Waita, 2010). Dhana ya upokezaji wa ngano ina mshabaha na kazi ya Miruka (1999) anapodokeza kuwa ngano ni masimulizi ya kinathari yanayopokezwa kizazi hadi kizazi kwa njia ya mdomo. Hivyo basi, dhana ya upokezaji wa ngano kutoka kwa *nyanya* na mama hadi kumfikia Wanjira wa Rukenya ni ithibati tosha kuwa Wanjira wa Rukenya hamiliki ngano zozote bali ngano zenyewe ni mali ya Wandia. Ngano teule zilizotumika kuchanganua mwonoulimwengu wa Wandia zilisheheni tajriba ya Wandia.

Aghalabu ngano huwa na fomula ya kuanza na kumalizia (Akivaga na Odaga, 1982). Fomula ya kuanzia hulenga kuteka makini ya hadhira na kuanzia utayari wa hadhira kutambiwa ngano. Kwa mujibu wa Kabira na Waita, (2010), upekee wa ngano za Wandia unadhihirika katika fomula ya kuanzia na kumalizia mfano;

Msimulizi: Semeni `*itho!*`
Hadhira: `*itho!*`
Msimulizi: Hapo zamani za kale

Vivyo hivyo fomula ya kumalizia inasisitiza upekee wa ngano za Wandia. Mfano, Wanjira wa Rukenya huhitimisha ngano zote kwa ``*mundu utagana aroria gatutu, na niĩ ngaria gaturume ka baba gaitaga maguta* Ca! Ca! Ca! Ca! inayomaanisha ``mtu

asiyetamba ngano na ale nguchiro nami nikila kondoo wa baba anayechirizisha mafuta Ca! Ca! Ca! Ca!.

Ngano za Wandia zinatumia wahusika kuendeleza msuko (Waita, 1995). Wamitila (2008) ameainisha wahusika katika makundi mawili; Binadamu na wanyama. Wamitila (mtaje) ameelezea kuwa wahusika ni watu, wadudu, miti, mashetani na majini wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upashaji wa ujumbe.

Maudhui katika ngano ni kipengele muhimu. Ngano za Wandia zilisheheni maudhui kama vile; mapenzi, uchumba, ndoa, masuala ya kijinsia, kilimo, ufugaji, uhunzi, uongozi, migogoro, na kadhalika.  Maudhui haya yalikitwa kwenye tajriba ya Wandia na ndio msingi wa uchanganuzi wa mwonoulimwengu katika ngano teule.

Mtindo ni kipengele muhimu katika kazi ya sanaa (Akivaga na Odaga, 1982). Watunzi wa ngano za Wandia wametumia mbinu za kimtindo kama vile; taswira, methali, jazanda, semi na taharuki miongoni mwa mitindo mingine (Waita, 1995; Mugambi na Waita, 2016). Mwauo wa maandishi kuhusu ngano za Wandia ulisaidia utafiti katika uteuzi wa ngano teule kwa kuongozwa na vipengele vya kimaudhui vilivyochangia uchunguzi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule.

## 2.7 Mfumo wa Maisha wa Jamii ya Wandia

Mfumo wa maisha wa jamii ya Agikúyú ni suala changamano linalosheheni masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Mfumo huu umefungamanishwa na dini ya Agikúyú, (Mbiti, 1969). Kwa mujibu wa Mbiti (mtaje), dini ya Waafrika ilijipenyeza kwenye mawanda mengine yote ya maisha hivi kwamba ilikuwa vigumu kutenganishwa. Suala hili linaungwa mkono na Leakey (1977b), anaposisitiza kuwa dini ya Agikúyú ilitekeleza majukumu mawili muhimu; Mosi, kudumisha maisha na utangamano wa familia na pili; kigezo cha utambulisho kuwa Mkikuyu. Utambulisho unaorejelewa hapa ni upekee wao ambao unatambulishwa kwa mwonoulimwengu wao wa maisha kijumla.

Msingi wa maisha wa jamii ya Agikúyú ni familia. Aidha, familia ilikuwa kituo cha dini na elimu ya kitamaduni iliyowasilishwa kwa kutumia ngano zenye mafunzo.

Watoto pia walifunzwa kwa kushirikishwa katika kazi zilizofanywa na wazazi wao, kwa mfano kupika kwa wasichana na kuchunga mifugo au kulinda jamii kwa wavulana (Leakey, 1977a). Ngano zilitumika kama chombo cha kupokezana elimu ya kidini na kitamanduni kwa watoto. Dhamira ya elimu hii ya kijadi ilikuwa kupokezana mwonoulimwengu wa jamii. Utafiti huu ulilenga kutathmini jinsi ngano za Wandia zinavyotumika kama njia ya kufafanulia na kupokezana mwonoulimwengu wao.

Kigezo kingine muhimu cha kutathminia mwonoulimwengu wa jamii ni uchumi wa jamii inayohusika. Uchumi wa Agikúyú ulijengeka kwenye kilimo, ufugaji na biashara (Munene, 1995). Kwa mujibu wa Kenyatta (1938), kila familia ilichukuliwa kuwa kitengo cha kiuchumi kwa kuwa ilijukumika kuzalisha mali ili kutimiza mahitaji yote ya familia. Mtaalamu huyu anaendelea kuelezea kwamba uzalishaji mali ulishurutisha kugawa majukumu ya kijamii kulingana na umri na jinsia. Aidha, katika nyanja za biashara, mbuzi na kondoo walitumika kama sarafu ya kawaida licha ya kuweko kwa biashara ya kubadilishana bidhaa.

Agikuyu kimsingi walikuwa wakulima stadi. Baadhi ya vyakula vilivyokuzwa kabla ya ujio wa Wakoloni ni kama vile: ndizi, viazi vitamu, viazi vikuu, mawele, wimbi, fiwi, mbaazi, wanga na njegere. Mahindi yalianza kukuzwa mwishoni mwa karne ya kumi na nane na mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa (Leakey, 1977a). Baada ya ujio wa wamishonari na walowezi, mazao ya fedha kama vile kahawa, chai, mpunga na pareto yalianza kukuzwa na Agikuyu wakiwemo Wandia. Agikúyú walikuwa wamezama kwenye kilimo hivi kwamba mwaka uligawanywa katika misimu miwili: msimu wa fiwi na msimu wa mtama. Ni dhahiri kuwa kilimo na ufugaji ni mambo mawili yaliyosisitizwa na jamii ya Agikúyú kutokana na msingi kwamba bidhaa za kimsingi katika miviga ya Agikúyú zilitokana na shughuli za ukulima na ufugaji (Munene, 1995).

Maarifa kuhusu mfumo wa kiuchumi wa Agikuyu uliwezesha uchanganuzi wa masuala nyeti yanayohusiana na uchumi wa Wandia kwa sababu wao ni sehemu ya jamii pana ya Agikuyu. Hivyo basi ulingano wa shughuli za kiuchumi katika jamii pana ya Agikuyu na hii ya Wandia ulitumika katika utafiti huu kama msingi mwafaka wa uchanganuzi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao.

Mfumo wa kisiasa wa jamii ni suala muhimu ambalo kwalo mwonoulimwengu wa jamii hubainika. Mathalan, katika kiwango cha uongozi wa mbari, kamati ya mbari iliyoongozwa na mtawala wa jina tu (*múramati*) iliwajibikia uongozi wake (Muriuki, 1974). Kwa mujibu wa Muriuki (mtaje), '*Kiama*' kilichojumlisha wazee wakomavu waliostaafu kutoka kwenye kikosi cha vita na ambao wameoa kilitwikwa mamlaka ya juu sana na kilijihusisha na majukumu ya kuunda sheria, uendeshaji wa serikali, na kuamua kesi. Mtaalamu huyu anaendelea kuelezea kuwa, jukumu muhimu mno la "kiama" lilikuwa uamuzi wa kesi, jambo lililotekelezwa na wakadiriaji wa "*kiama*".

Ufahamu wa mfumo wa kisiasa wa Wandia uliusaidia utafiti huu kuelewa mihimili ya mfumo wa kisiasa wa Wandia kwa lengo la kuhakiki mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia katika ngano zao. Mihimili hii ni kama vile usuluhishi wa migogoro, uongozi,kushirikisha umma katika miradi ya maendeleo na kuzingatia haki miongoni mwa masuala mengine.

**2.8 Utamaduni wa Wandia**

Utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za jamii fulani, (TUKI, 2018: 703). Maelezo haya yanaonyesha kuwa utamaduni unahusishwa na jamii fulani na sio mtu binafsi. Utamaduni wa jamii hubainisha upekee wa watu hao na upekee huu ndio hudhihirisha mwonoulimwengu wao kuhusiana na mawanda yote ya maisha.

Wandia wana utamaduni wao ambao unatumika kuonyesha upekee wao kama jamii na fasiri ya mwonoulimwengu wao (Waita, 2021). Mtaalamu huyu ametambua kuwa baadhi ya elementi za utamaduni wa Agikuyu zinadhihirika kupitia ngano zao ambazo ndizo chombo cha kupokezana utamaduni huu. Elementi hizi ni kama vile: mfumo wa kuwapa watoto majina, uchumba , ndoa; na kuadhibu wanawake wakaidi.

Utamaduni wa Agikúyú wakiwemo Wandia, unaanza pindi tu mtoto anapozaliwa. Kabira na Waita (2010) wamebainisha kuwa mtoto anapozaliwa, hupewa jina kwa kufuata mwongozo wa utamaduni wa Agikúyú. Mathalan; mtoto wa kwanza wa kiume hupewa jina la babu kuumeni na akiwa wa kike hupewa jina la *nyanya* kuumeni. Mtoto wa pili wa kiume hupewa jina la babu kuukeni na iwapo wa kwanza alikuwa wa kike, wa pili wa kike, atapewa jina la *nyanya* kuukeni. Watalaamu hawa wanaendelea

kuelezea kuwa, utamaduni wa Wandia ulisisitiza elimu ya kijadi. Elimu ya kisasa kwa wasichana ilihusishwa na umalaya. Aidha msichana aliyesoma ingemwia vigumu kupata mume, jambo ambalo lilikuwa sawa na kumnyima babake nafasi ya kupokea mahari.

Suala muhimu kuhusiana na maisha ya kijadi ya Agikúyú ni kutahiriwa kwa wavulana na kupashwa tohara kwa wasichana (Kenyatta, 1938; Muriuki, 1974). Tohara iliwapa vijana wa kiume na wa kike kibali cha kushiriki densi pamoja. Ubikira ulikuwa kigezo muhimu katika maandalizi ya ndoa hivi kwamba msichana akienda densini angefungwa kikaza na mama yake. Waita (2021) ameeleza kuwa yeyote ambaye angefungua kikaza hiki angeshurutishwa kumwoa. Aidha, msichana yeyote ambaye angekubali kikaza chake kifunguliwe angedhihakiwa na jamii.

Jamii ya Agikúyú ilisisitiza suala la ndoa kwa kila mwanajamii (Waita, 2021). Msichana aliyeolewa akiwa bikira aliimba wimbo wa '*kĩrĩro*' kwa kuwa kuanzia wakati huo, angepoteza uhuru wake (Kabira na Waita, 2010). Aidha kulikuwa na ndoa za kupangwa ambapo msichana angebebwa hobelahobela na wavulana na kupelekwa kwa mumewe, ( Kabira na Waita Mtaje).

Baadhi ya mihimili ya utamaduni wa Agikúyú wakiwemo Wandia ambayo ilishughulikiwa hapa ni dira ambayo ilitumiwa kuongoza uchanganuzi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao. Ngano ni chombo ambacho kinatumiwa kuelezea mwonoulimwengu wa jamii ambao umekitwa kwenye utamaduni wa jamii husika (Webster na Mertova, 2007). Hivyo basi, ufahamu fika wa utamaduni wa Wandia uliufaa utafiti huu kuelezea mwonoulimwengu wa Wandia kwa ujumla wake.

### 2.9 Historia Fupi ya Fanani Wanjira Wa Rukenya

Suala muhimu mno katika uwasilishaji wa ngano ni nafasi ya fanani. Kabira (1983) ameelezea kuwa fanani anachukuliwa kuwa kiungo cha kati katika uwasilishaji wa ngano kwa kuwa msanii huakisi thamani, matumaini na maratajio ya jamii. Ukamilifu wa kazi ya sanaa umekitwa kwenye uwasilishaji na unapokosekana thamani halisi ya kiumbuji haiwezi kueleweka (Kabira, mtaje). Mtafiti huyu anaendelea kueleza kuwa

kila uwasilishaji unakuwa mpya na mchakato wa umbuji unashawishiwa na wakati, mahali pa uwasilishaji, hadhira, umri wa hadhira, idadi ya hadhira na mazingira ya uwasilishaji. Aidha, fanani anachangia pakubwa kwa kuwa anachukuliwa kuwa kiungo cha kati katika uwasilishaji wa ngano kwa kuwa msanii huakisi thamani, matumaini na matarajio ya jamii (Kabira, 1983). Kazi ya Kabira (mtaje) iliwezesha utafiti huu kuchunguza kipengele cha uwasilishaji na msanii pamoja na data kuhusu hadhira.

Kwa mujibu wa Kabira na Waita (2010), fanani Wanjira wa Rukenya alizaliwa 1937 katika kijiji cha Mukitho, Baricho, kaunti ndogo ya Kirinyaga Magharibi, eneo la kati nchini Kenya. Fanani huyu alijifunza utambaji kutoka kwa *nyanya* yake mzaa baba na mama yake waliokuwa na kipawa cha utambaji wa ngano. Wataalamu hawa wanaendelea kuelezea kuwa shughuli ya utambaji wa ngano ilitendeka jioni watoto walipokuwa wakingoja chakula kiive.

Mugambi na Waita (2016) wamethibitisha kuwa mbinu za kimtindo na kisanii zinazousawiri upekee wa fanani Wanjira wa Rukenya ni: Mdukizo, unaowezesha kutoa ufafanuzi kwa hadhira na kuhamasisha hadhira shirikishi; maigizo kati ya wahusika yanayosaidia ujenzi wa wahusika ili kuzipa ngano zake uyakinifu; matumizi ya njozi inayowezesha fasiri ya jambo ngumu kuwa rahisi kwa kuwasilisha njozi kama uhalisia; tanakali za sauti zinazotumika kuunda taharuki na kusisitiza ujumbe na; nyimbo na uradidi zinazotumika kuendeleza msuko na kufanya hadithi ifikie kilele. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, matumizi ya mbinu hizi za mtindo wa uwasilishaji wa ngano ndizo zinazodhihirisha upekee wa fanani Wanjira wa Rukenya na ndicho kichocheo kikuu cha kumshirikisha katika usimulizi wa ngano teule.

Ufahamu wa wasifu wa fanani Wanjira wa Rukenya uliwezesha utafiti huu kumchunguza Wanjira wa Rukenya katika muktadha wa jamii yake ya Wandia. Sababu ni kuwa fanani ana sifa mbili kuu: sifa ya kuwa sauti ya simulizi pamoja na ile ya kuwa mwenye mtazamo (Bal, 1997). Sifa hizi mbili ndizo msingi ambao ulifanikisha uwasilishaji wa usimulizi wa mwonoulimwengu katika ngano za Wandia. Suala hili lilichukuliwa kuwa msingi wa uchanganuzi wa mwonoulimwengu wa wandia kijamii, kiuchumi na kisiasa katika ngano teule.

## 2.10 Usawiri wa Wahusika Katika Ngano

Usawiri ni istilahi inayomaanisha taswira za wahusika wa fasihi zinazoundwa na wasanii ili kuwasilisha tabia na matendo mbalimbali ya binadamu katika Maisha halisi. Istilahi hii inatumika zaidi na wahakiki kuchambua kazi za fasihi hasa kipengele cha wahusika (Kawia, 2015). Kwa mujibu wa Wamitila (2003), taswira ni picha inayoumbika mawazoni mwa msomaji ama mtazamaji wa kazi za fasihi.Wamitila (mtaje) amebainisha aina za taswira kama vile; taswira mwendo, taswira uoni, taswira mwonjo, taswira Sikivu na taswira  hisi.

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya fasihi. Matendo ya viumbe hawa hufanana na yale ya binadamu. Waita (1995), ameelezea kuwa wahusika wanachangia pakubwa katika uumbaji wa msuko. Matendo ya wahusika ndiyo msingi wa ufahamu wa usawiri wa wahusika katika ngano. Mtaalamu huyu ameendelea kufafanua kuwa uumbaji wa wahusika unazua athari fulani kwa hadhira ambayo hutokana na hali kwamba ulimwengu wa ngano umeumbika kutokana na ulimwengu halisi. Kazi hii iliufaa utafiti huu kubainisha jinsi usawiri wa wahusika katika ngano za Wandia unavyosawiri mwonoulimwengu wao.

Wahusika ni watu, wanyama, wadudu, miti, mashetani na majini wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upashaji wa ujumbe. Aidha, kuna aina mbili za wahusika: binadamu au wanyama ambao wamepewa sifa za binadamu (Wamitila, 2008). Mtaalamu huyu ameeleza kuwa katika usimulizi wa hadithi, mpaka uliopo kati ya ulimwengu wa kawaida wa binadamu na wanyama hufutwa. Si ajabu basi kuwa binadamu wanaweza kutagusana, kujadiliana, kuzungumziana na kuhusiana kwa jumla na wanyama.

Wahusika ndio huipa hadithi kusudi na msukumo wa hadhira kutaka kujua kinachoendelea. Aidha, usawiri wa wahusika ndicho kigezo muhimu zaidi katika ngano, (Reams, 2015). Isitoshe, mtaalamu huyu anaendelea kuelezea kuwa matendo ya mhusika katika hadithi yanadhihirisha wao ni wahusika wa aina gani. Kazi ya mtaalamu huyu iliufaa utafiti huu kwa kuwezesha uchanganuzi wa mwonoulimwengu wa Wandia kupitia usawiri wa wahusika katika sampuli ya ngano teule.

Kipengele cha usawiri wa wahusika kilitumika kuongoza usimulizi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule. Umuhimu wa wahusika katika ngano unatokana na uwakala wa simulizi unaowezesha wahusika kuchangia hadithi kwa njia yenye maana. Hivyo basi uwakala wa uhusika unampa mhusika sababu ya kufanya mambo. Mhusika anapofanya hivyo anashawishi ulimwengu wa hadithi na kuendeleza ploti. Aidha usawiri wa wahusika uliufaa utafiti huu kwa kubainisha mtazamo wa wahusika ambao ni msingi wa ubainisho wa mwonoulimwengu wa jamii.

### 2.11 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya naratolojia kwa sababu utafiti ulichunguza usawiri wa mwonoulimwengu katika ngano za Wandia. Kimsingi nadharia ya naratolojia inachunguza sifa za muundo wa ngano kwa kugawa vipengele vya simulizi na kuzingatia uamilifu na uhusiano uliopo. Suala la kimsingi katika naratolojia ni kutalii muundo wa ngano na kwa kufanya hivyo kuna haja ya kuchunguza sehemu mbalimbali za muundo na kufafanua uhusiano uliopo baina ya sehemu hizo (Ong`ondi, 2005).

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), nadharia ya naratolojia iliegemezwa kwenye misingi ya mawazo ya mwanafalsafa wa Kiyunani, Plato (428-348kk). Mawazo haya yanapatikana katika maandishi ya *The Republic III* (1943) ambapo alitumia dhana mbili za kimsingi ambazo ni mimesia na daigesia. Katika mimesia msimulizi hajitokezi wazi ilhali katika daigesia msimulizi anajitokeza waziwazi na kutambulika. Dhana ya Mimesia ilipanuliwa na mwanafunzi wa Plato aitwaye Aristotle kwa kuihusisha na maelezo (Mtaje). Kulingana na Aristotle, kipengele cha kueleza kina sifa ya Ki-mimesia au simulizi.

Aristotle, katika andiko la *The Poetics* (1961) amebainisha kuwa mhusika na kitendo ni vipengele muhimu katika hadithi na kusema kwamba tabia ya mhusika sharti ionyeshwe kupitia ploti (Habib, 2011). Naratolojia ilichipuka kutokana na nadharia ya umuundo ya Kirusi iliyoasisiwa na Propp (1928). Katika *The Morphology of The Folktale*, Propp alichunguza hurafa zaidi ya mia moja na kutambua kuwa matukio tofauti yalikuwa yamepangwa kwa mfuatano maalumu wa kiusababishi. Matukio haya aliyaita vihimili na mfuatano huu akautambulisha kama msuko.

Shughuli mbalimbali kuhusu nadharia ya kimuundo zilianza kuchukua mkondo maalum baada ya 1958 hususan baada ya tafsiri ya kazi ya Propp ya *The Morphology of The Folktale*. Nadharia ya naratolojia ilikita mizizi mwaka wa 1966 baada ya uchapishaji wa Makala maalum *`Communications`* yaliyotengewa uchambuzi wa muundo wa hadithi. Istilahi naratolojia inatokana na istilahi ya Kifaransa `naratologie` iliyobuniwa na Tondorov (1969) ambaye alitetea mabadiliko ya mwelekeo wa uhakiki wa matini ya ngano kutoka kiwango cha juu juu hadi kiwango cha diskosi thabiti ya mantiki ya jumla ya muundo wa ngano.

Raglan (1936), anahusishwa na ukuaji wa nadharia ya naratolojia. Katika kazi yake "*The Hero",* alichunguza visasili kutoka jamii mbalimbali na kugundua motifu ishirini na mbili katika maisha ya mashujaa wa kitamaduni. Motifu hizi huwa zimepangwa kwa mfuatano maalum; mathalan, kuzaliwa kwao hutanguliwa na matukio maalum ya kushangaza, wanafanyiwa jaribio la kuuawa, wanaenda kuishi mbali na kwao, hukumbana na majaribio mengi, hurejea baadaye na kukomboa jamii yao na kufa kwao hutokana na usaliti. Mawazo haya yalitumika kama msingi wa uchanganuzi wa motifu ya mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule.

Naratolojia ni nadharia, ambayo inajihusisha na sifa ambazo zinafafanua matukio, muundo wa matukio na mfuatano wa visa kiusababishi au maudhui yake (Wamitila 2002). Aidha, inashughulikia aina za wasimulizi na mbinu za usimulizi zinazotumika kusimulia ngano (Abrams, 1999). Ufaafu wa nadharia ya naratolojia ni kusaidia kuelewa, kuchanganua na kutathmini ngano (Bal, 1999). Inasaidia kufafanua ngano kwa kutoa maelezo ya matukio fulani na mfuatano halisi au ya kibunilizi na kutambua kuwa hadithi hutambwa kwa njia mbalimbali kama vile kusimuliwa kwa njia ya nathari, ushairi, maandishi au simulizi (Wamitila, 2002). Kulingana na Bal (1999), naratolojia huchunguza mfuatano wa matukio katika matini kiwakati na kwamba mbinu mbalimbali za kisimulizi kama vile mbinu rejeshi au mbinu elekezi husababisha matukio kutofautiana kiwakati.

Nadharia ya naratolojia inashughulikia jinsi mbalimbali za kuwasilisha matukio katika matini yoyote ya simulizi. Jinsi hizi ni mimesia (uelezaji) na daigesia (uonyeshaji). Aidha matukio yanaweza kusimuliwa baada ya kutokea, kabla ya kutokea ama wakati huo yanapotokea (Wamitila, 2002). Nadharia ya naratolojia inajumlisha dhana mbili za

kimsingi, yaani hadithi na diskosi (Rimmon-Kenan, 2002). Naratolojia iliweza kutenganisha hadithi na diskosi, yaani, kile kinachosimuliwa na jinsi hadithi inavyowasilishwa (Hogan, 2013). Hadithi katika utafiti huu inahusu suala la usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia kama sehemu ya kipande cha ngano teule ambazo zilihusika na utafiti huu. Diskosi katika utafiti huu ni nyenzo ambazo zilitumiwa kuwasilisha suala la mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao. Baadhi ya nyenzo hizi ni kama vile usimulizi, sauti ya simulizi na mtazamo.

Wananaratolojia wamedhihirisha umuhimu wa masimulizi, namna mbalimbali za kuwasilisha hadithi, wakati na nafasi ya wahusika katika kujenga msuko na kuendeleza hadithi. Wamebainisha umuhimu wa nadharia ya naratolojia katika kutoa mwongozo wa kuhakiki matini ya simulizi. Nadharia ya naratolojia iliufaa utafiti huu kwa vile uchunguzi wa kinaratolojia unahusisha hadithi, msimulizi, njia na jinsi ya kusimulia hadithi na mfuatano wa matukio kiwakati pamoja na wahusika. Hivyo basi nadharia ya naratolojia ilitoa mwelekeo wa yaliyochunguzwa kuhusiana na vipengele vya sauti ya simulizi na mtazamo. Nadharia ya naratolojia ina mihimili mingi kama ilivyojadiliwa hapo juu lakini utafiti huu ulitumia mihimili mitatu ifuatayo;

I. Kutambua kuwa matukio katika ngano hupangwa kwa mfuatano wa kiusababishi. Uhimili huu ulitumiwa kuchunguza jinsi mfuatano wa matukio katika ngano teule ulitumika kufafanulia mwonoulimwengu wa Wandia.
II. Kutambua kuwa matukio katika matini huweza kusimuliwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za usimulizi. Mhimili huu ulitumiwa kuchunguza namna dhana ya mwonoulimwengu wa Wandia ilisimuliwa katika ngano teule kwa kutumia mbinu mbalimbali.
III. Kutambua kuwa Wananaratolojia wanajihusisha na suala la wakala wa usimuliaji, yaani uwezo wa wahusika wa kutagusana na kushawishi ulimwengu wa ngano kwa maamuzi na matendo yao. Mhimili huu ulitumiwa kuchunguza jinsi wahusika wanavyochangia dhana ya mwonoulimwengu wa Wandia kwa kuwezesha kutendeka kwa mambo na kuendeleza ploti.
IV. Kutambua suala la mkabala la kimtazamo ambapo msimulizi hadhamirii kuwasimulia wasikilizaji mambo tu bali ana mtazamo wake kuhusu masuala anayowashirikisha. Mhimili huu ulisaidia katika ufahamu wa mtazamo wa fanani Wanjira wa Rukenya kuhusu mwonoulimwenu wa jamii ya Wandia.

Kwa jumla, uchunguzi wa kinaratolojia unahusisha kinachosimuliwa, matukio, wakati, mpangilio, njia na mitindo ya usimulizi pamoja na ufanisi wake. Nadharia ya naratolojia ilitumika kama dira ambayo iliongoza utafutaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data katika utafiti huu. Nadharia hii ilituelekeza katika matini ya ngano za Wandia kuhusiana na fani ya usimulizi kwa lengo la kubaini mwonoulimwengu wa Wandia kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Hivyo basi, nadharia ya naratolojia ni faafu kwa utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani na ulifanywa katika kijiji cha Baricho kilichoko kaunti ya Kirinyaga nchini Kenya. Uteuzi wa Baricho ulitokana na misingi kwamba huko ndiko makazi ya fanani Wanjira wa Rukenya ambaye alichukuliwa katika utafiti huu kuwa kiwakilishi cha utamaduni wa Wandia. Aidha, Fanani Wanjira wa Rukenya ni sauti ya simulizi na kiakisi cha mtazamo wa Wandia. Isitoshe, uteuzi wa Baricho ulilenga kudumisha uasilia kwa kutoa mifano kutoka kwa mazingira asilia.

## 3.2 Mpangilio wa Utafiti

Utafiti huu ulichukua mpangilio wa kihistahilifu kwa sababu ulitumia maelezo katika ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data (Silverman, 2000). Utafiti huu ni wa kifasihi ambapo kipera cha ngano kiliteuliwa miongoni mwa vipera vinginevyo vya fasihi simulizi. Ni utafiti wa nyanjani ambao ulishurutisha mtafiti kusimuliwa jumla ya hadithi kumi na Fanani Wanjira wa Rukenya. Mpangilio huu umeegemezwa kwenye mhimili wa kiethnografia ambao umekitwa kwenye mitazamo ya kimwonoulimwengu katika utafiti wa fasihi. Utafiti huu ulichochewa hususan na mawazo ya Webster na Mertova (2007) walipodokeza kuwa ngano zinaibuka kutokana na tajriba ya jamii na sio ombwe tupu. Aidha, maoni ya Kabira (1983) kuwa msanii anapaswa kuchunguzwa katika muktadha wa jamii yake ili kuelewa mwonoulimwengu wa jamii yalichochea matumizi ya mpangilio huu wa utafiti. Utafiti huu ulihusu utafutaji wa data msingi kutoka kwa ngano sita teule zilizotumiwa katika utafiti huu. Data hii iliwezesha uchanganuzi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule.

## 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la wasailiwa (Kothari, 2009; Mugenda na Mugenda, 2003). Sampuli maksudi ilitumiwa kuteua utanzu wa fasihi simulizi kutokana na misingi kwamba fasihi simulizi ni zao la jamii iliyoizaa. Sampuli lengwa katika utafiti huu ni usimulizi wa mwonoulimwengu katika ngano teule. Fanani Wanjira wa Rukenya aliteuliwa miongoni mwa fanani wengi wa jamii ya Wandia kwa sababu ana tajriba pana ya utambaji wa ngano. Mtafiti alishiriki uwasilishaji wa ngano kumi uliofanywa na Wanjira wa Rukenya. Kisha

udondoshaji ulifanywa ili kupata idadi ya ngano sita teule zilizosheheni maudhui ya mwonoulimwengu. Unukuzi wa ngano teule ulifanywa kwa lahaja ya Kindia na kutafsiriwa kwa Kiswahili Sanifu. Mbinu hii iliufaa utafiti katika ukusanyaji wa ngano teule kutokana na utambaji wa fanani Wanjira Wa Rukenya. Utafiti ulihakiki mwonoulimwengu kutokana na ngano teule.

### 3.4 Vifaa vya Utafiti

Utafiti huu ulitumia orodha ya ukaguzi kama kifaa cha utafiti. Orodha hii ilitumiwa kukagua ikiwa vipengele vya utafiti vilivyonuiwa kuchunguza mwonoulimwengu wa Wandia vilijitokeza katika ngano teule. Ukaguzi huu ulisaidia kuonyesha namna ambavyo maudhui ya mwonoulimwengu wa Wandia ulivyosawiriwa kinaratolojia katika ngano teule. Mtafiti alitayarisha orodha ya ukaguzi kwa kuongozwa na madhumuni ya utafiti. Orodha ya ukaguzi ya kwanza ilionyesha usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa wa Wandia kwa kuzingatia shughuli na matendo ya wahusika. Orodha ya ukaguzi ya pili ilionyesha jinsi sauti ya simulizi na mtazamo zilivyochangia usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia vyanzo vya msingi na vyanzo vya pili.

#### 3.5.1 Vyanzo vya Msingi vya Data

Data iliyotumiwa katika utafiti huu ni data msingi. Ngano zilikusanywa nyanjani na mtafiti mwenyewe. Ngano kumi zilitambwa na fanani Wanjira Wa Rukenya na kurekodiwa kwa kinasa video. Udondoshaji ulifanywa ili kupata sampuli ya ngano sita iliyotumiwa katika utafiti huu. Unukuzi ulifanywa kwa lahaja ya Kindia. Mfumo wa kialfabeti ambao umetumika katika Kamusi ya T.G Benson (1964), *Kikuyu –English Dictionary* ulitumika katika unukuzi wa ngano teule. Mfumo huu wa kialfabeti unatambua sauti /a/, /b/, /c/, /e/, /g/, /h/, /i/ /ĩ/, /k/. /mb/, /m/, /n/, /nd/, /ng/ /ng`/, /nj/, /ny/, /o/, /r/, /t/ /th/, /u/ ,/ũ/, /w/ na /y/. Matini za unukuzi wa ngano zilitafsiriwa kwa Kiswahili sanifu. Tafsiri zilizingatia mtazamo wa Kloepfer (1967) ambao husisitiza ujumi wa matini ya tafsiri kwa kuzingatia vipengele vya maudhui na muundo (Tanrikulu, 2017). Mtafiti alidumisha ujumi wa matini ya tafsiri kwa kuzingatia

maudhui katika ngano asilia na muundo wa ngano. Lengo lilikuwa kuwasilisha dhana katika lugha asilia kwa hadhira lengwa bila kupotosha maana.

Makala ya unukuzi wa ngano teule pamoja na tafsiri zake yalisomwa na mtafiti na kupata data. Mtafiti alihakiki ngano teule kwa kuzingatia mihimili teule ya nadharia ya naratolojia na malengo ya utafiti. Mchakato wa udondoshaji ulitumika katika utafiti huu. Mtafiti alisoma ngano zote na kuchanganua data kwa kuiweka katika makundi matatu kama vile, data inayohusu mwonoulimwengu wa kijamiii, kiuchumi, na kisiasa.

Uchambuzi wa kimaudhui wa ngano ulifanywa na kuwezesha kuwepo kwa sura ya nne na ya tano. Sura hizi ziliibuka kwa sababu ngano zilipangika katika kategoria za ngano ambazo zilishughulikia lengo la kwanza na la pili mtawalia. Data iliyokusanywa ni maudhui yanayoonyesha jinsi mwonoulimwengu wa Wandia unavyojitokeza katika ngano zao kwa kuzingatia vigezo vya shughuli na matendo ya wahusika. Aidha, vigezo vya sauti ya simulizi na mtazamo vilitumiwa kubainisha jinsi vinavyochangia usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia Kijamii, kiuchumi na kisiasa.

### 3.5.2 Vyanzo vya Pili vya Data

Utafiti wa maktabani ulifanywa ili kuakisi mitazamo ya kinadharia na kazi zingine zinazohusiana na utafiti huu. Utafiti wa maktabani ulifanywa katika maktaba ya Chuo Kikuu Cha Chuka, Chuo Kikuu Cha Nairobi na Maktaba ya Kitaifa. Uteuzi wa chuo kikuu cha Chuka ulitokana na sababu kuwa maktaba ya chuo hiki ina vitabu, tasnifu, majarida na machapisho tosha yaliyotumiwa kufanikisha utafiti huu. Uteuzi wa maktaba ya Chuo kukuu cha Nairobi ulitokana na misingi kwamba chuo hiki kimekuwepo kwa muda mrefu na watafiti wengi wamewahi kuwasilisha tasnifu zao katika taaluma ya fasihi simulizi. Aidha, maktaba hii ina vitabu, majarida na machapisho yaliyotumiwa kufanikisha mwauo wa maandishi katika utafiti huu. Maktaba ya Kitaifa iliufaa utafiti huu kwa kuwa ina vitabu kongwe ambavyo havipatikani katika maktaba za vyuo teule. Maktabani, tasnifu za wasomi mbalimbali waliotumia nadharia ya naratolojia zilipitiwa.

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Kila ngano ilitambulishwa kwa konsonanti N pamoja na nambari za tarakimu, mfano N1-Kabindura ili kurahisisha uchanganuzi wa data. Makala ya unukuzi wa ngano teule pamoja na tafsiri zake yalisomwa na mtafiti na kupata data. Mtafiti alihakiki ngano teule kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya naratolojia na malengo ya utafiti. Uchanganuzi wa data ulilenga kueleza namna mwonoulimwengu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa ulivyojitokeza katika ngano za Wandia. Aidha, kutathmini jinsi sauti ya simulizi ilitumiwa katika usimulizi wa mwonoulimwengu wa Wandia. Isitoshe, mitazamo ya msimulizi na wahusika ilitumiwa kuwasilisha mwonoulimwengu katika ngano zao. Uchanganuzi wa data ulitumia mbinu ya uhakiki wa mada uliokitwa kwenye mihimili ya nadharia ya naratolojia.

### 3.7 Uwasilishaji wa Data

Uwasilishaji wa kimaelezo ulizingatiwa katika kuwasilisha data iliyokusanywa kuhusu usimulizi wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano zao. Mtafiti aliwasilisha matokeo ya data aliyokusanya kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Mchakato wa udondoshaji ulitumika katika utafiti huu. Mtafiti alisoma matini za tafsiri za ngano zote na kuchanganua data kwa kuiweka katika makundi matatu kulingana na malengo ya utafiti. Mtafiti alidondoa vifungu vinavyodhihirisha shughuli za kijamii, kiuchumi na kisiasa na kuzifasiri kwa mtazamo wa mwonoulimwengu. Aidha mtafiti alidondoa mbinu za kisimulizi katika ngano teule huku akinukuu matumizi ya sauti ya simulizi na mtazamo, akatoa fasili pamoja na mchango wake katika kuelezea mwonoulimwengu wa Wandia.

Kazi hii iliwasilishwa katika sura sita. Sura ya kwanza ina utangulizi. Sura ya pili iliangazia mwauo wa maandishi pamoja na msingi wa kinadharia. Sura ya tatu ilishughulikia mbinu za utafiti. Sura ya nne na ya tano zilishughulikia matokeo ya utafiti. Sura ya sita ni muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

### 3.8 Maadili ya Utafiti

Mtafiti aliwanukuu wasomi na waandishi wengine kitaaluma na kuandika katika marejeleo ili kuepuka kosa la wizi wa maarifa. Kamati ya maadili ya chuo kikuu cha

Chuka iliidhinisha utafiti huu kwamba umekubaliwa kufanywa na kupendekeza kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi kutoa kibali. Mtafiti alipata cheti cha kufanya utafiti kutoka kwa Halmashauri hiyo kabla ya kuanza utafiti. Mtafiti alimjulisha fanani Wanjira wa Rukenya azma ya kushiriki uwasilishaji wa ngano hapo awali na akahakikisha kuwa data iliyopatikana ilitumika katika utafiti pekee ili kudumisha usiri.

# SURA YA NNE

# USAWIRI WA MWONOULIMWENGU WA KIJAMII, KIUCHUMI NA KISIASA KATIKA NGANO ZA WANDIA

## 4.1 Utangulizi

Mwonoulimwengu ni fasiri ya maana ya uhalisia wa maisha uliokitwa kwenye utamaduni wa watu fulani. Nyonje (2006), anaeleza kuwa utamaduni wa watu una dhima ya utambulisho wa upekee wa watu fulani na ndicho kibainishi cha mwonoulimwengu wao. Ngano ni chombo muhimu cha kufafanulia mwonoulimwengu wa watu kwa sababu zinaibuka kutokana na tajriba ya jamii (Webster na Mertova, 2007). Ngano za Wandia zinasheheni mionoulimwengu mingi. Baadhi ya mionoulimwengu hii ni kama:

## 4.2 Usawiri Wa Mwonoulimwengu Wa Kijamii Wa Wandia

Musungu (2016) amedokeza kuwa tanzu nyingi za fasihi simulizi huakisi maisha ya jamii zilizozizaa. Katika utafiti huu usawiri wa mwonoulimwengu ulihusisha matendo, matamshi, falsafa na shughuli za kila siku za maisha ya jamii ya Wandia. Ilibainika kuwa mada za mivutano ya kijinsia, uchumba, ndoa, malezi, kudhibiti nafsi, maadili, udugu, haki ya kijamii na tabaka ndiyo masuala ambayo yanatawala fasiri ya mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia. Sehemu inayofuata ilishughulikia kila kipengele cha fasiri ya mwonoulimwengu wa kijami wa Wandia.

### 4.2.1 Mivutano ya Kijinsia

Uhusiano wa nguvu za kijinsia ulibainika kuwa chanzo cha itikadi ya kijinsia inayodhihirisha mkinzano wa kijinsia unaosababishwa na wanaume kwa upande mmoja waking`ang`ania udhibiti wa wanawake huku wanawake wakitaka kijitanzua kutokana na minyororo ya ubabedume (Waita, 2019: 50). Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti huu katika N1, N2, N3 na N4. Migogoro ya kijinsia ilichukua taswira ya mgomo wa wasichana uliohusu kiapo cha kutoongea wala kuolewa na wanaume katika N1. Hali hii iliwawia vigumu wanaume kutongoza wasichana. Mgomo huu umeelezewa kinathari kama ifuatavyo;

> Hapo zamani za kale, kulikuwa na wasichana waliogoma na kula kiapo cha kutoongea na wanaume. Wakasema kuwa mwanamume yeyote atakayeongea naye ndiye atakayemwoa…Wasichana wamekataa kuolewa. Walipokataa kuolewa, wakasema, `` Msichana ambaye ataongea na mvulana yeyote ndiye atakayemwoa.

Dondoo hili lilibainisha kuwa wasichana walijiwekea masharti ya kutoongea na wanaume kama kigezo mwafaka cha kuwezesha kuolewa kwao. Kigezo hiki cha kutoongea na wanaume ni kinyume cha maadili ya jamii ya Wandia na ni chanzo cha mtamauko wa barobaro. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Naye Kabindura akabishana na barobaro. Alipobishana nao akawaambia, `` mimi kwa sababu mnakataa kwenda kuongea na wasichana hao ambao wamegoma na hawataki kuolewa, nitamwoa mmoja wa wasichana hao ambao wamegoma.

Dondoo hili lilithibitisha kuwa mgomo wa wasichana uliwatamausha wanaume na kuathiri uhusiano wa kawaida wa kijinsia. Dondoo hili linaafiki mawazo ya Propp (1928) yanayoshikilia kuwa matukio hupangwa kwa mfuatano maalum wa kiusababishi. Hapa kitendo cha wasichana cha kususia uchumba na ndoa ndicho kichocheo kikubwa cha Kabindura kujitolea mhanga kubadilisha hali hii. Kabindura alijitokeza kama wakala wa simulizi ambaye aliathiri ulimwengu wa ngano hii na kuendeleza msuko wake kwa kuzua mikakati ya kusitisha mgomo wa wasichana na kurejesha hali ya kawaida ya mahusiano ya kijinsia. Muktadha huu ulishurutisha Kabindura kuwarai barobaro wamwekee dau. Dondoo hili linathibitisha haya;

> …Na nikiwaoa mtanipatia nini? Kabindura akaambiwa, `` nitakupatia ndama``. Mwenzake akajitolea, `` nitakupatia mbuzi watano na kwa sababu walikuwa watatu, `` nitakupatia fahari``.

Dondoo hili lilidhihirisha wazi mtamauko wa barobaro kutokana na ahadi za ng`ombe, fahali na mbuzi iwapo Kabindura angefaulu kumwoa msichana aliyegoma. Taswira sikivu ilitumika kusawiri mtamauko wa barobaro hivi kwamba barobaro walikuwa radhi kumwahidi Kabindura mbuzi na ng`ombe. Katika muktadha huu, barobaro walipania kuona urejesho wa uhusiano wa kawaida wa kijinsia katika mazingira ya kawaida. Uwakala wa simulizi wa Kabindura unaendelea kudhihirika katika kifungu kifuatacho:

> ``Sasa mbona unang`oa mtama? Njoo uniambie. Njoo useme kile unachotaka…Sasa kwa sababu umeng`oa mtama na unaendelea kung`oa. Using`oe tena…Sasa kwa sababu tulisema, mtu tutakayeenda naye ni yule ambaye tutakuwa tumeongea naye. Sasa kwa sababu nimeongea nawe twende sasa``.

Dondoo hili lilibainisha kuwa msichana alichukua nafasi ya wakala wa simulizi na kukuza ploti na kuendeleza maudhui ya mivutano ya kijinsia. Taswira uoni inayohusu

msichana kumwona Kabindura aking`oa mtama ilichochea taswira mwendo hasa msichana alipomrai Kabindura aende alipo amwelezee alichotaka badala ya kuong`oa mtama. Kuolewa kwa msichana na Kabindura kumeibua kiwango kingine cha mivutano ya kijinsia katika jamii ya Wandia. Kiwango hiki kilikitwa kwenye misingi ya ulemavu, kutokuwa na haiba na kutovutia kwa jumla. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> Sasa Kabindura na mkewe wakatoka nje. Nao barobaro wamekuja kuona ili kuondoa shaka… Kuhusu mgomo, wasichana wakaitana tena. Njooni tusitishe mgomo kwa sababu wasichana wote wazuri ndio wanaolewa na *`mang`ong`oi`*- barobaro wasio hali wala fasili, waisovutia, wasioweza hata kujitetea.

Taswira mwendo katika dondoo hili ilihusisha Kabindura na Mkewe kutoka nje pamoja na ujio wa barobaro. Taswira hii ni ithibati kwamba mivutano ya kijinsia ni sehemu ya usawiri wa mwonoulimwengu wa Kijamii wa Wandia. Isitoshe, dondoo lenyewe liliibua taswira mwono kutokana na lengo la barobaro kwenda kuona msichana aliyeolewa na Kabindura. Aidha, taswira hisi ndicho kichocheo kikuu kilichowafanya wasichana kusitisha mgomo. Hapa mivutano ya kijinsia kama kibainishi cha mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia ilitokana na hisia kwamba msichana mrembo hapaswi kuolewa na maskini hohehahe kama Kabindura. Kusitishwa kwa mgomo kuliashiria urejesho wa nguvu kwa wanaume katika mawanda ya uchumba na Kuchumbiana. Kabindura alitumika kama wakala wa simulizi aliyewarejeshea wanaume nguvu za kutongoza, kuchumbia na kuoa wasichana. Kufikia hapa uhalalisho wa utaratibu wa mahusiano ya kijinsia ulidhihirika wazi. Mgomo wa wasichana ni jazanda inayoashiria jitihada za wasichana kujikomboa kutokana na athari za dhuluma za wanaume. Matokeo ya mgomo huu ni tanzia ambayo ilifanya wasichana warembo kuolewa na wanaume wenye kasoro kama vile Kabindura. Muktadha wa uwasilishaji ulibainisha kuwa msimulizi aliwasuta wasichana kwa kuzingatia maamuzi yasiyokitwa kwenye mantiki yoyote na kuishia kuolewa na wanaume wasiowapenda. Hapa mtazamo wa msimulizi kuhusu mahusiano ya kijinsia ulijitokeza. Alipowasuta wasichana kwa kufuata maamuzi ya kijinga alionyesha mtazamo wake kwamba ndoa ni suala nyeti na maamuzi yoyote yalipaswa kukitwa kwenye mantiki ya ufahamu na utambuzi wa vipengele vya msingi wa ndoa. Mtazamo huu ulichukuliwa katika utafiti huu kama msingi wa uhakiki wa mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia kwa kuwa msimulizi ni kiwakilishi cha tajriba ya jamii ya Wandia.

N3, Muya na dada yake Cinji ilidhihirisha mivutano ya kijinsia inayotokana na kudhibitiwa kwa msichana na utamaduni ambao ulimtengea nafasi finyu nyumbani. Majukumu haya yalielezewa kinaratolojia na Muya kupitia balagha ambapo alijuta katika dondoo lifuatalo;

> Akaakaa, akaakaa. Akaathiriwa na funza. Akaathiriwa na njaa. Akasema, `` Sasa dada yangu angekuwa hapa si ningekuwa nikishiba kama zamani? Ningekuwa nimetolewa funza hawa? Sasa nitafanya nini? Sasa nitaamka niende kumtafuta kupitia njia aliyopitia.

Dondoo hili linaafiki mawazo ya Propp (1928) yaliyosisitiza kuwa matukio hupangwa kwa mfuatano wa kiusababishi. Ilibainika kwamba kutwaliwa kwa Cinji ndiko kulisababisha kutamauka kwa Muya ambako kulimfanya ajutie mateso aliyopitia kupitia balagha. Aidha, dondoo hili lina mshabaha na maoni ya Musungu (2016) anapodokeza kuwa; asili ya mivutano ya kijinsia ni muktadha wa kitamaduni ambao hugawa majukumu ya kijamii kwa misingi ya kijinsia na kwamba mtu huzaliwa katika utamaduni fulani ambao unamwongoza mtu kuhusu jinsi ya kufikiri na kutenda hasa katika mahusiano yake na watu wengine. Uzungumzi nafsia wa Muya ulimfanya kuwa wakala wa simulizi ambaye alitumiwa kuendeleza dhana ya mivutano ya kijinsia kwa kudhihirisha majukumu yaliyotengewa wasichana. Baadhi ya majukumu haya ni k.v; kupika, kufua nguo, kutoa funza na kutunza nyumba kwa jumla.

Dondoo hili linaafiki mawazo ya Habib (2011) yanayobainisha kuwa mhusika na kitendo ni vipengele muhimu katika hadithi na kwamba tabia ya mhusika sharti ionyeshwe kupitia ploti. Hapa tabia ya Muya ilidhihirisha utegemezi wa jinsia ya Kike kupita kiasi, suala ambalo linaibua mvutano wa kijinsia kama sehemu ya usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia. Utamaduni umebainisha wazi majukumu ya wanaume na wanawake. Ubainisho wa majukumu haya ndio msingi thabiti wa mivutano ya kijinsia. Mathalan, utamaduni huu umedekeza mtoto wa kiume na kumdhibiti mtoto wa kike. Kwa mfano, Muya alimwacha dada yake Cinji nyumbani akitekeleza majukumu kama vile kupika na kufua naye alihudhuria densi za usiku.

Nafasi ya utamaduni katika usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii wa jamii ya Wandia kwa misingi ya mivutano ya kijinsia ilisimuliwa kinaratolojia kwa kuzingatia kaida ya mfuatano wa matukio kiusababishi (Propp, 1928). Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, utamaduni wa Wandia umepewa nafasi mahususi katika fasiri

ya mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Ndugu yake aliporejea kutoka densini akamwambia, `` Muya unajua kuna wanaume watatu wanaokuja hapa kunikuta unapoondoka?... utanitafuta wewe. Na njia nitakayopitia nitakuelekeza. Nitabeba vitu vyote; nibebe mtama, fiwi, njegere, maharagwe na wimbi. Nitabeba chochote kitakachopatikana ili ile njia utakayopitia ukinitafuta uione ikiwa imeota mimea hii sababu hutanikuta.

Suala la ajenti wa simulizi katika dondoo hili lilijitokeza kutokana na Cinji kukubaliana na matakwa ya kitamaduni na kuhiari kutochukua hatua yoyote dhidi ya kutwaliwa na kuozwa mume kwa lazima. Aidha, barobaro waliomtwaa Cinji kwa nguvu ni wakala wa simulizi kwa kuwa walizingatia masharti ya kitamaduni na kuathiri ulimwengu wa ngano hii na kuendeleza msuko wake. Utamaduni uliwaruhusu wanaume kumtwaa msichana Kwa nguvu na kumpelekea mwanamume. Katika muktadha huu wa kijamii, msichana hakuwa na hiari ya kujichagulia mume. Cinji alifahamu masharti ya utamaduni huu ndiposa hangejipigania bali alimtahadharisha ndugu yake Muya kuwa kulikuwa na uwezekano akakuta ametwaliwa kwa nguvu. Hapa ilibainika kuwa utamaduni ulimpokonya msichana uwezo wa kujiamulia masuala kuhusu mkondo wa maisha atakaoufuata kuhusu mustakabali wake. Nguvu hizi zilipokezwa wanaume ambao walizitumia kuwanyanyasa wasichana. Maoni haya yana mshabaha na Bauman (1986:2) anapodai kuwa ngano hutoa umakini mkubwa wa uchunguzi wa uhusiano baina ya fasihi simulizi na maisha. Hii inatokana na sababu kuwa muundo hasa wa ngano umekitwa kwenye matukio ya binadamu yanayojitokeza katika muktadha fulani wa uwasilishaji. Hapa inabainika kuwa ngano huakisi maisha ya jamii ambayo yalikitwa kwenye utamaduni fulani.

Mhimili wa kinaratolojia wa utambuzi wa suala la mkabala la kimtazamo huwezesha msimulizi kudhihirisha mtazamo wake kuhusu masuala anayoishirikisha hadhira. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, mtazamo wa fanani Wanjira wa Rukenya kuhusu nafasi ya mtoto wa kike katika jamii ulibainika. Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya:

> …akaathiriwa na funza. Akaliwa na funza. Akaathiriwa na njaa. Akasema, `` sasa dada yangu angekuwa hapa si ningekuwa nikishiba kama zamani? Ningekuwa nimetolewa funza?

Dondoo hili linaafiki mawazo ya Propp (1928) kwa kuelezea masaibu yaliyompata Muya kwa kuzingatia mfuatano wa matukio kiusababishi. Maelezo haya yanazua taswira uoni ambayo ilichora picha ya kudhoofika kwa Muya kiafya. Msimulizi amefaulu kuthibitisha kuwa msichana ana uwezo wa kufanikisha maisha ya mvulana. Aidha, mwanamume amechorwa kama kiumbe dhaifu ambaye hana budi kumtegemea mwanamke. Hapa uhusiano wa kijinsia unabadilika na kuchukua mkondo wa taswira ya kutegemeana ambapo kufaulu kwa jinsia moja kunategemea jinsia nyingine.

### 4.2.2 Uchumba

TUKI (2018: 662) wameelezea fasiri ya uchumba kwa njia mbili: Makubaliano ya pande mbili baina ya mwanamke na mwanamume wanaotaka kuoana na kipindi ambacho mwanamume na mwanamke wanakaa kabla ya kufunga ndoa baada ya kuwa na makubaliano ya kuoana. Utafiti huu ulizingatia vigezo hivi viwili katika uchanganuzi wa maudhui ya uchumba katika ngano teule. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti huu katika N1 na N3. Mfano, katika N1, Kabindura, mgomo wa wasichana wa kutoongea na barobaro ulisababishia jamii masaibu mengi. Aidha mgomo huu uliinyima jamii msisimko wa mabaleghe ulioambatanishwa na kipindi cha uchumba (Waita, 2003; Kenyatta, 1938). Msimulizi anaeleza;

> Hapo zamani za kale paliishi wasichana waliogoma na kusema kuwa yeyote watakayeongea naye ndiye atakayewaoa.

Taswira sikivu ilifanikisha usawiri wa mgomo wa wasichana. Hii ina maana kuwa kugoma kwa wasichana dhidi ya kuongea na barobaro ni sawa na kugomea kutongozwa na kuchumbiwa na barobaro. Mgomo huu ulisononesha barobaro na jamii ilijawa na ukiwa hadi Kabindura alipojitokeza kuwa wakala wa simulizi aliyejitolea kubadilisha hali hii. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> Sasa msichana akamwona Kabindura aking`oa mtama. "Ni nani huyo anayejiita Kabindura huku aking`oa mtama wetu?"... Msichana akamwambia Kabindura. "Wacha kung`oa mtama wetu. Njoo uniambie unachotaka kwa kuwa sasa unakosea."

Mpangilio wa matukio katika kifungu hiki ulizingatia mfuatano wa kiusababishi na hivyo basi kuafiki mawazo ya Propp (1928). Msichana alipomwona Kabindura aking`oa mtama, kitendo hicho kilijenga taswira uoni ambayo iliathiri msichana kihisia, suala ambalo lilijenga taswira hisi iliyowezesha kuongea kwa msichana. Kuongea huku

kuliibua taswira sikivu. Kabindura alifaulu kumshurutisha msichana aongee na kustahiki kumwoa kwa mujibu wa kiapo cha mgomo wa wasichana. Hapa Kabindura alijitokeza kama wakala wa simulizi ambaye alibadilisha ulimwengu wa ngano hii kwa kumfanya msichana aongee na kumpa nafasi ya kumwoa. Muktadha huu ulidhihirisha kuwa msichana hakupewa nafasi ya kuchumbiwa na Kabindura lakini aliolewa papo hapo kulingana na masharti ya kiapo cha mgomo.

N3, Muya na dada yake Cinji ilidhihirisha kuwa mazingira ya densini yalikuwa mazingira mwafaka ya kuchumbiana. Mazingira haya yalijitokeza katika data ya utafiti huu. Mfano, msimulizi anasema,

> …Mvulana alikuwa ameenda densini, msichana akabaki nyumbani. Mvulana alikuwa akienda kuimba nyimbo zilizokuwa zikiimbwa zamani na barobaro na wasichana.

Dondoo hili lina mshabaha na kazi ya Kenyatta (1938:56) inayosisitiza kuwa muktadha wa densini, ulikuwa muktadha mwafaka wa kuchumbiana. Muktadha wa kutwaliwa kwa nguvu ulimdhalilisha msichana na kumnyima nafasi ya kufurahia raha ya kuchumbiwa na kuchumbiana kwa hiari. Msimulizi anasema;

> Msichana akiachwa nyumbani, alikuwa akiviziwa na wanaume waliopenda kumtongoza. Ndugu yake akirejea kutoka densini, akamwambia, “Muya unajua kuna wanaume watatu wanaokuja hapa kunikuta unapoondoka?... Nami sitakubali kuuawa kwa kukataa kuwafuata. Lazima niandamane nao.”

Dondoo hili liliibua taswira uoni iliyochora picha ya msichana mpweke aliyeachwa nyumbani peke yake. Aidha, taswira mwendo ilihusishwa na jinsi wanaume walivyomvizia Cinji na azma yao ya kumtwaa kwa nguvu pasipo hiari yake. Usawiri huu ulizingatia mpangilio wa matukio kwa mfuatano wa kiusababishi (Propp, 1928). Matukio haya yalielezewa kwa njia ya nathari na hivyo basi kuafiki mhimili wa kinaratolojia unaohusu namna mbalimbali za usimuliaji wa hadithi. Usawiri wa muktadha wa kutwaliwa kwa msichana kwa nguvu ulidhihirisha nguvu za mila na utamaduni. Cinji alitambua uwezo wa nguvu hizi hadi akahiari kukubali kutwaliwa na wanaume watatu. Alichelea kuwa akiendelea kukataa kutwaliwa kwa nguvu angeuawa. Taasubi ya kiume ilitumika kudhalilisha wasichana, mfano; Cinji hakuchukua hatua yoyote na kutochukua hatua, kulimfanya wakala wa simulizi, suala ambalo lilidhihirisha nafasi ya utamaduni katika kuzua na kudumisha mivutano ya kijinsia.

Uhakiki wa N1 na N3 ulithibitisha kuwa uchumba ni kipengele muhimu ambacho kinatumiwa na jamii ya Wandia kusawiri mwonoulimwengu wao wa Kijamii. Suala la uchumba lilijitokeza bayana katika ngano mbili teule na ni ithibati tosha kuwa uchumba ni miongoni mwa tajriba muhimu ya kijamii inayotumika kufafanulia mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia.

### 4.2.3 Ndoa

Ndoa ni taasisi ya kijamii inayotumika kama chombo cha kufafanulia mwonoulimwengu wa jamii (Waita, 2003). Suala la ndoa liliangaziwa katika N1, N3 na N4. Data ya utafiti katika N1 ilithibitisha kuwa wasichana walisusia ndoa na kushiriki mgomo ambao uliwashurutisha kula kiapo cha kutoongea na wanaume na kusisitiza kuwa msichana yeyote akiongea na barobaro hangekuwa na budi kuolewa naye pasipo kujali iwapo ana kasoro zozote za kimaumbile. Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> Wasichana wamekataa kuolewa. Walipokataa kuolewa wakasema, "Msichana ambaye ataongea na mvulana yeyote ndiye atakayemwoa."

Taswira sikivu iliyotokana na kitendo cha wasichana kuafikiana wasiongee na barobaro ilitumika kuelezea kiapo cha mgomo wa wasichana. Hii ina maana kuwa wasichana walizua msingi wa kiajabuajabu wa uteuzi wa mume wa ndoa. Msingi huu uliegemezwa kwenye kipengele cha kutoongea na wanaume na haukuwa na mantiki yoyote. Mtazamo huu ulihitaji kubadilishwa ili kuwarejeshea wanaume hadhi yao. Ujio wa Kabindura ulibadilisha hali hii. Kabindura ambaye alijitokeza kama wakala wa simulizi alichukua hatua ya kuongea na msichana mrembo na kuathiri mazingira ya simulizi. Kabindura aling`oa mtama hadi msichana alipoongea. Msimulizi anaeleza:

> "Ni nani huyo anayejiita Kabindura huku akingo`oa mtama wetu? Nitakuja kuambiwa vipi na mama na walienda mkutano? Wacha kung`oa mtama. Mbona unang`oa mtama? Njoo useme kile unachotaka."

Taswira uoni iliyohusisha msichana kumwona Kabindura aking`oa mtama iliibua taswira hisi ambayo ilimfanya msichana achelee kuchapwa na mama yake. Taswira uoni na taswira hisi zilimchochea msichana kuuliza maswali ya balagha. Japo alishiriki mgomo wa kudumisha ukimya aliuliza maswali yaliyolenga kujua aliyekuwa aking`oa mtama ni nani na iwapo angeendelea kung`oa mtama, matokeo yake yangekuwa yepi.

Maswali haya yaliibua taswira hisi ambayo ilimshinikiza kuongea na Kabindura na mwishowe kumrai aende asemezane naye. Papo hapo msichana alimrai Kabindura amwoe na akaandamana naye hadi kwake na kuwa mkewe. Kadhia ya msichana kuolewa na Kabindura ilipenyeza mhimili wa wakala wa simulizi. Kadhia hii iliwafanya wasichana kuchukua hatua nyingine na kusitisha mgomo. Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya:

> Kuhusu mgomo wa wasichana, wakaitana tena, "Njooni tusitishe mgomo kwa sababu …. wasichana wale wazuri ndio wanaolewa na *mang`ongo`i*. Barobaro wasio hali wala fasiri, wasioweza hata kujitetea kwa wasichana."

Dondoo hili lilipenyeza mhimili unaosisitiza mpangilio wa matukio kwa mfuatano wa kiusababishi (Propp, 1928). Hapa kusitishwa kwa mgomo kulifuatia tanzia ya kuolewa kwa wasichana wazuri na barobaro wasiovutia. Uwakala wa simulizi uliwezesha wasichana kuchukua hatua ya kusitisha mgomo na kuwarejeshea barobaro uwezo wa kutongoza, kuchumbia na kuoa wasichana. Kwa kuongozwa na mhimili wa suala la mkabala la mtazamo, ilibainika kuwa mtazamo wa jamii kuhusu ndoa ni kwamba kila mwanamume alipaswa kuoa pasipo kujali misingi ya iwapo ni maskini au mwenye kasoro za kimaumbile. Hii ndiyo fasiri ya mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia.

N3, Muya na dada yake Cinji ilielezea utaratibu wa ndoa kati ya barobaro na msichana. Simulizi hii ina mshabaha na kazi ya Kenyatta (1938:171) anaposisitiza kuwa siku ya arusi ilipangwa na msichana hangejulishwa lakini angeviziwa na barobaro na kubebwa kwa mabega na kupelekwa hadi kwa mumewe. Maelezo haya ya Kenyatta (mtaje) yana mshabaha na utaratibu wa ndoa katika ngano ya Muya na dadake Cinji. Katika ngano hii utamaduni una nguvu nyingi kiasi kwamba msichana anatwaliwa kwa nguvu na kuridhia hali hii pasipo malalamishi yoyote. Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> Haya! Wakakaa huku Muya akiambiwa ``utanitafuta wewe, na njia nitakayopitia nitakuelekeza. Nitabeba vitu vyote; nibebe mtama, fiwi, njegere, maharagwe na wimbi. Nitabeba chochote kitakachopatikana ili ile njia utakayopitia ukinitafuta uione ikiwa iliota mimea hii. Sababu hutanikuta. Mimi sitakubali kuuawa kwa kukataa kuwafuata lazima niandamane nao.

Dondoo hili lilizingatia mfuatano wa matukio kiusababishi (Propp, 1928) na kuibua taswira sikivu iliyobainisha nguvu za utamaduni wa Wandia. Aidha, taswira uoni kuhusu kuota kwa mimea tofauti ilipaswa kutumiwa kama kielekezi cha njia

aliyopitishiwa Cinji. Njia yenye mimea ni kielelezo cha taswira mwendo iliyoashiria safari ya Cinji. Safari hii ni sitiari ya safari ya ndoa ya Cinji na kibainishi cha nguvu za utamaduni wa Wandia. Cinji aliridhika kwamba hakuwa na budi kutwaliwa kwa nguvu na kuifanya kadhia ya msichana kutwaliwa kwa nguvu kuonekana kuwa kadhia ya kawaida. Kitendo cha wasichana kuridhia hali hii kinaonyesha utendakazi wa mhimili wa wakala wa simulizi ambapo msichana hachukui hatua yoyote ya kupinga dhuluma hii ya kijinsia. Vivyo hivyo mtazamo wa jamii ya Wandia kuhusu nafasi na umuhimu wa ndoa ulithibitika. Mtazamo wa jamii unaoshikilia kwamba kila mtu sharti aoe ama aolewe ndio msingi wa fasiri ya mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia kwa kuongozwa na kigezo cha ndoa.

### 4.2.4 Malezi

Suala la malezi lilijitokeza katika N1, N2 na N3, mfano; katika N1 Kabindura, malezi ya mtoto yalifungamanishwa na majukumu ya kijamii katika utu uzima. Mathalan, malezi ya mtoto wa kike yalipendekeza mojawapo wa majukumu yake kuwa kuwinga ndege. Hii ndiyo sababu Kabindura alimpata msichana kwenye ulingo akiwinga ndege wasile mtama. Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> Ndipo Kabindura akakuta msichana akiwinga mtama usiliwe na ndege. Akaenda. Hata hakuongea na msichana huyo. Alienda akaanza kung`oa mtama upande ambapo msichana hakuwa huku akiimba.

Dondoo hili lilithibitisha kuwa Kabindura alifahamu fika masharti ya malezi ya mtoto wa kike kwamba hangekubali mtama ung`olewe pasipo kuongea. Msichana alipoongea, alijitokeza kuwa wakala wa simulizi katika ufafanuzi wa suala la malezi bora. Msukumo wa malezi bora ulimfanya msichana kukiuka masharti ya mgomo wa wasichana mradi asitishe kung’olewa kwa mtama.

Malezi ya watoto yaliyojumuisha heshima kwa wazazi yalisisitizwa katika jamii ya Wandia. Ilithibitika kwamba kibainishi kimoja kilichoashiria heshima ya mtoto kwa mama ni kutomtaja kwa jina lake lakini kumrejelea kwa istilahi iliyoonyesha heshima kwake. Usimulizi wa kinathari unaendeleza dhana hii kama ifuatavyo;

> Msichana akamwambia Kabindura, ``wacha kung`oa mtama. Njoo uniambie unachotaka kwa kuwa sasa unakosea. Kwa sababu umeng`oa mtama, nitakuja kupigwa na `*nyanya*```. Wakati huo ndiyo tuliitana `*nyanya*`.

Dondoo hili, lilibainisha kuwa msichana aliyelelewa na kufunzwa kuwa msichana wa Kindia hakupaswa kumwita mama mzazi mama bali `*nyanya*`. Muktadha wa uwasilishaji ulizua taharuki hadi hadhira ikataka kufumbuliwa fumbo la istilahi `*nyanya*`. Kwa kutumia mtindo wa ufaraguzi, msimulizi alielezea maana ya `*nyanya*` kama ifuatayo.

> … tulikuwa tukiitana `*nyanya*` kwa kuwa kulikuwa na tofauti. Wasichana waliitana `*nyanya*`. Heshima ya mama ya mtu. Tuliitana `*nyanya*`.

Matumizi ya istilahi `*nyanya*` ni kibainishi cha heshima aliyo nayo msichana kwa mama yake mzazi. Hangeweza kumrejelea kwa istilahi mama ili kuzingatia masharti ya heshima kwa mujibu wa malezi. Heshima ya mama mzazi ni kipengele cha kimsingi katika usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia.

N2 ilidhihirisha kuwa lengo la malezi lilikuwa kulea watoto wanaowajibikia vitendo vyao. Aghalabu mtoto akiwa na tabia nzuri alipendwa na wazazi. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, msimulizi anaelezea;

> Wacuka ndiye alianza kuchota maji na alipendwa na baba kwa kuwa alikuwa na maadili mema kuliko Kamwagirwa. Wacuka akaenda mtoni na kibuyu cha baba na ndicho alikuwa akitumia kuchota maji.

Dondoo hili lilithibitisha kuwa Wacuka ametimiza masharti ya malezi bora na kukumbatia maadili mema. Kupendwa kwake na baba yake ni njia moja ya kumpa motisha aendelee kuzingatia maadili mema na aidha changamoto kwa Kamwagirwa amwige dada yake Wacuka.

N2, iliambatanisha malezi na suala la wajibu. Jamii ilitarajia mtoto ambaye amelelewa vizuri atambue wajibu wake katika jamii. Suala la wajibu lilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, msimulizi anaelezea;

> Wacuka akaenda mtoni. Akaenda na Kibuyu cha baba na ndicho alikuwa akitumia kuchota maji. Akichota maji kibuyu kikaanguka mtoni. Mawimbi ya maji yakagonga kibuyu kabla kujaa… Kibuyu kiliposombwa akasema, ``kwa sababu kibuyu hiki cha baba kilisombwa na ndicho huwa anawekewa uji, sitarudi nyumbani bila kibuyu hicho. ``

Kadhia ya kusombwa kwa kibuyu cha baba ilisimuliwa kwa njia ya nathari. Usimulizi huu uliibua taswira mwendo iliyotokana na mawimbi kukigonga kibuyu na kukisomba.

Taswira mwendo ilipisha taswira sikivu ambapo Wacuka aliamua kutorudi nyumbani bila kibuyu. Huu ni uwajibikaji ambao ni ishara ya malezi bora. Wacuka alitambua umuhimu wa kibuyu cha baba katika familia. Aidha alitambua kuwa uwajibikaji unamlazimu kuzua mikakati ya kukitafuta kibuyu cha baba hadi kipatikane. Kitendo cha kuamua kukitafuta kibuyu cha baba kilimfanya Wacuka kuwa wakala wa simulizi ambaye aliathiri ulimwengu wa ngano hii na kutoa taswira kamili ya dhana ya uwajibikaji katika malezi.

Kwa upande mwingine, taswira ya kutowajibika ilinasibishwa na kutofuata matakwa ya malezi bora. Aidha, kutowajibika kuliadhibiwa vikali. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano; kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> …Kamwagirwa naye alipomwona dadake akiwa hivyo akajua, "hata mimi nitachukua kibuyu na kukisombesha mtoni."

Dondoo hili lilithibitisha kwamba Kamwagirwa alisombesha kibuyu cha baba kimakusudi ili aweze kutunukiwa zawadi za pete na mikufu kama Wacuka. Muktadha huu ulibainisha kuwa Kamwagirwa alijitokeza kama wakala wa simulizi ambaye aliendeleza dhana ya kutozingatia malezi bora.

N3 ilishughulikia wajibu wa utekelezaji wa majukumu katika muktadha wa familia. Japo malezi ya Muya na Cinji hayakuelezewa kwa kina kwa kuwa walikuwa mayatima, Cinji alizingatia mfumo wa malezi aliyopokea na kuwajibikia maisha ya ndugu yake. Kulingana na ngano hii, dada alitwikwa wajibu wa kumtunza ndugu yake na kukosekana kwake kulisababisha madhara makubwa. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, msimulizi anaelezea;

> Mvulana alikuwa ameenda densini. Msichana akabaki nyumbani. Ndiye alikuwa akimsaidia ndugu yake kupika. Ndiye alimsaidia ndugu yake kupata mlo… Msichana hakuwa akishiriki nyimbo ili asiache nyumba hivyo.

Matukio yaliyobainisha uwajibikaji wa Cinji yalisimuliwa kinathari. Dondoo hili liliibua taswira ya msichana mpweke ambaye alihiari kukaa nyumbani pasipo kwenda densini. Tabia hii ni zao la malezi bora. Kutokana na dondoo hili ni bayana kuwa Cinji alitekeleza wajibu wake kwa ndugu yake Muya kadiri na malezi aliyopokea. Suala hili lilikaririwa na Muya baada ya Cinji kutwaliwa na kuolewa na mumewe. Muya alijutia

kuwa Cinji angekuwepo, hangepata matatizo. Mbinu ya balagha ilitumika kufanikisha majuto haya. Muya anasema;

> …dada yangu angekuwa hapa, si ningekuwa nikishiba kama zamani? Ningekuwa nimetolewa funza hawa. Sasa nitatolewa na nani? Sasa nitafanya nini?

Dondoo hili, lilitaja baadhi ya wajibu wa wasichana kwa ndugu zao wa kiume. Majuto haya yalimsawiri Muya kama mwanamume ambaye alidekezwa na utamaduni hivi kwamba pasipo dada yake maisha yake yangesambaratika. Hivyo basi taswira ya mwanamume wa Kindia ilithibitisha ya kwamba, mwanamume ni kiumbe dhaifu ambaye kufanikiwa kwake hakuna budi kuhusishwa na msaada wa mwanamke. Data ya utafiti kuhusu malezi katika ngano hii, iliafiki fasiri ya mwonoulimwengu wa Kijamii wa Wandia.

### 4.2.5 Kudhibiti Nafsi

Suala la kudhibiti nafsi ilijitokeza katika N1, N2, N3, N4 na N6. Taswira ya wasichana walioshiriki mgomo wa kutoongea wala kuolewa na wanaume ilijitokeza katika N1. Mgomo huu haukuwa na sababu yoyote yenye mantiki. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya';

> Hapo zamani za kale paliishi wasichana waliogoma na kuapa kutoongea na barobaro. Wakasema mwanamume yeyote atakayeongea nao ndiye atakayewaoa.

Dondoo hili lilithibitisha kuwa wasichana walioshiriki mgomo walikuwa na upungufu wa udhibiti nafsi na ndiposa wakashindwa kujitanzua kutokana na ushawishi wa shinikizo la marika. Wasichana katika dondoo hili walijitokeza kama wakala wa simulizi kwa kushiriki mgomo ambao ulikitwa kwenye shinikizo la kihisia na kuathiri ulimwengu wa simulizi hii. Uwakala huu wa simulizi unaendeleza ploti na kubainisha athari za kuthibiti nafsi katika mahusiano ya kijamii.

Maamuzi yaliyokitwa kwenye kituo cha kihisia aghalabu huwacha pengo la uwezekano wa matokeo mabaya katika muktadha wa kijamii. Mfano, wasichana waliposhiriki mgomo, hawakukadiria matokeo iwapo hali ingewalazimu kuongea na mwanamume yeyote. Hali hii ilijitokeza katika N1. Mfano, msimulizi anaeleza;

> Sasa, msichana akamwona Kabindura aking`oa mtama. Akamuuliza, ``ni nani huyo anayejiita Kabindura`` huku aking`oa mtama wetu?

> Msichana akamwambia, `` wacha kung`oa mtama wetu, njoo uniambie unachotaka kwa kuwa sasa unakosea, ``…akapakuliwa chakula kisha akaambiwa, `` sasa kwa sababu tulisema mtu tutakayeenda naye ni yule ambaye tutakuwa tumeongea naye, twende sasa ukanioe.

Dondoo hili linaafiki mhimili wa kinaratolojia unaoelezea kuwa kuna njia mbalimbali za usimuliaji wa matukio. Usimulizi wa tukio hili ulitumia usimulizi wa kinathari na kuibua taswira mwono inayoonyesha jinsi Kabindura alivyong`oa mtama. Taswira hii iliibua taswira sikivu ambapo msichana alimrai Kabindura aache kung`oa mtama bali aende amwambie alichotaka. Dondoo hili lilibainisha wazi kuwa kushawishika na ushawishi wa shinikizo la rika ni tanzia ambayo madhara yake yanadumu. Mfano, msichana alihiari kuolewa na Kabindura, mwanamume ambaye aliambaliwa na wasichana wengi kwa sababu ya maamuzi ya kijinga. Kabindura alitumiwa kama wakala wa simulizi aliyebainisha wazi ujinga wa wasichana wa kuongozwa na hisia pasipo kudhibiti nafsi. Huu ndio mtazamo wa jamii ya Wandia kuhusu mwonoulimwengu wa kijamii kwa kuongozwa na kipengele cha kudhibiti nafsi. Ngano hii inaonya wanajamii kuepuka kuongozwa na hisia katika maamuzi kuhusu masuala nyeti kama vile ndoa.

N2, ilitumia motifu ya safari iliyopitia kwenye mazingira ya ajabu yenye chakula kilichojipika na kujila, uji uliojipika na kujinywa, njegere zilizojiponda na kujila miongoni mwa hali zingine za kiajabu. Ngano hii ilitumia hali zingine za tabia ya wahusika katika kubainisha taswira ya kudhibiti nafsi na faida zake kwa upande mmoja na kutodhibiti nafsi na hasara zake kwa upande mwingine. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti huu. Mfano, msimulizi anaeleza

> …akipita hapo ndipo anaitwa, `` msichana huyu njoo unile ukinipondaponda na unaona kuwa tunajila. Akasema, `` sili vijilavyo`` ``Njoo uniponde na unile na tunapenda kujiponda na kujila. Ndio hizo ni fiwi kwa sababu ametoka kwa njegere. Sasa amekuja kwa uji. Ametoka kwa `*uura*`. Huo uliitwa `*uura*` wa nguchiro.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya utafiti unaotambua kwamba kuna jinsi mbalimbali za usimuliaji wa hadithi. Dondoo hili lilisimulia mandhari ya ajabu kwa njia ya nathari. Usimulizi huu ulizua taharuki inayotokana na hadhira kutaka kujua iwapo Wacuka angekula vyakula vile au la. Hapa taswira mwonjo ilitumika kama mizani ya kupima udhibiti nafsi wa Wacuka. Katika dondoo hili, uwezo wa kudhibiti

nafsi ulimwezesha Wacuka kushinda majaribu yote kwa kukataa kula chakula, kunywa uji, kula njegere na kulamba asali. Wacuka alisawiriwa kama wakala wa simulizi ambaye vitendo vyake vilitumiwa kumtuza na aidha msingi wa kumwadhibu dada yake Kamwagirwa. Kudhibiti nafsi kwa Wacuka kulimpa lakabu ya `mgeni mwenye nyumba` na aliyestahiki kutuzwa. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> …kumekuja mtu yule ambaye alikuwa mchunguzi. Amekuja na kumuuliza, `` wewe ni nani? `` ni mimi. Kuja nikupeleke nyumbani ukajikinge mvua. Anachukuliwa na kupelekwa. Nao wazazi wakamuuliza``msichana aliyemleta mwenzake…ni mgeni wa aina gani, ``huyu ni `mgeni `*kigeni*` au mgeni mwenye nyumba? naye aliyemwendea akajibu, `` ni mgeni mwenye nyumba. ``

Dondoo hili lilibainisha kuwa Wacuka alirejelewa kwa istilahi` mgeni mwenye nyumba`. Msimulizi alifafanua kuwa mgeni mwenye nyumba ni mtu ambaye hakula mali ya wenyewe safarini, yaani mtu ambaye alithibiti nafsi yake. Katika muktadha huu, Wacuka ni wakala wa simulizi ambaye alitumiwa kudhihirisha umuhimu wa kudhibiti nafsi na kuibua mtazamo wa Wandia kuhusu suala hili. Kilele cha safari hii kilidhihirika Wacuka alipopelekwa kwenye nyumba ya mwenyeji wake ili kutathmini kiwango cha ulafi na Wacuka akashinda jaribio hili. Msimulizi anaelezea

> Kondoo wangekatwa mkia na kisha kukatwa vipande vidogo vidogo na kukaangwa jikoni. Vipande hivyo vidogo vidogo kisha vililetwa kwa sahani. Sasa ukiwa na kipande kimoja naye mwenyeji ana vitatu. Yule akiwa na vinne, nawe una vitatu. Wakaendelea hivyo. Vipande vilipoisha wakalala. Sasa amemaliza mtihani na ameenda kulala.

Dondoo hili lilipenyeza mhimili wa nadharia ya utafiti ambao ulitambua jinsi mbalimbali za usimuliaji wa matukio. Matukio katika dondoo hili yalisimuliwa kwa maelezo ya nathari. Taswira mwono ilionyesha vipande vya nyama ya mkia wa kondoo na utaratibu wa ulaji wa vipande vya nyama. Taswira iliyojitokeza ni ya msichana ambaye amethibiti hisia zake. Katika dondoo hili kudhibiti nafsi kulimwezesha Wacuka kupita mtihani wa maisha wa kiwango cha juu. Hivyo basi Wacuka hakuwa na budi kutuzwa. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> ``…asubuhi aende afunguliwe ghala kama hili. Lina mapambo. Lina mikufu. Akaambiwa, jaribu ujipambe kwa chochote unachotaka. Vitu vyote akajaribu. Akajaribu pete zilizokuwa zikivaliwa kwenye mikono hii.

Dondoo hili lilielezea mandhari ya ghala lenye mapambo kinathari kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya naratolojia. Maelezo haya yalizua taswira uoni ambayo

ilionyesha jinsi Wacuka alirembeshwa kwa mapambo. Kutuzwa kwa Wacuka kuliashiria faida ya kudhibiti nafsi. Kufikia hapo, mhimili wa kinaratolojia wa suala la mkabala la kimtazamo ulijipenyeza. Tunaweza kuona mtazamo wa Fanani ambao ndio mtazamo wa jamii ya Wandia kuwa kudhibiti nafsi ni kigezo muhimu cha usawiri wa mwonoulimwengu wao wa kijamii.

Kwa upande mwingine N2, ilichora taswira ya kutodhibiti nafsi na hasara zake. Hali hii ilimfanya mtu kupeperushwa na mawimbi ya maisha kama jani kavu na matokeo yake huwa mabaya. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Dada yake alipomwona dadake akiwa hivyo akajua...hata mimi nitachukua kibuyu na kukisombesha mtoni…Msichana akaambiwa hii ndiyo sababu ulitunukiwa maganda iwapo `*uura*` wenyewe ulipokuangukia ulikula… Ungepewa pete kama hizi zangu. Sasa iwapo uliramba na ukaenda ukila chakula… "Ndio nilikuwa nikila chakula na kunywa uji." Ndio kwa sababu ulifanya hivyo ndipo hukupata vitu vizuri. Ndiyo sababu ulipewa maganda.

Dondoo hili lilielezea kinathari matukio yaliyobainisha kutodhibiti nafsi kwa Kamwagirwa. Usimuliaji huu uliegemezwa kwenye mhimili wa nadharia ya utafiti unaozingatia mpangilio wa matukio kwa mfuatano wa kiusababishi. (Propp, 1928) Hapa usombeshaji wa kibuyu kimaksudi ulifuatwa na kula chakula, kunywa uji, kuramba `*uura*` na mwishowe kuvishwa vazi la maganda. Taswira uoni katika dondoo hili ilituchorea picha ya msichana ambaye alipewa adhabu kali kutokana na kushindwa kudhibiti hisia zake. Muktadha wa uwasilishaji ulithibitisha mtazamo wa msimulizi kwamba Kamwagirwa alistahiki adhabu hiyo. Dondoo hili lilisawiri madhara ya kutodhibiti nafsi. Mathalan, Kamwagirwa kukisombesha kibuyu cha baba kimakusudi, akala chakula kilichojipika na kujinywa, akaramba `*uura*` wa Nguchiro na kula vipande vingi kuliko mwenyeji wake. Kamwagirwa alifanya makosa hayo yote kwa kuongozwa na hisia pasipo kudhibiti nafsi. Hatimaye alivikwa vazi la maganda.

Uhakiki wa N3, ulibainisha kuwa suala la kudhibiti nafsi lilinasibishwa na utambuzi wa mambo yaliyostahiki kupewa kipaumbele. Katika muktadha huu, wahusika walijikuta katika hali ya mtanziko ambapo ingewabidi kuchagua hili na kuacha lile. Data ya utafiti inathibitisha madai haya;

> Mvulana alikuwa ameenda densini. Msichana akabaki nyumbani. Ndiye alikuwa akimsaidia ndugu yake kupika. Mvulana alikuwa akienda kuimba nyimbo zilizokuwa zikiimbwa zamani na wavulana na wasichana. Msichana hakuwa akishiriki ili asiache nyumba hivyo.

Dondoo hili liliafiki mhimili unaosisitiza mpangilio wa matukio kwa mfuatano wa kiusababishi (Propp, 1928). Mfano, Muya aliendа densini, naye msichana akaamua kutoshiriki densi. Maelezo haya yaliibua taswira uoni ambayo ilipambanua picha ya msichana ambaye aliathiriwa na upweke. Dondoo hili lilithibitisha kuwa kudhibiti nafsi kulimwezesha Cinji kuamua kukaa nyumbani ili amtunze ndugu yake pamoja na nyumba. Muya, kwa kuongozwa na hisia, alizamia kwenye densi na matokeo yake yakawa Cinji kutwaliwa kwa nguvu na mwishowe Muya binafsi kutaabika. Masaibu yaliyompata Muya baadaye yalipenyeza mhimili wa suala la mkabala la mtazamo uliodhihirisha mtazamo wa Fanani na jamii ya Wandia kuwa kutodhibiti hisia kuna madhara yake.

N4 ilithibitisha kuwa kudhibiti nafsi ni kigezo muhimu cha ujenzi wa mshikamano wa mfumo wa maisha wa kijamii. Aidha, kutodhibiti nafsi kunabomoa mshikamano huu wa kijamii na watu kuishia katika migogoro ya kijamii. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti huu. Mfano, Thigiti alipoona kuwa ng`ombe wa Kanyonyo wanazaa ndama wazuri alibadilisha ndama wa Kanyonyo. Msukumo wa hisia za wivu ndizo zilizomsukuma Kanyonyo kutekeleza uovu huo kwa kuwa alishindwa kudhibiti nafsi. Msimulizi anaeleza;

> Mtu aliyekuwa na shida sana ni Thigiti kwa sababu alitamani mali ya Kanyonyo kwa sababu aliona Kanyonyo alikuwa ametunza ng`ombe wake ilhali wake hawakuwa wamenona. Alipoona kuwa ndama wa Kanyonyo amezaa ndama mzuri na wake akazaa ndama asiyevutia akabadilishana ndama hao.

Usimulizi wa dondoo hili ulizingatia mhimili wa nadharia ya utafiti unaoshikilia kuwa matukio hupangwa kwa mfuatano wa kiusababishi. Mfano, Thigiti alitamani ndama wa Kanyonyo na kisha kubadilisha ndama. Taswira uoni iliyotokana na mwonekano wa ndama wa Kanyonyo ilimfanya Thigiti kutamani ndama huyo. Kitendo cha kutamani ndama wa Kanyonyo kilijenga taswira dhahania. Taswira hii ilimpa Thigiti msukumo wa kubadilisha ndama wa Kanyonyo. Dondoo hili lilionyesha kuwa kutamani mali ya wenyewe ni matokeo ya kutodhibiti nafsi. Kitendo cha Thigiti kilivunja mshikamano

wake na Kanyonyo na hatima yake ikawa ni kupeleka kesi mbele ya baraza la wazee iamuliwe. Katika ngano hii Thigiti alisawiriwa kama wakala wa simulizi kwa kuwa matendo yake yalibadilisha ulimwengu wa ngano hii kwa kuathiri hali ya mahusiano. Thigiti angedhibiti hisia, asingebadilisha ndama wa Kanyonyo na urafiki wao ungeendelea kuwepo;

N6, Ndovu na Fisi, ilibainisha kuwa kutodhibiti nafsi, tamaa na ulafi ni mambo ambayo huvunja mahusiano ya kidugu. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Fisi akikaakaa, mtoto akasema, Ihi! Ihi! Ihi! Ihi!
> Akaulizwa na mama yake, `` unataka nini?
> Akajibu, ``nataka kuuma uwayo wa Ndovu mafuta yachirizike ta!
> Akaambiwa nenda ukaume, akaenda akauma uwayo wa Ndovu.
> Mtoto mwingine akasema, Ehe! Ehe! Ehe!
> Akaulizwa, `` unataka nini?
> Ninataka kuuma uwayo wa Ndovu mafuta yachirizike ta!
> Naye mke akaiga
> Ehe! Ehe! Ehe! Ehe!
> Akaulizwa unataka nini?
> Ninataka kuuma uwayo wa Ndovu
> Mafuta yachirizike ta!
> Mumewe naye akasema
> Ehe! Ehe! Ehe! Ehe!
> Akaulizwa, `` unataka nini?
> Ninataka kuuma uwayo wa ndovu
> Mafuta yachirizike ta!

Katika dondoo hili udhalimu wa fisi umeelezewa kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza mpangilio wa matukio kwa mfuatano wa kiusababishi. Mfano, kilio cha mtoto, swali, idhini na kuuma uwayo wa ndovu. Taswira uoni imechora picha ya ndovu mwenye uwayo uliojaa mafuta hivi kwamba uking'atwa, mafuta yangechirizika. Taswira uoni ilichochea taswira mwonjo ambayo iliwafanya watoto wa fisi, mkewe pamoja na fisi kuuma uwayo wa ndovu kwa zamu. Kitendo cha kuuma uwayo wa ndovu kiliibua taswira hisi ambapo hadhira inaona mawazoni picha ya ndovu mwenye uchungu kutokana na kuumwa na fisi. Taswira hizi zililenga kuonyesha matokeo ya kutodhibiti nafsi. Dondoo hili limethibitisha kuwa kutodhibiti nafsi kuliathiri familia ya fisi hivi kwamba kulikosekana hata mmoja wa kurekebisha mwenzake alipopotoka kimaadili. Muktadha huu ulibainisha kuwa, fisi, mkewe na wana wao wawili ndio wakala wa simulizi kwa kuwa vitendo vya kumla ndovu vilibadilisha mkondo wa usimulizi wa ngano hii. Fisi wangedhibiti nafsi, wangemtunza ndovu mjamzito na urafiki baina ya familia ya ndovu na fisi ungedumishwa. Kinyume

chake ulafi wa fisi ulizua uhasama uliosababisha kuuawa kwa fisi. Mauaji ya fisi ni jazanda inayoelezea mtazamo wa Wandia kuhusu umuhimu wa kudhibiti nafsi ili kuepuka maafa kama haya yaliyowapata kina fisi. Mtazamo huu ndio msingi wa fasiri ya mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia kwa misingi ya udhibiti nafsi.

### 4.2.6 Maadili

Maadili yanahusu mwenendo wa binadamu ambapo maadili ndiyo shughuli ya utendaji (Churchil, 1982). Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, katika N1, mgomo wa wasichana wa kutoongea wala kuolewa na wanaume ulidhihirisha ukiukaji wa maadili ya jamii. Wasichana hawa walipuuza kaida za kitamaduni zinazoongoza mahusiano ya kijinsia, uchumba na ndoa katika jamii ya Wandia. Kiapo cha mgomo dhidi ya wanaume na uundaji wa kaida mpya ya mwongozo wa ndoa ni ukiukaji wa maadili kwa mujibu wa utamaduni wa Wandia. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Hapo zamani za kale paliishi wasichana waliogoma kuongea wala kuolewa na wanaume. Wakasema kuwa yeyote watakayeongea naye ndiye atakayewaoa…wasichana wamekataa kuolewa. Walipokataa kuolewa wakasema`` mtu ambaye wataongea naye ndiye atakayewaoa.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya utafiti unaoshikilia kuwa usimulizi wa matukio hupangwa kwa mfuatano wa kiusababishi. Mfano, kugoma kwa wasichana, wasichana kukataa kuolewa na kisha kula kiapo cha kutoongea na barobaro. Dondoo hili liliibua taswira ya ukaidi wa wasichana walioshiriki mgomo. Hawakujali maadili ya jamii ya Wandia ambayo ndiyo dira ya kuangazia suala nyeti kama hili la ndoa. Wasichana walijitokeza kama wakala wa simulizi na kuendeleza msuko wa ngano hii kwa kukaidi utaratibu wa jamii ya Wandia kuhusu masuala ya uchumba na ndoa.

Maadili ya Wandia yalikitwa kwenye msingi wa ukweli na uaminifu. Muktadha wa uwasilishaji wa N1 ulibainisha kuwa kigezo cha kutimiza ahadi ama masharti ya kuwekeana dau kilikuza maadili ya jamii. Mfano, katika N1, Kabindura na barobaro waliwekeana dau ambapo Kabindura aliahidiwa ndama, fahali na mbuzi watano iwapo angeoa mmoja wa wasichana waliogoma. Kabindura alipofaulu kumwoa msichana, barobaro walitimiza ahadi yao kama walivyomwahidi Kabindura kutokana na msukumo wa kimaadili. Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya

> “Mimi nitaoa mmoja wa wasichana hao wamegoma, na nikimwoa mtanipatia nini?” Kabindura akaambiwa, “Nitakupatia ng`ombe”. Mwenzake akajitolea, “nitakupatia mbuzi watano”… Hapo ndipo Kabindura aliahidiwa ng`ombe, ndama, fahali na mbuzi watano na wale barobaro.

Barobaro walipothibitisha kuwa Kabindura alimwoa msichana, kila mmoja alimpa ahadi yake. Kabindura alipewa ng`ombe, ndama na mbuzi watano. Kutimizwa kwa ahadi hii kulidhihirisha jinsi uaminifu ulivyochangia fasiri ya mwonoulimwengu wa Wandia. Suala la kuchukulia uaminifu kama msingi wa maadili ya Wandia lilijitokeza katika kutimiza masharti ya mgomo wa wasichana. Kwa kuwa mgomo huu ulikitwa kwenye masharti ya kutoongea na wanaume, ni bayana kuwa msichana yeyote ambaye alikiuka masharti ya mgomo aliolewa na mwanamume huyo pasipo kujali vigezo vingine. Mfano, msichana aliyeongea na Kabindura, alimrai amwoe kwa kuwa alikuwa amevunja sheria za mgomo wa wasichana. Data ya utafiti inadhibitisha madai haya; Mfano, msimulizi anaelezea;

> Akapakuliwa chakula, akaambiwa ``sasa kwa sababu tulisema mtu tutakayeenda naye ni yule tutakuwa tumeongea naye. Sasa kwa sababu nimeongea nawe. Twende sasa! ukanioe.”

Taswira mwonjo iliyohusishwa na upakuaji wa chakula ilionyesha kukubalika kwa Kabindura na msichana baada ya kuongea naye. Taswira sikivu ilitumika kuchora picha ya msichana ambaye uaminifu wake kwa kiapo cha ukimya ulimsukuma kumrai Kabindura amwoe. Taswira sikivu iliibua taswira mwendo hususan msichana alipomwambia Kabindura waende akamwoe. Dondoo hili lilionyesha jinsi ukweli na uaminifu kwa kiapo ni dhihirisho la maadili ya jamii ya Wandia. Kabindura alifahamu kuwa jamii yake ilithamini ukweli na uadilifu. Hii ndiyo sababu iliyompa msukumo wa kushurutisha msichana aongee kwa kung`oa mtama kwa kuwa pindi akiongea hangekaidi kuolewa naye. Katika muktadha wa uwasilishaji wa N1, mhimili wa suala la wakala wa simulizi ulijipenyeza. Msichana alipoongea na kuolewa na Kabindura, mkondo wa usimulizi wa hadithi ulibadilika. Wasichana walisitisha mgomo ili kuepuka tanzia ya kuolewa na wanaume wasiopendeza kama vile Kabindura.

Uhakiki wa N2, ulibainisha kuwa maadili yalihusishwa na uzingativu wa miiko katika jamii ya Wandia. Mwiko ni jambo au kitu anachozuiwa mtu kutumia kwa kuogopa kudhurika. Miiko hutumika kuelekeza na kudhibiti mwenendo wa jamii. Hali hii

ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano. Dhana ya ulaji wa `*uura*` katika kifungu kifuatacho:

> Ukila `*uura*` huo wa nguchiro, hakuna jambo jema utakalopata. La! Ndiyo sababu alikuwa akipangusa na kuutupa kwa sababu `*uura*` haupaswi kuliwa na binadamu. Ulikuwa ukiliwa na watu walafi.

Dondoo hili lilithibitisha kwamba mpangilio wa matukio ulizingatia masharti ya mhimili wa nadharia ya utafiti inayosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi. Katika dondoo hili `*uura*` ni sitiari ambayo inaashiria mikosi. Ulaji wa `*uura*` uliibua taswira mwonjo ambayo iliibua taswira hisi ambayo iliashiria mtu bure au mtu wa mikosi. Ilibainika kuwa kuramba `*uura*` ni mojawapo wa miiko ya jamii ya Wandia. Ulaji wa `*uura*` ulikuwa sawa na kukaribisha mikosi maishani kuramba `*uura*` ni kinyume cha maadili.

Maadili yalifungamanishwa na imani na mielekeo ya mtu binafsi (Rennie, 2007). Imani hii inamfanya mtu kuamua kuchukua mkondo fulani wa maisha na kutetea msimamo wake. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kilithibitisha madai haya;

> …Akipita hapo ndipo akaitwa, "msichana huyu njoo unile ukinipondaponda na unaona kuwa tunajila", akasema, "sili vijilavyo"

Dondoo hili liliafiki mhimili wa kinaratolojia unaosisitiza kuwa kuna njia mbalimbali za kusimulia hadithi (Propp, 1928). Hapa njia ya nathari ilitumika kusimulia tukio hili. Aidha, usimulizi huu ulizingatia mfuatano wa matukio kiusababishi. Taswira mwendo iliyobainishwa kwa maneno kama vile ``akipita hapo`` na ``njoo` ilidhihirisha mwondoko. Taswira sikivu iliyobainishwa kwa kuitwa kwa msichana na mwitikio wake kuwa hali vijilavyo inaonyesha msimamo wa Wacuka kuhusu uzingativu wa maadili. Muktadha huu ulionyesha kuwa Wacuka aliongozwa na maadili yaliyokitwa kwenye imani na mtazamo wake kwamba hawezi kula vyovyote vijilavyo. Mtazamo wake ulimfanya atuzwe kwa mapambo ya kila aina. Mtazamo wa jamii ni kwamba maadili mema hutuzwa. Wacuka alijitokeza kuwa wakala wa simulizi kwa kuendeleza maadili ya jamii kwa kudhibiti nafsi na kukataa kula wala kunywa chochote asichojua asili yake.

N5, Mkutano wa Wanyama wa Porini, ilibainisha kuwa msingi wa maadili ya jamii ni umoja na ushirikiano wa jamii ambao ndio msingi wa mfumo wa kijamii. Mtu yeyote akijitenga na jamii ama kutenda kinyume cha ushirikiano wa jamii alichukuliwa kuwa mtu aliyepotoka kimaadili. Hali hiii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya:

> Sungura akajua kuwa hakwenda kuchimba kisima, "nitatumia ujanja wangu" … Wazee wanne walishika doria. Wakamkamata sungura. Sungura alipokamatwa alipelekwa pale ambapo alipaswa kuchomewa.

Utapeli wa sungura ulisimuliwa kinaratolojia kwa kuzingatia mpangilio wa mfuatano wa matukio kiusababishi (Propp,1928). Usimulizi huu ulizua taswira mwendo iliyohusishwa na ushikaji doria pamoja na kukamatwa kwa sungura na kupelekwa alikopaswa kuchomewa. Maelezo haya yalizua taswira hisi iliyojenga picha ya hatari iliyomkabili sungura. Dondoo hili lilithibitisha kuwa kupotoka kimaadili kulichukiwa sana na Wandia na matokeo yake yangeweza kusababisha hata kifo. Wazee wanne waliolinda kisima ndio wakala wa simulizi kwa kufichua uovu wa sungura. Mhusika sungura alitumiwa kijazanda kuonyesha upotovu wa kimaadili katika jamii. Adhabu aliyopewa sungura ilidhihirisha mtazamo wa Wandia kwamba mtu asiyeshirikiana na umma katika masuala muhimu alipaswa kutengwa na jamii. Isitoshe iwapo angetumia ujanja kama alivyofanya sungura alistahiki kuadhibiwa.

Kwa mujibu wa N6, Ndovu na Fisi, ukiushi wa kanuni za maadili ya kijamii husababisha maafa katika jamii. Mfano, dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Watoto wa ndovu walitoroka. Wale waliokuwa tumboni. Wakaponyoka. Wakatoroka wakamwacha mama yao akiliwa… walipomwacha akiliwa, watoto wakatoroka wakaenda kuita ndovu wengine.

Dondoo hili linaafiki mhimili wa kinaratolojia unaoshikilia kuwa usimuliaji wa matukio hupangwa kwa mfuatano wa kiusababishi. Mfano, kuponyoka na kutoroka kwa watoto wa ndovu, kumwacha mama akiliwa na fisi na kuwafahamisha ndovu wengine. Maelezo haya yanaibua taswira mwendo hivi kwamba hadhira iliweza kuona mawazoni watoto wa ndovu wakikimbia. Katika dondoo hili watoto wa ndovu ndio wakala wa simulizi ambao kutoroka kwao kuliathiri ulimwengu wa ngano hii. Uwakala wa watoto wa ndovu ulidhihirika katika mchakato wa kuwajulisha ndovu wengine kuhusu tanzia ya mama yao kuliwa na fisi. Hapa mtindo wa wimbo umetumika kama ifuatavyo.

Ndovu hawa mlienda kukaa
Mkamwacha mama nyikani mwa fisi
Mtoto wa fisi akilia
Niume uwayo wa ndovu
Kila kukicha asubuhi ni;
Ii, Ii! Uwayo, uwayo wa ndovu
Ikifika jioni ni;
Ii! Ii! Uwayo, uwayo wa ndovu.

Matumizi ya wimbo katika dondoo hili yana mshabaha na mhimili wa kinaratolojia unaotambua kuwa kuna jinsi mbalimbali za kusimulia matukio. Wimbo huu ulitoa taswira ya jinsi fisi na aila yake walikaidi maadili ya kijamii na kusambaratisha mshikamano wa jamii. Katika wimbo huu ulafi wa fisi unawapelekea kuuma uwayo wa ndovu hadi wakamla akakwisha.

### 4.2.7 Haki Ya Kijamii

Suala la haki ya kijamii ni suala ambalo lilisawiriwa kisanii katika uwasilishaji wa ngano za Wandia ambapo Fanani alidhihirisha msimamo wake hususan kwa kuunga mkono wasio na uwezo au wanaodhulumiwa. Kitengo hiki cha watu kinachojumlisha watoto, walemavu , na mayatima huinuiliwa juu zaidi ya matarajio ya jamii. Mawazo haya yana mshabaha na kazi ya Mwanzi (2005: 11) anapodokeza kuwa hadhi ya watu hawa dhaifu huinuliwa zaidi ya watu wa kawaida. Suala la haki ya kijamii kama kigezo cha kimsingi cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia lilijitokeza katika N1, N2 na N3 .

N1 ilibainsha kuwa haki ya kijamii ilichukua sura mbili: Mgomo wa wasichana na unyanyampaa dhidi ya walemavu. Mgomo wa wasichana dhidi ya kutoongea wala kuolewa na barobaro uliwanyima barobaro haki ya kuoa. Mgomo huu ulisononesha barobaro kwa kiwango kikubwa hadi ukawa sehemu ya mazungumzo yao. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya:

> Hapo zamani za kale paliishi wasichana waliogoma kuongea wala kuolewa na wanaume. Wakasema kuwa yeyote watakayeongea naye ndiye atakayewaoa. Naye Kabindura akabishana na barobaro. Alipobishana nao akawaambia,`` mimi, kwa sababu mnakataa kwenda kuongea na wasichana hao na wamegoma, hawataki kuolewa. Nitamwoa mmoja wa wasichana hao wamegoma.

Dondoo hili, lilizingatia msingi wa mawazo ya Propp (1928) kwa kuelezea mgomo wa wasichana na matokeo yake kwa kupanga matukio katika mfuatano maalum wa kiusababishi. Mgomo wa wasichana uliwanyima barobaro haki ya kijamii ya kutongoza na kuoa wasichana. Hii ni dhuluma dhidi ya barobaro. Udhalimu huu ulifanikishwa kwa taswira sikivu, taswira mwendo na taswira uoni. Taswira sikivu ilitokana na kiapo cha wasichana. Vivyo hivyo mabishano baina ya Kabindura na barobaro yaliibua taswira sikivu. Taswira hii ilibainisha kuwa mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia ulichukulia ndoa kuwa mojawapo ya haki za kijamii. Hii ndiyo sababu mgomo wa wasichana ulisababisha simanzi miongoni mwa barobaro na jamii. Dondoo hili lilihusisha taswira mwendo. Taswira hii ilidhihirika Kabindura alipowakashifu barobaro kwa kuchelea kwenda kuongea na wasichana. Kabindura aliapa kwenda kuongea na mmojawapo wa wasichana waliogoma kwa lengo la kumwoa . Taswira hii ilidhihirisha ukakamavu wa Kabindura na ufahamu wake kuhusu nafasi ya ndoa katika usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii.

Sura ya pili ya haki ya kijamii ilihusu unyanyapaa dhidi ya watu wenye kasoro za kimaumbile katika jamii. Data ya utafiti ilithibitisha kuwa sampuli ya watu wenye kasoro za kimaumbile kama vile Kabindura walidhalilishwa kutokana na hali zao. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> ``sasa unajua nitaoa mmoja wa wasichana waliogoma``. ``Nawe utaoa aje?,una matege. Hata huvutii yeyote densini, hata wasichana hawaongei na wewe!`` Akaulizwa ,`` sasa utaoaje?`` Akasema,`` nitaoa msichana mmoja wa hao waliogoma, au hao waliopo kwa mgomo

Taswira uoni ilitumiwa kusawiri unyanyapaa dhidi ya watu wenye kasoro za kimaumbile kama vile Kabindura. Swali la barobaro kwa Kabindura liliashiria kuwa kutokana na hali kwamba Kabindura alikuwa na matege , aliambaliwa na wasichana na ingemwia vigumu kuoa. Mtazamo wa barobaro ulikitwa kwenye taswira hisi ambayo ilisawiri mtazamo wa jamii ya Wandia kuhusu walemavu. Muktadha huu ulibainisha kuwa unyanyapaa dhidi ya walemavu uliwanyima haki yao ya kijamii ya kushiriki masuala ya kimsingi kama vile ndoa kutokana na misingi ya kasoro za kimaumbile. Ujio wa Kabindura ni jazanda iliyotumika kusuluhisha tatizo hili na kuwarejeshea walemavu haki yao. Ilipodhihirika kuwa Kabindura alimwoa mmoja wa wasichana waliogoma, unyanyapaa dhidi ya walemavu uliendelezwa zaidi. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> Wakamwambia msichana,`` ulikawia hivyo muda huo wote ukimngojea Kabindura ilhali ana matege na hata hapendezi yeyote densini?”

Dondoo hili liliashiria kuwa, Kabindura aliyewakilisha walemavu alinyanyapaishwa na kunyimwa haki yake ya kijamii. Suala hili lilisawiriwa kwa taswira sikivu hususan barobaro walipomwuliza msichana kwa nini alikawia hivyo mwishowe akaolewa na Kabindura aliyekuwa na matege. Ndoa ya Kabindura na msichana ilidhihirisha mtazamo wa jamii ya Wandia kuwa kila mwanamume alipaswa kuoa licha ya kuwa na kasoro zozote za kimaumbile ( Waita, 2003, Kenyatta, 1938) . Kabindura alijitokeza kuwa wakala wa simulizi kwa kuwa ndoa yake iliathiri ulimwengu wa hadithi na kuendeleza ploti.

Kusitishwa kwa mgomo kulibainisha kilele cha unyanyapaa dhidi ya walemavu. Data ya utafiti ilithibitisha haya katika kifungu kifuatacho;

> Sasa akaambiwa amefanya vizuri. Kuhusu mgomo wa wasichana, wakaitana tena ``Njooni tusitishe mgomo kwa sababu…. Wasichana wale wote wazuri ndio wanaolewa na mang`ong`oi….barobaro wasio na hali wala fasiri, wasiovutia, wasioweza hata kujitetea.”

Kifungu hiki kilidhihirisha mtazamo wa Fanani kuwa mgomo wa wasichana haukuwa na msingi wowote. Sadfa ya wasichana wote wazuri kuolewa na barobaro wasio hali wala fasili ilitumika kufidia barobaro ambao walikuwa wamepokonywa haki yao ya kijamii.

Uhakiki wa N2, Wacuka, Kamwagirwa na Kibuyu cha Baba ulidhihirisha kuwa haki ya kijamii iliambatanishwa na wajibu wa mtu binafsi . Mathalani, mtu aliyetenda mambo kwa kuzingatia maadili ya jamii, alituzwa ilhali aliyetenda kinyume cha maadili ya jamii aliadhibiwa. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> …akipita hapo ndipo akaitwa, “msichana huyu, njoo unile ukinipondaponda na unaona kuwa tunajila.” Akasema “sili vijilavyo.” Hizo ni fiwi kwa sababu ametoka kwa njegere. Sasa amekuja kwa uji. Sasa emekuja kwa fiwi…. Ametoka kwa `uura`

Taswira mwendo, taswira mwonjo pamoja na taswira sikivu zilitumika kuelezea kipengele cha haki ya kijamii kama sehemu ya usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia. Maneno kama vile akipitia hapo, ‘njoo’ na ‘alitoka’ yalitumika

kuibua picha ya mwondoko katika nchi ya ajabu ambapo baadhi ya vyakula vilikuwa vimenafsishwa. Wacuka alipoitwa na baadhi ya vyakula, taswira sikivu ilitumika kuonyesha msimamo wake na udhibiti nafsi. Alijibu,`` ``sili vijilavyo``. Hapa taswira mwonjo ilitumika kama chambo cha kumvutia Wacuka kwenye majaribio lakini Wacuka alishinda yote.

N2, ilibainisha kuwa uzingativu wa maadili ya jamii hutuzwa na jamii kama njia ya kuwamotisha kuendelea kutenda wema. Hii ni haki ya kijamii. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Kondoo wangekatwa mkia na kisha kukatwakatwa vipande vidogo vidogo na kukaangwa jikoni. Vipande hivyo vingekatwa vidogo vidogo kisha vinaletwa kwa sahani. Sasa uko kwa mtihani. …sasa ukiwa na kipande kimoja, naye mwenyeji ana vipande viwili, ukiwa na viwili, mwenyeji ana vitatu. Yule akiwa na vinne nawe una vitatu. Vipande vilipokwisha wakalala. Sasa amemaliza mtihani . Wameenda kulala. Asubuhi aende afunguliwe ghala kama hili. Lina mapambo. Lina mikufu. Akaambiwa,`` jaribu jipambe kwa chochote unachotaka. Vitu vyote.

Dondoo hili lilibainisha kuwa Wacuka alijitokeza kuwa wakala wa simulizi ambaye aliendeleza msuko wa ngano hii kwa kuzingatia maadili. Ushindi wa Wacuka ulielezewa kwa njia ya nathari ambayo ni mhimili mojawapo wa nadharia ya naratolojia. Aidha maelezo haya yalizingatia mfuatano wa matukio kwa njia ya kiusababishi (Propp, 1928). Ilibainika kuwa taswira uoni na taswira hisi ndizo taswira zilizotumika aghalabu kubainisha kushinda au kushindwa kwa mtu binafsi. Mfano, japo Wacuka aliona na kutamani vipande vya nyama ya mkia wa mbuzi, alikula kwa utaratibu, akaonyesha heshima hadi akapachikwa lakabu ya `Mgeni mwenye nyumba. Mgeni kama huyu alistahiki kutuzwa' . Wacuka alipelekwa kwenye chumba chenye mapambo na kupambwa kwa pete, bangili na mikufu. Taswira mwendo na taswira uoni zilitumika kufanikisha usawiri wa haki ya kijamii kwa Wacuka ambaye alishinda majaribio yote. Kutuzwa kwa Wacuka kuliashiria kupewa haki ya kijamii, suala ambalo lilitumiwa kusawiri mwonoulimwengu wa Wandia. Kwa upande mwingine ,adhabu ilitolewa kwa mtu yeyote aliyeenda kinyume cha maadili ya jamii. Adhabu hii ilitolewa ili kuwa funzo kwa wengine wenye tabia kama hiyo. Hali hii, ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;'

> Msichana akaambiwa, "hii ndiyo sababu ukatunukiwa maganda . Iwapo `uura` wenyewe ulipokuangukia ulikula…sasa iwapo uliramba na ukaenda ukila chakula" … "Ndio, nilikuwa nikila chakula na kunywa

> uji." Ndiyo sababu ulipewa maganda…maganda ni msichana asiyeweza kudhibiti hisia zake , amefanya mapenzi na kupata mtoto.

Taswira uoni, taswira sikivu na taswira hisi zilitumika kusawiri haki ya kijamii kama sehemu ya fasiri ya mwonoulimwegu wa kijamii wa Wandia. Taswira sikivu ilitumika kumwelezea Kamwagirwa sababu ya kuadhibiwa kwa kutuzwa maganda. Taswira uoni ilitoa picha kamili ya adhabu aliyopewa mtu ambaye alikaidi maadili ya jamii. Vazi la maganda lilionekana wazi. Adhabu hii ni stahiki ya Kamwagirwa kwa kukiuka maadili ya jamii na ndio haki ya kijamii kwake.

Suala la haki ya kijamii lilijitokeza katika N3 kutokana na adhabu iliyompata Muya kutokana na kutowajibika kwake. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika kifungu kifuatacho;

> ``… siku moja , Muya alipotoka densini akakuta hakuna mtu. Akakaa, akakaa, akaathiriwa na funza . Akaathiriwa na njaa. Akasema, ``Sasa dada yangu angekuwa hapa, si ningekuwa nikishiba kama zamani? Ningekuwa nimetolewa funza hawa, sasa nitatolewa na nani? sasa nitafanya nini? Sasa nitaamka niende kumtafuta kupitia njia aliyopitia.*"*

Kifungu hiki kilidhihirisha kutowajibika kwa Muya na matokeo yake yakaelezewa kwa kuzingatia mpangilio wa mfuatano wa matukio kiusababishi (Propp 1928). Matokeo haya ambayo yalichukua sura ya adhabu ni kama vile njaa na kutekenywa na funza. Kupitia balagha, Muya alishiriki mjadala na nafsi yake na kujutia laiti dada yake angekuwepo hangeathiriwa na njaa ama funza. Taswira uoni ilidhihirisha athari za njaa na funza na kubainisha adhabu aliyopata Muya kutokana na kutowajibika kwake. Kufikia hapa, ni dhahiri kuwa Muya alipewa haki ya kijamii na alistahiki adhabu hiyo. Mjadala kuhusu haki ya kijamii ulithibitisha kwamba haki ya kijamii ni kipengele muhimu cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia. Usawiri huu ulijumlisha uzingativu wa maadili ya kijamii ambayo yalifanya wahusika watuzwe. Aidha, ukiukaji wowote wa maadili ya jamii uliadhibiwa vikali.

### 4.2.8 Tabaka

Kwa mujibu wa Weber (1947), kuwa na mali ama kukosa mali ni msingi wa uainisho wa utabaka. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, suala la matabaka kama kipengele cha usawiri wa mwonoulimwemgu wa kijamii lilijitokeza katika N1 na N3. N1, Kabindura, mgawanyiko wa jamii kitabaka ulitumia kigezo cha umiliki wa mali.

Hapa tabaka la juu lilinasibishwa na uwezo wa kulipa mahari huku tabaka la chini likishindwa kulipa mahari. Dondoo lifuatalo lilibainisha haya;

> …Hata watu walikuwa wanalipiwa mahari na ukoo iwapo mtu ni maskini… ndio iwapo mtu hana chochote. Watu wanachanga kila mtu mbuzi mmoja mmoja… Ndio yule hana mbuzi angetoa shilingi thelathini, ndizo zilikuwa zikinunua mbuzi.

Dondoo hili lilichora taswira ya mtu wa tabaka la chini ambaye hana chochote. Ilibidi ukoo uhusishwe katika ulipaji wa mahari ili maskini apate mke. Kadhia ya kuchanga mbuzi ilielezewa kinathari na kutoa taswira kamili ya wana tabaka la chini.

N1, ilijumlisha wafanya kazi wa kibarua katika tabaka la chini na kuwaweka waajiri wao katika tabaka la juu. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> Tena mnataka asiende kuwa,`*Ndũrua*` kwa wenyewe… akienda kwa wenyewe kuajiriwa kazi…
> Huyo ndiye aliitwa *, `ndũrua`.*

Dondoo hili lilitumia istilahi 'wenyewe' kurejelea mabwanyenye wa tabaka la juu wenye uwezo wa kuajiri maskini. Istilahi `*ndũrua*` ilimaanisha mwanamume aliyetoka kwao na kuhamia kwingine alikoajiriwa kazi ya kibarua ambayo haikumpa mtu hadhi yoyote. Kazi hii ilidharauliwa na Wandia. Hii ndiyo sababu jamii ya Wandia ilipendelea kumchangia maskini ili angaa apate mke badala ya kwenda kuwa `*ndũrua*`. Inayumkinika kuwa kitengo cha `*ndũrua*` ndicho kitengo cha chini mno katika uainishaji wa watu wa tabaka la chini.

N3, ilidhihirisha kuwa suala la matabaka lilibainika wazi kutokana na uhusiano kati ya waajiri na waajiriwa. Data ya utafiti inadhihirisha haya katika dondoo lifuatalo;

> Cuuaaii! Ndege wa shamba hili
> Paeni! Hamfahamu maskini na matajiri
> Sawa na Wacinji wetu. Anayenilaza kwenye majivu
> Na ninapokula, nalia kwenye kigae
> Aaai! Cuuaaii!
> Paeni.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia unaotambua kuwa kuna jinsi mbalimbali za kusimulia matukio. Dondoo hili lilitumia mtindo wa maghani kusimulia uhusiano kati ya tabaka la juu na tabaka la chini hususan waajiri na waajiriwa. Dhamira ya maghani hii ni kuonyesha kuwa tofauti za kitabaka hazifai kuwepo katika jamii.

Dhana hii ilifanikishwa kupitia jazanda ya ndege ambao walipoharibu mtama mashambani hawakutambua tofauti kati ya shamba la tajiri na maskini. Kulingana na ndege, mtama ni mtama, uwe wa maskini au tajiri. Kutobagua huku kunaashiria usawa wa binadamu. Hata hivyo ndege walifukuzwa na kuamrishwa kupaa. Matumizi ya ndege kijazanda ni uovu. Hivyo basi uovu wa utengano kati ya maskini na matajiri ulipaswa kuondolewa ili kudumisha utangamano wa kijamii.

Aidha, dondoo hili lilisawiri mikinzano kati ya tabaka la juu na tabaka la chini. Mabwanyenye waliwadhulumu vibarua kwa kuwalaza kwenye majivu badala ya kitanda na kuwapakulia chakula kigaeni badala ya sahani. Katika maghani hii, Muya alilalamikia hali hii ambapo hakuchukuliwa kama mtu wa maana bali kama taka. Motifu ya utabaka katika dondoo hili ilifanikishwa kwa kutumia taswira sikivu ambapo Muya aliamuru ndege wapae na kulalamikia uhusiano wa maskini na tajiri. Aidha taswira hisi iliibua uchungu wa maisha ya maskini mikononi mwa mabwanyenye.

**4.3 Mwonoulimwengu wa Kiuchumi wa Wandia**

Uchumi ni ujumla wa shughuli zote za binadamu zinazolenga kutosheleza mahitaji yao. Shughuli hizi zinajumulisha uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa bidhaa pamoja na kutolewa kwa huduma kwa njia mbalimbali. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti ambapo uchumi ulijitokeza kama kigezo cha kimsingi katika usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia. Mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia ulihakikiwa kutokana na shughuli za kiuchumi katika ngano teule. Uhakiki wa usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia ulikitwa kwenye shughuli mahususi za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji, biashara na kibarua.

**4.3.1 Kilimo**

Suala la kilimo, ambalo ni kipengele muhimu cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia, lilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, suala la kilimo liliangaziwa katika N1, N2 na N3. Kilimo cha mtama kiliendelezwa na kutumika kama kibainishi cha misimu katika N1. Mawazo haya yana mshabaha na kazi za Munene (1995) aliyetambua nafasi ya kilimo cha mtama katika ubainisho wa misimu. Mfano, katika N1, mgomo wa wasichana ulitekelezwa katika kipindi cha kuwinga ndege wasiharibu mtama. Mpango wa Kabindura wa kushurutisha msichana aongee naye

ulitekelezwa shambani alipokuwa msichana akiwinga ndege. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Ndipo Kabindura akakuta msichana akiwinga mtama usiliwe na ndege. Akaenda. Hata hakuongea na msichana huyo. Akaenda akaanza kung`oa mtama upande ambapo msichana hakuwa huku akiimba.

Dondoo hili, lilizingatia mpangilio wa mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, Kabindura kukuta msichana, kisha kuanza kung`oa mtama. Dondoo hili lilithibitisha kwamba jamii ya Wandia ilisisitiza umuhimu wa kilimo hivi kwamba wasichana walitengewa jukumu la kuwinga ndege miongoni mwa majukumu mengine. Kilimo kilifungamanishwa na mwonoulimwengu wa jamii ya Wandia hali ambayo ilimfanya Kabindura kutumia uhalisia huu wa kijamii kumnasa msichana aliyegoma. Kutokana na msukumo wa mwonoulimwengu wa kiuchumi kuhusu kilimo, inamlazimu msichana kuongea na kwenda kinyume cha masharti ya mgomo wa wasichana. Mathalan, msimulizi anaelezea;

> Msichana akamwambia Kabindura, "Wacha kung`oa mtama. Njoo uniambie unachotaka kwa kuwa sasa unakosea. Kwa sababu umeng`oa mtama sasa nitakuja kupigwa na `*nyanya*`."

Usimulizi wa matukio katika dondoo hili ulizingatia kanuni ya mfuatano wa matukio kiusababishi kulingana na mhimili wa nadharia ya naratolojia. Maelezo haya yalijenga taswira uoni ambapo hadhira ilimwona mawazoni msichana akimrai Kabindura asing`oe mtama. Dondoo hili lilibainisha kuwa kilimo kama kigezo cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi kina nguvu hata za kushurutisha msichana kutenda kinyume cha kiapo. Kabindura alifahamu fika kuwa kung`oa mtama ni sawa na kugusa neva ya uchumi wa familia na jamii kwa jumla na msichana sharti angeongea. Kabindura alijitokeza kama wakala wa simulizi. Kitendo chake cha kung`oa mtama ambacho kilimshurutisha msichana kuongea kilitumika kusisitiza nafasi ya kilimo katika usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi. Uwakala huu wa simulizi ulibainisha mtazamo wa msimulizi na jamii ya Wandia kuhusu mwonoulimwengu wa jamii ya Wandia kwa kutumia kipengele cha kilimo.

N2, ilitaja baadhi ya vyakula kama vile pure, njegere, fiwi na uji ambao ulitokana na unga wa mahindi. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya:

> Huko akakuta kuna uji unaojipika ukijinywa. Kuna njegere zinazojipika, zikijiponda huku zikijila…kuna pure na uji.

Dondoo hili lilithibitisha kuwa vyakula hivyo vilitokana na mazao ya kilimo.

Uwepo wa vyakula mbalimbali katika ngano hii ni ithibati tosha kuwa kilimo kilikuwa msingi wa usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia.

N3, ilidhihirisha kuwa suala la kilimo liliambatanishwa na suala muhimu la misimu hususan masika na vuli. Ufahamu wa misimu ulimwezesha Cinji kung`amua mbinu ya kutapakaza mbegu za kila namna ili zikiota, mimea hiyo iwe kielekezi kwa Muya atakapokuwa akimtafuta. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Haya wakakaa huku Muya akiambiwa, ``utanitafuta wewe na njia nitakayopitia nitakuelezea. Nitabeba vitu vyote. Nibebe mtama, fiwi, njegere, maharagwe na wimbi. Nitabeba chochote kitakachopatikana ili ile njia utakayopitia ukinitafuta uione ikiwa imeota mimea hii.

Usimulizi wa matukio katika dondoo hili ni wa kinathari na ulizingatia mfuatano wa matukio kiusababishi kulingana na nadharia ya naratolojia. Taswira uoni ilijenga picha ya Cinji akiwa amebeba aina tofauti za mbegu. Taswira hii vilevile ilionyesha hali itakavyokuwa baada ya mbegu kuota. Hadhira iliweza kuona akilini picha ya mimea hiyo kando kando mwa njia. Dondoo hili lilibainisha kuwa, Cinji alikuwa akishiriki kilimo cha mazao yaliyotajwa. Cinji alipoangusha mbegu za wimbi, mtama, fiwi, njegere na maharagwe alikuwa na matarajio kuwa mbegu hizi zikiota, mimea yenyewe ingetumika na Muya katika mchakato wa kumtafuta. Mwangusho wa mbegu uliashiria matumaini ya msimu wa mvua na aidha ishara ya heri na fanaka. Cinji alijitokeza kama wakala wa simulizi ambaye alitumia misimu kuonyesha fasiri ya mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia.

N3, ilihusisha suala la matabaka na kilimo. Weber (1947) alidokeza kuwa kumiliki mali ni kigezo cha kimsingi katika uainishaji wa matabaka. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mathalan, mtindo wa maghani ulitumika kusawiri uhusiano wa matajiri na masikini. Muya anaghana;

> Cuaiii! Ndege hawa wa shamba hili
> Paeni! Paeni’Hamtambui masikini na matajiri
> Sawa na Wacinji wetu anayenilaza kwenye majivu
> Na ninapokula, nalia kwenye kigae

Matumizi ya maghani haya yaliafiki mhimili wa kinaratolojia unaoshikilia kuwa kuna njia mbalimbali za kusimulia matukio. Katika dondoo hili, taswira uoni ilijenga akilini mwa hadhira picha ya ndege wengi wakiharibu mtama mashambani. Matumizi ya maneno masikini na matajiri ni sitiari iliyoonyesha mgawanyiko wa jamii ya Wandia kitabaka. Aidha, taswira uoni ilichora picha ya Muya akilalia majivu na kulia kigaeni, taswira ambayo iliashiria tabaka la chini na kubainisha kuwa kulikuwa na matajiri ambao walijitajirisha kutokana na kilimo. Maghani haya yaliashiria kuwa kilimo kama kipengele cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia ni kibainishi cha hadhi ya kijamii na utabaka. Mtazamo wa jamii kuhusu utabaka ulibainika hasa Muya aliposuta ndege kwa kutochagua shamba la tajiri wala la maskini na kuwalinganisha na Wacinji aliyemlaza majivuni na kumlishia kigaeni. Muya ambaye ni wakala wa simulizi alibainisha mtazamo kuwa utabaka haupaswi kuwepo katika jamii.

Diskosi ya kilimo katika N1, N2 na N3 ilibainisha kuwa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia umekitwa katika mhimili wa kilimo. Matokeo ya utafiti huu yana mshabaha na kazi za Kenyatta (1938) na Munene (1995). Kulingana na kazi hizi, kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Agikuyu wakiwemo Wandia. Matokeo ya utafiti huu yalitilia mkazo mhimili wa kilimo na umuhimu wake katika kuafikia mpango wa maendeleo wa kaunti ya Kirinyaga wa 2023-2027. Katika mpango huu kilimo kilipewa thamani na nafasi kubwa katika mpango wa maendeleo ya kaunti ya Kirinyaga. Hii ina maana kuwa kufikia sasa kilimo kiliendelea kuwa kipengele muhimu cha fasiri ya mwonoulimwengu wa Wandia.

### 4.3.2 Ufugaji

Ufugaji ni kazi ya kufuga au kutunza wanyama pamoja na ndege. Ruwaza ya mpango wa maendeleo ya Kaunti ya Kirinyaga (2023-2027: 40) ilisisitiza kuwa ufugaji ni shughuli muhimu ya kiuchumi ya Wakirinyaga. Kenyatta (1938: 64-67) alihusisha ufugaji wa ng`ombe, mbuzi na kondoo na fasiri ya mwonoulimwengu wa kiuchumi kwa kurejelea thamani ya mifugo hawa katika fasiri ya hadhi ya mtu. Data ya utafiti huu ilidhihirisha aina mbalimbali za ufugaji wa mifugo katika usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule. Mifugo hawa ni pamoja na ng`ombe, mbuzi, kondoo na kuku. Fasiri ya mwonoulimwengu wa Wandia kwa misingi ya ufugaji ilijitokeza katika N1 , N2 na Na 4.

N1, ilidhihirisha kuwa ufugaji wa mbuzi, ng`ombe na kondoo uliendelezwa. Ufugaji ni kipengele muhimu cha fasiri ya mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia. Fasiri hii ilitokana na majukumu yaliyotwikwa umiliki wa mifugo kama vile ng`ombe na mbuzi. Jukumu la kwanza ni kuwekeana dau kama njia ya kuthibitisha kuwa mhusika angeweza kutekeleza jambo lililoaminika kuwa ngumu. Mfano, barobaro walimwekea dau Kabindura iwapo angefaulu kumwoa msichana aliyegoma. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Sasa, Kabindura akasema, `` sasa kwa sababu wamekasirishwa na barobaro, mimi nitaoa msichana mmoja wa hao waliogoma. Na nikimwoa mtanipatia nini? Kabindura akaambiwa, ``Nitakupatia ndama! ``. Mwenzake akajitolea, `` Nitakupatia mbuzi watano``, na sababu walikuwa watatu, ``nitakupatia fahali…"

Dondoo hili lilibainisha kuwa suala la kuwekeana dau lilisimuliwa kwa njia ya nathari. Usimulizi huu uliibua taswira sikivu iliyotokana na mazungumzo kati ya Kabindura na barobaro. Makubaliano ya pande zote mbili, yalizua taswira uoni iliyowezesha hadhira kuunda picha ya kifikra kuhusu ndama, mbuzi na fahali. Taswira hii ilidhihirisha thamani ya chombo kilichotolewa. Muktadha wa uwasilishaji wa N1 ulithibitisha kuwa ng`ombe na mbuzi walikuwa na thamani ya juu hivi kwamba barobaro walimwahidi kwa sababu ya thamani yazo. Barobaro hawa ni wakala wa simulizi ambao waliibua taswira ya thamani ya mbuzi na ng`ombe katika jamii ya Wandia. Jukumu la pili kwa mujibu wa ngano hii ni kulipia mahari. Mtazamo wa msimulizi na jamii nzima kuhusu thamani ya mbuzi ulipelekea jamii kuchanga mbuzi mmoja mmoja ili barobaro maskini apate mke. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya:

> Hata watu walikuwa wanalipiwa mahari na ukoo iwapo mtu ni masikini…watu wangechanga kila mtu mbuzi mmoja mmoja.

Dondoo hili lilithibitisha nafasi ya mbuzi katika ulipaji wa mahari. Jamii nzima ilihusishwa kuchangia masikini mbuzi ili kumlipia mahari. Muktadha wa uwasilishaji wa N1 ulibainisha jinsi umiliki wa ng`ombe na mbuzi ulivyoambatanishwa na ulipaji wa mahari. Hadhira ilisisitiza kuwa Kabindura alipata mali ya kulipia mahari. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Sasa ataenda kupeleka mahari? Kabindura kwanza atakaa na mali yake ili apeleke zikiwa nyingi.

Utafiti huu ulichukulia kuwa baada ya mifugo kuzaana, Kabindura angechukua sehemu ya mifugo kulipia mahari na kubakisha mifugo wengine ili waendelee kuzaana.

Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa kulikuwa na uhusiano wa moja kwa moja kati ya umiliki wa mifugo na fasiri ya mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia. Aidha, N1, ilidhihirisha kuwa umiliki wa mifugo ulimithilishwa na kuwa tajiri. Hapa mifugo walikuwa chanzo cha kuwa na hadhi. N1, ina mshabaha na kazi ya Kenyatta (1938) anapodai kuwa mifugo walikuwa kigezo muhimu cha kukadiria hadhi ya mtu.

N2, ilitaja ufugaji wa Kondoo. Kulingana na ngano hii, umuhimu wa kondoo ni kulisha jamii. Nyama ya mkia wa kondoo iliandaliwa wageni kama njia ya kuonyesha heshima kwao na kukadiria utu wao. Kifungu kifuatacho kinathibitisha ukweli huu;

> Kondoo wangekatwa mkia na kisha kukatwakatwa vipande vidogo vidogo na kukaangwa jikoni. Vipande hivyo vingekatwa vidogo vidogo kisha vinaletwa kwa sahani. Sasa uko kwa mtihani… sasa ukiwa na kipande kimoja, naye mwenyeji ana vipande viwili, ukiwa na viwili mwenyeji ana vitatu.

Dondoo hili liliibua taswira uoni iliyoiwezesha hadhira kuona mawazoni vikaango vya vipande vya nyama ya mkia wa kondoo. Taswira hii ilipisha taswira mwonjo ambayo ilihusiana na sahani yenye vipande vya nyama pamoja na ulaji wake. Dondoo hili lilibainisha kuwa ufugaji wa kondoo ulifungamanishwa na utoshelevu wa chakula na kukirimu wageni. Mwenyeji ndiye wakala wa simulizi kwa sababu makaribisho yake kwa wageni yalibainisha umuhimu wa ufugaji wa kondoo katika usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia.

N4, ilibainisha kuwa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia ulihusisha ufugaji kama shughuli muhimu ya kiuchumi yenye uwezo wa kuleta mshikamano wa kijamii. Mshikamano huu ulitokana na kushirikiana kuchunga mifugo kwa pamoja. Data ya utafiti inadhihirisha madai haya katika kifungu kifuatacho;

> Hapo zamani za kale palikuwa na barobaro wawili. Mmoja aliitwa Kanyonyo na mwenzake Thigiti. Watu hao walikuwa na urafiki wa dhati kwa sababu walikuwa katika Kitongoji kimoja…Thigiti wakaishi pamoja na Kanyonyo. Kila mmoja alikuwa na ng`ombe wake. Ng`ombe hao wao walipoanza kuzaana, ng`ombe wa Kanyonyo akazaa naye wa Thigiti akazaa pia.

Dondoo hili linaafiki mhimili wa kinarotolojia unaosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, Uhusiano wa Kanyonyo na Thigiti, ufugaji wa mifugo kwa zamu na wizi wa ndama. Kutokana na dondoo hili, ni dhahiri kuwa mwonoulimwengu wa

Kiuchumi wa Wandia ulithamini ujima. Hii ndiyo sababu Thigiti na Kanyonyo walishirikiana kuchunga mifugo wao kwa zamu kutokana na falsafa ya ujima. N4, ilibainisha kuwa shughuli za ufugaji zikiendeshwa kiujima wakati mwingine ziliweza kuzua migogoro ya kijamii kutokana na thamani iliyotwikwa mifugo na Wandia. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano,

> Mtu aliyekuwa na shida sana ni Thigiti kwa sababu alitamani mali ya Kanyonyo kwa sababu aliona Kanyonyo alikuwa ametunza ng`ombe wake ilhali wake hawakuwa wamenona… Alipoona kuwa ng`ombe wa Kanyonyo amezaa ndama mzuri na wake akazaa ndama asiyevutia, akabadilishana ndama hao.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa kinaratolojia unaoshikilia kuwa kuna njia mbalimbali za kusimulia matukio. Mfano, wizi wa ndama wa Kanyonyo ulisimuliwa kwa njia ya nathari. Taswira uoni ilibainisha tofauti kati wa ng`ombe wa Kanyonyo waliotunzwa vizuri na wa Thigiti waliotelekezwa na kukondeana. Thigiti, alichukua nafasi ya wakala wa simulizi kwa kubadilisha ndama wa Kanyonyo. Uwakala huu wa simulizi unabadilisha mpangilio wa utunzaji wa mifugo pamoja na kuathiri mshikamano wa kijamii. N4 ilitoa tahadhari kwamba kuna uwezekano wa kuweko kwa chuki na uadui kutokana na ushirikiano wa utekelezaji wa shughuli muhimu ya kiuchumi kama vile ufugaji. Mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia ulidhihirisha kwamba ni muhimu kutekeleza shughuli muhimu kama vile ufugaji peke yako pasipo kuhusisha wengine ili kuepuka migogoro ya kijamii ambayo ilikitwa kwenye misingi ya kiuchumi.

### 4.3.3 Biashara

Biashara ni shughuli ya ununuzi na uuzaji wa bidhaa. Biashara kama kipengele cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, katika N1, biashara ya ununuzi na uuzaji wa mbuzi ilijitokeza. Kifungu kifuatacho kinathibitsha haya;

> Na iwapo mtu hana chochote na ni *`mang`ong`oi`* watu wangechanga kila mtu mbuzi mmoja mmoja…Ndio yule ambaye hana mbuzi angetoa shilingi thelathini. Ndizo zilikuwa zikinunua mbuzi… Ndio. Wewe utoe shilingi thelathini iwapo huna mbuzi… Walikuwa rahisi kwa kuwa ungeuza debe ya mtama.

Dondoo hili lilionyesha nafasi ya biashara katika usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia. Maelezo haya yaliibua taswira mwono ambapo hadhira iliwezeshwa kuunda picha akilini ya kuchanga mbuzi pamoja na ununuzi wa debe ya

mtama kwa shilingi thelathini. Dondoo hili lilibainisha kuwa kilimo cha mtama kilichochea biashara ya mtama ambao ulinunuliwa kwa pesa. Thamani ya debe moja ya mtama ilibainishwa kuwa shilingi thelathini. N1, ilithibitisha kuwa biashara ya uuzaji na ununuzi wa mtama ilitumika kama kipengele muhimu cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia.

### 4.3.4 Kibarua

Kibarua ni kazi ya muda ambapo mfanyakazi hulipwa kwa kutwa ama mwisho wa mwezi. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti ambapo kibarua kilitumika kama kigezo cha usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia. Mfano, maudhui ya kibarua yaliangaziwa katika N1 na N3.

N1, ilibainisha kuwa kazi ya kibarua ilidharauliwa na yeyote ambaye alishiriki kazi ya kibarua alidharauliwa na watu wa familia yake. Hii ndiyo sababu ukoo ulikuwa ukichangia mtu mbuzi ili aoe, awajibike na asiende kuajiriwa kama kibarua. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Mmeitishwa bidhaa za kuchangia mtu huyu wenu. Tena mnataka asiende kuwa `*ndũrua*` kwa wenyewe. Kuajiriwa kazi… Sasa huyo ndiye aliitwa `*ndũrua*` barobaro akitoka kwao aende kuajiriwa.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia uliosisitiza kuwa msimulizi hadhamirii kusimulia tukio tu bali huonyesha mtazamo wake kuhusiana na suala analosimulia. Hapa mtazamo wa Fanani Wanjira wa Rukenya ulibainika kuwa mwanamume alipaswa kujitegemea ili asiwe kibarua kwa wenyewe. Dondoo hili lilithibitisha kuwa istilahi `*ndũrua*` ni kisawe cha kibarua katika jamii ya Wandia. Ilibainika kuwa kibarua si kazi mbaya lakini Wandia walichukia mwanamume kwenda kutumikishwa kwa wenyewe. Hapa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia uliegemezwa kwenye dhana ya kujitegemea. Huu ndio mtazamo wa msimulizi pamoja na Wandia kwa jumla.

N3, ilithibitisha kuwa kibarua ni chanzo cha riziki hasa kwa maskini. Kibarua ni kazi ya kijungu jiko na haithaminiwi na jamii. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, msimulizi anaelezea;

> …Naenda kumtafuta dada yangu. Hata nikienda kibarua… Akaenda, akaenda akakuta nyumba akapewa kazi. Alipopewa kazi ikawa kwamba kazi yake ni kuchunga mifugo… akachunga mifugo kwa muda.

Harakati za Muya za kutafuta kazi ya kibarua zilisimuliwa kinathari kwa kuzingatia mhimili wa kinaratolojia wa mfuatano wa matukio kiusababishi. Dondoo hili lilitumia taswira mwendo kutuchorea picha ya Muya akienda kutafuta kibarua. Muya alijitokeza kama ajenti wa simulizi ambaye badala ya kumtafuta dada yake kwa kutumia vielekezi vya mimeaa iliyoota njiani kama alivyoelekezwa, aliamua kutafuta kazi ya kibarua. Uwakala wa simulizi ulitanguliza kuwepo kwa kazi ya kibarua katika jamii ya Wandia. Aidha, mfanyakazi wa kibarua hathaminiwi wala kuheshimiwa. Ubinadamu wake unabezwa na kutokana na kutotunzwa vizuri afya yake inadhoofika. Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> …akiwa malishoni, alishiriki uzungumzi nafsia, ``Tungekuwa na Cinji ningekuwa na shibe. Tungekuwa na Cinji ningekuwa nikitolewa funza…Tungekuwa na Cinji ningekuwa nikifuliwa nguo. Haya. Akakaa huko kwa mtu huyo. Kisha akajua ``hapa sikai` Akaondoka. Akapewa pesa zake.

Matumizi ya balagha katika dondoo hili, yalizua taswira uoni ambayo ilichora picha ya Muya ambaye alidhoofika kiafya kutokana na njaa,funza na uchafu. Taswira hii ilionyesha athari za kuwa kibarua. Hapa balagha ilitumika kuonyesha kuwa mfanyakazi wa kibarua hatunzwi vizuri, hatolewi funza na nguo zake hazifuliwi kumaanisha angeendelea kuteseka. N3, ilimsawiri Muya kama wakala wa simulizi kwa kuchukua hatua nyingine ya kuacha kazi na kuanza kumtafuta dada yake Cinji ili kuepuka mateso. Muktadha wa uwasilishaji ulibainisha kuwa katika mchakato wa kumtafuta Cinji, sadfa ilimfikisha hadi kwa Cinji na akapewa kibarua cha kuwinga ndege. Cinji hakumtambua Muya lakini Muya alimfahamu.’ Msimulizi ameelezea;

> Akapewa kiti. Akaketi. Akaulizwa, “Mzee unataka nini? Ninataka kazi.” Huku kazi tuliyonayo ni ya kuwinga ndege. Utaweza kuwinga ndege? “Akamwambia,” ndio nitaweza”.

Dondoo hili lilitumia mbinu ya dayolojia kufanikisha mazungumzo baina ya Muya na Cinji. Dayolojia hii iliafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza kuwa kuna njia mbalimbali za kusimulia matukio katika ngano. Dondoo hili lilithibitisha kuwa Muya alipewa kibarua cha kuwinga ndege. Hii ni awamu ya pili ya Muya kuajiriwa kazi ya kibarua ili kumwezesha kupata riziki. Mateso na madharau

yanayoambatanishwa na kazi ya kibarua yalirejelewa kupitia kwa maghani ya kuwinga ndege. Muya anaendeleza maghani ;

> Ndege hawa wa shamba hili
> Paeni
> Cuaaii!
> Aiyaya! Uuu!
> Hamfahamu kati ya maskini na matajiri
> Sawa na Wacinji wetu.
> Anayenilaza kwenye majivu na ninapokula nalia kwenye kigae

Dondoo hili ni maghani ambayo yaliibua taswira uoni ya Muya katika mazingira ya kazi ya kibarua cha kuwinga ndege. Maghani hii iliafiki mhimili wa nadharia ya utafiti unaoshikilia kuwa kuna njia mbalimbali za usimuliaji wa matukio. Kutokana na dondoo hili, ni bayana kuwa wafanyakazi wa kibarua walidharauliwa. Hii ndiyo sababu Muya alilazwa kwenye majivu na kulia kigaeni. Matumizi ya sadfa iliyompa nafasi Cinji kumtesa Muya pasipo kujua ilitumika kusuta udhalimu wa aina hii kwa wafanyakazi wa kibarua.

### 4.4 Mwonoulimwengu wa Kisiasa wa Wandia

Magesa (1998) amehusisha suala la siasa na kuwepo kwa viongozi kama vile wafalme, machifu na mamlaka mengine yanayovuka mipaka ya kifamilia. Magesa (mtaje) ameonyesha kuwa sheria, utangamano wa kijamii na usuluhishi wa migogoro ndivyo vipengele muhimu katika mfumo wa kisiasa wa jamii. Naye Muriuki (1974) ametambua kiwango cha uongozi wa mbari chini ya kiongozi wa jina tu (*Muramati*) na uongozi wa kiwango cha baraza la wazee ( *kiama*) lililojukumika kuunda sheria, uendeshaji wa serikali na kuamua kesi. Kenyatta ( 1938) ametambua nafasi ya baraza la wazee katika kuendesha shughuli za kisiasa. Ili kutimiza matilaba ya utafiti huu, mwonoulimwengu wa kisiasa wa jamii ya Wandia ulikitwa kwenye masuala ya usuluhishaji wa migogoro, uongozi, na haki. Masuala haya yalihakikiwa kutokana na N4, Thigiti na kanyonyo na N5, Mkutano wa Wanyama wa porini.

#### 4.4.1 Usuluhishi wa Migogoro

Ngano ni chombo muhimu kinachotumiwa kusuluhisha migogoro katika jamii. Katika muktadha huu, ngano hutoa msingi wa usuluhishi wa migogoro katika mfumo wa kijamii kwa kuwa matendo ya majagina hutumiwa kama kigezo cha kuhukumu

matendo ya sasa (Ogbalu, 2018). Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, migogoro ilijitokeza katika N4 na N5.

N4, ilidhihirisha kuwa kulikuwa na ubia wa migogoro baina ya Thigiti na Kanyonyo. Mgogoro huu ulitishia kuangamiza mshikamano wa kijamii uliokuwepo. Data ya utafiti ilibainisha kuwa kiini cha mgogoro huu ni wivu uliotokana na ukweli kwamba ndama wa Kanyonyo walikuwa wazuri na walivutia. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> …Thigiti wakaishi pamoja na Kanyonyo. Kila mmoja alikuwa na ng`ombe wake. Ng`ombe hao walipoanza kuzaa, ng`ombe wa Kanyonyo akazaa, naye wa Thigiti akazaa pia. Mtu aliyekuwa na shida nyingi sana ni Thigiti kwa sababu aliona Kanyonyo alikuwa ametunza ng`ombe wake ilhali wake hawakuwa wamenona. Alipoona kuwa ng`ombe wa Kanyonyo amezaa ndama anayevutia, akabadilishana ndama hao.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia uliosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, kuishi pamoja kwa Thigiti na Kanyonyo, wivu wa Thigiti na wizi wa  ndama wa Kanyonyo. Taswira uoni ilitumika kutuchorea jozi ya ng`ombe wa Kanyonyo walionona kwa upande mmoja na wale wa Thigiti waliokondeana kwa upande mwingine. Taswira mwono ndiyo iliibua taswira hisi ambayo ilimchochea Thigiti kubadilisha ndama wa Kanyonyo. Dondoo hili lilithibitisha kuwa wizi wa ndama wa Kanyonyo na Thigiti ndio kiini cha mgogoro wa kijamii baina yake na Kanyonyo. Mgogoro huu ni kiwakilishi cha kuwepo kwa migogoro katika jamii ya Wandia. Muktadha wa wizi wa ndama ulithibitisha kuwa Thigiti ndiye wakala wa simulizi ambaye alibadilisha mkondo wa usimulizi na mshikamano wa jamii kwa jumla. Uwakala huu ulitoa msisitizo kwa jamii kuwa wivu unaweza kusababisha kusambaratika kwa mshikamano wa mfumo wa kijamii. Mgogoro huu haukuwa na budi kutatuliwa ili kuhakikisha kuwa Kanyonyo alipata haki na kudumisha mshikamano wa kijamii. Hapa nafasi ya mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia katika ngano teule ilijitokeza wazi. Mchakato wa usuluhishi wa mgogoro huu ulihusisha kusikizwa kwa kesi ili hukumu itolewe kwa mujibu wa sheria. kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> “..Tutaenda kwa baraza la wazee… kule uwanjani kulikuwa kumechimbwa shimo. Ndani ya shimo hilo mliwekwa kijana na wazee wa baraza. Baraza la wazee huku juu linaamua kesi pamoja na kijana aliyemo shimoni… Wazee wale wakasema, ``tutafanya hivi ili tujue ni

> nani aliyeiba ndama. Wewe ndiwe utakayeondoa jabali``… Alijaribu kuvuta, akavuta, alipovuta akachoka, akasema, ``sasa ninachoka namna hii na ni ndama wa Kanyonyo niliyeiba. Naye mtu aliye shimoni anasikiliza na kuandika taarifa yake…Aai! Sitavuta tena sababu ninachoka bure. Mimi ndiye mwizi wa ndama wa mwenyewe… Kanyonyo naye akaambiwa na wazee, ``ingia hapo`` Kanyonyo akasukuma, akasukuma, akasukuma, akasema; `` sasa ninachoka hivi kwa sababu ndama wangu aliibiwa na Thigiti. Sitavuta tena. ``

Dondoo hili lilizingatia mfuatano wa matukio kiusababishi kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya naratolojia. Aidha, usimulizi wa matukio katika dondoo hili ulitumia njia ya nathari ambayo ni mojawapo ya njia za usimulizi wa hadithi kwa mujibu wa nadharia ya naratolojia. Taswira uoni ilitumika kuchora picha ya shimo lililochimbwa, kijana aliyekuwa shimoni, jabali pamoja na wazee waliokuwa juu ya jabali. Taswira hii ilidhihirisha nafasi ya baraza la wazee katika jamii ya Wandia. Dondoo hili pia liliibua taswira mwendo ambayo ilitokana na usukumaji wa jabali. Hadhira iliona taswira ya watu ambao walijaribu kuvuta jabali lakini jitihada zao hazikufua dafu na taswira hii ndiyo ilichochea ungamo kutoka kwa kila mhusika. Taswira uoni, taswira mwendo na taswira hisi ni baadhi ya taswira ambazo zilifanikisha usawiri wa mwonoulimwengu wa kisiasa wa wandia katika N4. Usuluhishi wa migogoro ulihusisha utafutaji wa ushahidi. Mchakato wa kusukuma jabali ulidhamiriwa kutoa nafasi kwa mshukiwa ya kuungama makosa yake pasipo kujua kuwa maungamo yalikuwa yakinakiliwa na mtu aliyekuwa shimoni. Data ya utafiti ilithibitisha kwamba Thigiti ndiye mwizi. Hivyo basi mchakato wa hukumu ulifuatia ili kuhakikisha kuwa maamuzi ya kesi yalikitwa kwenye haki na ukweli. Kifungu kifuatacho kinadhibitisha madai haya;

> …alikuja akawaambia, `` Je mnajua mimi ndiye nilikuwa hakimu katika kesi hii?... wewe Thigiti ulisemaje? Maandishi yako ndiyo haya; eti unachoka hivyo na ni ndama wa Kanyonyo uliiba ili uboreshe ng`ombe wako wawe wanene. Nawe Kanyonyo unachoka hivyo na ni wewe uliibiwa ndama wako kwa sababu umemtunza vizuri. Sasa ninyi amueni kesi hii. Barua yenyewe ndiyo hii.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, udhihirisho wa kijana, ubainisho wa maungamo na baraza la wazee kukabidhiwa barua. Taswira uoni iliwezesha hadhira kuona picha ya kijana akikabidhi baraza la wazee barua yenye maandishi kuhusu maungamo ya Thigiti na Kanyonyo. Taswira hii ilitumika kufanikisha maamuzi ya kesi. Katika dondoo hili, ushahidi ulitolewa na kuthibitisha kuwa Thigiti aliiba ndama wa Kanyonyo. Kuwepo

kwa ushahidi ndio msingi wa hukumu zilizokitwa kwenye haki na ukweli. Kilele cha upembuzi wa mgogoro huu ni hukumu iliyotolewa na baraza la wazee. Katika muktadha huu hukumu ilitolewa kama ifuatavyo;

> …Wazee wakasoma barua na ikathibitika kwamba Thigiti ndiye mwizi. Wakati huo, watu walikuwa wakiwekwa kwa mzinga au kufungiwa matawi… ukifungiwa matawi makavu ya mgomba na yakawashwa moto. Wewe utawashwa moto. Ng`ombe wameachiwa Kanyonyo. Thigiti akachomwa kwa kuwa ndiye alikuwa mwizi na mwizi siku hizo za zamani hakupendeka.

Usimulizi wa hukumu ya Thigiti, ulizingatia mhimili wa nadharia ya utafiti kwa kuzingatia mfuatano wa matukio kiusababishi. Dondoo hili liliibua taswira uoni ambapo hadhira ilimwona Thigiti akiwa amefungiwa matawi makavu ya mgomba na alipowashwa moto, taswira hisi iliibuka. Hapa hisia za hofu zilitekeleza dhima ya kuonya jamii dhidi ya wizi. Dondoo hili lilibainisha kuwa Thigiti alihukumiwa kifo kwa kuchomwa. Naye Kanyonyo akafidiwa kwa kurejeshewa ndama wake pamoja na ng`ombe wa Thigiti.

N5, ilibainisha kuwa chanzo cha mgogoro huu ni sungura kususia shughuli muhimu ya uchimbaji wa kisima na kutumia ulaghai kutumia maji hayo. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Sungura akajua kwa kuwa hakwenda kuchimba kisima, `` nitatumia ujanja wangu. Hebu mimi niende nikanywe maji kwa sababu sikushiriki uchimbaji wa kisima. ``Akavaa matawi ya mgomba… Akaenda hivyo, unajua akienda ni kama matawi ya mgomba yanayotembea? Ni kana kwamba anajigaragaza akaenda akachota maji. Wanyama wakaambiana, ``Njooni muone, ala! Aiah! Njooni muone matawi yanakunywa maji huku yakichota. Akarudi nyumbani siku hiyo.

Mhimili wa kinaratolojia unaozingatia mfuatano wa matukio kiusababishi ulijipenyeza katika dondoo hili. Kwa mfano, sungura alivaa matawi, akachota maji na kurudi nyumbani. Taswira uoni katika dondoo hili ilitumika kusawiri ujanja wa sungura. Hapa hadhira iliweza kuona picha ya matawi yakichota maji. Data ya utafiti katika kifungu hiki ilithibitisha kuwa siku ya kwanza sungura hakukamatwa. Sababu ni kuwa mjio wake akiwa matawi ulionekana kama mazingaombwe na ukazua taharuki. Muktadha huu ulithibitisha kuwa sungura ni wakala wa simulizi ambaye vitendo vyake viliathiri mshikamano wa kijamii kwa kutumia mali ya umma kwa ulaghai. Mgogoro huu

uliendelezwa siku ya pili. Siku hiyo sungura alidhani angefanikiwa kuchota maji lakini juhudi zake zikagonga mwamba. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Siku iliyofuata, akajua hangevaa majani makavu ya mgomba; `` nitajibadilisha kwa kitu kingine nisije kujulikana. Ndipo akakumbuka matawi ya mwaloni… Akajifungia ili aachiwe macho tu. Ndiyo sababu akigaragara nayo yanaenda jinsi anavyoenda… Akaenda akachota maji. Wakaambiana, `` aai! Huyu ni mtu anayejua anachofanya. Sasa watoto wakatoka, na walipoona matawi haya yakigaragara… wazee wanne walishika doria. Wakamkamata sungura.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa kinaratolojia unaozingatia mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, sungura kuvaa majani ya mwaloni, kugaragara, kuchota maji na kukamatwa. Taswira uoni iliwezesha hadhira kuona picha ya sungura akiwa amevaa majani ya mwaloni akichota maji na hata akikamatwa na wazee wanne. Kukamatwa kwa sungura kuliibua taswira hisi miongoni mwa hadhira ambayo iliashiria hali ya hatari. Hapa, sungura alikabidhiwa adhabu ya kifo. Japo aliweza kuponyoka, sungura aliishi maisha magumu pasipo kutumia maji ya kisima kwa sababu alikataa kushirikiana na wanyama wengine. Kitendo cha sungura cha kujitenga na wanyama wengine kiliafiki methali ya Kiswahili isemayo, ` *mkataa wengi mchawi*` (Kingei na Ndalu, 2013: 190) iliyomaanisha kuwa mtu anayekataa ushirikiano huenda si mwema.

N6, Ndovu na Fisi, ilibainisha kuwa kiini cha mgogoro huu ni dhuluma aliyotendewa ndovu mjamzito na fisi pamoja na jamii yake. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Fisi akikaakaa, mtoto akasema,
> “ Ihi!Ihi!Ihi!Ihi!Ihi! akaulizwa na mama yake,” unataka nini?
> “Ninataka kuuma wayo wa ndovu, mafuta yachirizike ta!
> Akaambiwa” nenda ukaume``
> Akaenda akauma ndovu.
> Mtoto mwingine akasema, “Ehe! Ehe! Ehe! Ehe!
> Akaulizwa, `` unataka nini? ``
> Ninataka kuuma wayo wa ndovu mafuta yachiririzike ta!
> Mume naye akasema
> Ehe! Ehe! Ehe! Ehe! Ehe!
> Akaulizwa na mke, `` unataka nini? ``
> Akajibu “ninataka kuuma wayo wa ndovu mafuta yachririzike ta!
> Naye mke akaiga” Ehe! Ehe! Ehe! Ehe! Ehe!
> Akaulizwa, `` unataka nini?
> Akajibu, `` ninataka kuuma wayo wa ndovu mafuta yachiririzike ta!

Dondoo hili lina mshabaha na mawazo ya Habib ( 2011) yanayosisitiza udhihirisho wa tabia ya mhusika kupitia ploti. Kwa kuongozwa na maoni ya Habib ( mtaje) imebainika kuwa fisi na familia yake wameathiriwa na ulafi ambao ndicho chanzo cha mgogoro. Katika dondoo hili, taswira uoni kuhusu kunona kwa uwayo wa ndovu inasababisha taswira hisi ambayo inaathiri watoto wa fisi, fisi na mkewe hadi wakaanza kuiga vilio. Uigaji huu unajenga taswira sikivu ambayo inashurutisha kuomba idhini ya kuuma uwayo wa ndovu. Uumaji wa uwayo wa ndovu unazua taswira mwonjo ambayo inachochea kuliwa kwa ndovu mjamzito na fisi. Hapa taswira hisi kuhusu dhuluma hii inachochea hisia ya kupania kuona haki imetendewa ndovu mjamzito aliyeliwa na fisi. Dondoo hili limethibitisha kuwa chanzo cha mgogoro huu ni ulafi wa fisi na aila yake. Muktadha huu umebainisha kuwa fisi wamevunja mkataba wa udugu na maridhiano kwa kumla ndovu mjamzito badala ya kumtunza kulingana na makubaliano kati ya fisi na ndovu.

Usuluhishi wa mgogoro huu unaanza pindi tu ndovu wanapoarifiwa kuhusu tanzia ya kuliwa kwa ndovu mjamzito. Taarifa hii iliwasilishwa kisanii na watoto wa ndovu kupitia mtindo wa wimbo kama ifuatavyo;

> Ndovu hawa mlienda kukaa
> Mlienda kukaa na msirudi
> Mkamwacha mama nyikani mwa fisi
> Mtoto wa fisi akilia
> Niume uwayo wa ndovu
> Ikifika jioni ni ii! ii! Uwayo, uwayo wa ndovu
> Kukicha asubuhi ni Ii! Ii!
> Uwayo, uwayo wa ndovu

Katika dondoo hili, mhimili wa nadharia ya utafiti unaoshikilia kuwa kuna njia mbalimbali za kusimulia matukio umejipenyeza kwa kutumia wimbo. Wimbo huu unazingatia mantiki ya mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, kukawia kwa ndovu, watoto wa fisi kulia, na kuuma uwayo wa ndovu asubuhi na jioni. Katika dondoo hili, taswira uoni kuhusu kuumwa kwa uwayo wa ndovu inasababisha taswira hisi ambayo inaathiri watoto wa fisi, fisi na mkewe hadi wakaanza kuiga vilio. Uigaji huu unajenga taswira sikivu ambayo inashurutisha kuomba idhini ya kuuma uwayo wa ndovu. Uumaji wa uwayo wa ndovu ulizua taswira mwonjo ambayo ilichochea kuliwa kwa ndovu mjamzito na fisi. Hapa taswira hisi kuhusiana na dhuluma hii ilichochea hisia za kupania kuona haki ilitendewa ndovu. Katika wimbo huu watoto wa ndovu waliwasuta ndovu kwa

kukawia mno na kuwapa fisi nafasi ya kuwatendea mama yao dhuluma. Wimbo huu ulitoa taswira ambayo ilichochea hisia za ndovu kuanza mchakato wa kutafuta haki ya ndovu aliyeliwa. Katika muktadha huu wana wa ndovu wamejitokeza kama wakala wa simulizi kwa kuwatanabahishia ndovu wengine tanzia ya kuliwa kwa mama yao na fisi. Huu ukawa mwanzo wa mgogoro na aidha mwanzo wa upembuzi wa mgogoro huu.

Hatua ya kwanza ya usuluhishi wa mgogoro huu ni kumtanabahishia mshukiwa makosa yake. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa mshukiwa ameadhibiwa kutokana na makosa ambayo yamethibitishwa kisheria. Suala hili lina mshabaha na kishazi cha kikatiba kinachosema kuwa `` mshukiwa hana hatia mpaka ithibitike kuwa amefanya kosa (Katiba mpya ya Kenya ya 2010, sehemu ya 50 ibara ya 2a). Watoto wa ndovu walitekeleza jukumu la wakala wa simulizi kwa kuponyoka na kwenda kuwaarifu ndovu wengine kuhusu tanzia ya kuliwa kwa mama yao. Habari hii ndiyo ilijenga msuko wa ngano hii kwa kuanzisha mchakato wa usuluhishi wa mgogoro huu.

Mgogoro huu uliwasilishwa mbele ya korti ya maoni ya umma. Muktadha wa korti ya umma hushurutisha malalamishi kuwasilishwa mbele ya hadhara na baada ya ushahidi kutolewa kesi kuamuliwa papo hapo. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Mkutano ukapangwa,``Ndovu mwenzetu tulipomwacha kwenu mlifanya nini?``
> ``Tulimla`` Ni watoto walimla. Sisi hatukujua alivyofanya kwa sababu ni watoto waliomla tulipowaacha hapo. Hatukujua walivyofanya. Haya wakaambiwa, sasa tunataka ndovu wetu.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya utafiti unaoshikilia kuwa kuna njia mbalimbali za kusimulia matukio. Mashtaka dhidi ya dhuluma za fisi kwa ndovu yalisimuliwa kinathari. Katika dondoo hili, fisi walipewa nafasi ya kujitetea ili ukweli uthibitike.

Kilele cha usuluhishi wa migogoro ni uamuzi wa kesi. Muktadha wa uwasilishaji wa N6 ulizua kinaya kilichobainisha kuwa ndovu ndiye mlalamishi, mwendesha mashtaka na mwamuzi wa kesi. Japo fisi walikosa kwa kumla ndovu mja mzito, utaratibu wa kutafuta haki ungeshurutisha kuwepo kwa mpatanishi ama hakimu asiyeegemea upande wowote. Hii ndiyo sababu ndovu waliamua kutumia mbinu ya vita baina yao na fisi ili kufidia ndovu mwenzao. Hali hii ilithibitika katika kifungu kifuatacho;

> Haya! Wakaambiwa, `` sasa tunataka ndovu mwenzetu`` Wakasema, `` sasa tutawapiga kwa nini? Sasa ni vita na tutapigana mpaka mtupatie ndovu mwenzetu. Vita vikaanza. Ni kupigana. Fisi wakapiga ndovu kwa mijeledi. Naye kinara wa ndovu akasema, Aa! Achana na hawa! Wacha niwaangushie kimoja tu… Wakang`oa mti mzima. Wakawazingira mahali wasitoroke. Walipoangushiwa walikufa wote.

Katika dondoo hili usimulizi wa vita baina ya ndovu na fisi ulizingatia matakwa ya mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, ndovu kudai fidia, fisi kupiga ndovu kwa mijeledi na mauaji ya fisi kwa kuangushiwa mti. Dondoo hili liliibua taswira uoni ambayo ilisawiri vita baina ya ndovu na fisi. Taswira hii iliibua taswira mwendo ambayo ilijumlisha miondoko ya ndovu na fisi katika harakati za vita. Hukumu ya kifo kwa jamii nzima ya fisi ilizua taharuki. Hadhira ilibaki na swali kuhusu iwapo uamuzi huu ulikuwa wa haki. Hukumu hii ya kifo ilitokana na maamuzi ya korti ya maoni ya umma. Adhabu ya kifo kwa fisi iliashiria kuwa katika jamii ya Wandia makosa ya jinai yalishurutisha mtuhumiwa kuhukumiwa kifo. Hapa suala la mkabala la mtazamo linajitokeza na kubainisha mtazamo wa Fanani Wanjira wa Rukenya pamoja na Wandia kuhusu makosa ya jinai kwamba mhalifu alistahiki kifo.

Maudhui ya usuluhishi wa mgogoro katika N4, N5 na N6 yana mshabaha na maoni ya Habib (2011) anapodokeza kuwa mhusika na kitendo ni kipengele muhimu katika ngano na kusisitiza kuwa tabia ya mhusika sharti ionyeshwe katika ploti. Hivyo basi tabia ya Thigiti katika N4 na Sungura katika N5 zilitumika kuendeleza ploti katika ngano hizo na kufafanua usawiri wa mwonoulimwengu wa kisiasa kwa kuongozwa na kipengele cha usuluhishaji wa migogoro.

### 4.4.2 Uongozi

Uongozi ni madaraka anayopewa mtu ya kusimamia shughuli au asasi. Madaraka haya yanamwezesha kiongozi kutoa maamuzi kwa niaba ya jamii. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti huu. Mfano, katika N5 na N6, suala la uongozi lilijitokeza. Katika N4, baraza la wazee lilijukumika kuongoza jamii katika shughuli mahususi kama vile kusikiza na kuamua kesi. Majukumu ya baraza la wazee katika N4, yana mshabaha na maoni ya Muriuki (1974) . Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> … akabadilisha ndama hao. Alipobadilisha Kanyonyo akamwambia Thigiti, wewe unakosea kwa sababu ulibadilisha ndama. Ulichukua ndama wangu. Tutaenda kwa baraza la wazee.

Dondoo hili lilibainisha kuwa Kanyonyo alikuwa na imani na baraza la wazee. Aidha Kanyonyo alitambua kuwa baraza la wazee lilitwikwa mamlaka ya juu sana na lilijihusisha na majukumu ya kuunda sheria, uendeshaji wa serikali na kuamua kesi (Muriuki, 1974). Hii ndiyo sababu badala ya Kanyonyo kuchukua sheria mkononi, aliamua kwenda kumshtaki Thigiti kwa baraza la wazee kwa kutambua dhima yake katika jamii. Suala la uongozi wa baraza la wazee lilijitokeza katika N4 kama suala muhimu linaloelekeza fasiri ya mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia.

N5 ilidhihirisha kuwa suala la uongozi ni kipengele mahususi cha fasiri ya mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia. Mathalan, N5, ilichora taswira ya kiongozi mwenye maono kuhusu watawaliwa. Uongozi wa aina hii ulitahadharisha umma kuhusu hatari inayowakabili. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Mnyama yeyote mwenye pembe inabidi akatwe pembe. Kwa sababu kichaka hiki tunakoishi kitawashwa moto na pindi kikichomeka hatutapata mahali pa kutorokea. Mashimo yote yaliyomo humu ndimo tutakamoingia kichaka kikichomeka.

Dondoo hili lilibainisha kuwa paa ndiye wakala wa simulizi kwa kutumia tahadhari kuathiri ulimwengu wa hadithi na kuendeleza ploti. Kutokana na ushauri wa paa, hatari ya pembe kuwazuia wanyama kuingia mashimoni ndilo suala ambalo lilishawishi wanyama kukubali kukatwa pembe. Hapa mtazamo wa msimulizi ni kwamba watawaliwa hawana budi kufuata maagizo ya kiongozi wao.

Kushirikisha umma kwenye miradi ya maendeleo ndio msingi wa usawiri wa mwonoulimwengu wa kisiasa katika N5. Sababu ni kuwa mojawapo wa lengo la siasa ni kuhakikishia jamii maendeleo. Uongozi wowote ule wenye maono ya maendeleo hauna budi kushirikisha umma kwenye maono ya kiongozi na utekelezaji wa maono hayo. Hii ina maana kuwa kiongozi na wafuasi wake wanapaswa kuwa na mwono sawa wa mambo. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, msimulizi anaelezea:

> Wakakaa mashimoni, sasa waliendelea kukaa mashimoni. Si moto ulizimika?
> ``sasa tuliambiana, tukitoka tutachimba kisima ili tusikose maji ya kunywa. Tutatoka humu tukiwa na kiu, mito itakuwa ilikauka.

Kutokana na dondoo hili ni dhahiri kuwa mwono wa mambo wa kiongozi ulimwezesha kushirikisha umma katika miradi ya maendeleo. Dhana hii ilielezewa kinaratolojia na kuibua ubainisho wa uongozi kwa kuwa paa ni wakala wa simulizi aliyetumika kukuza ploti kwa mwono wake wa mambo. Mtazamo wa Wandia kuhusu uongozi ulibainika na kuonyesha kuwa uongozi bora hauna budi kushirikisha umma katika miradi ya maendeleo. Hiki ni kipengele muhimu cha fasiri ya mwonoulimwengu wa Wandia.

N6, Ndovu na Fisi, ilibainisha kuwa jamii ya ndovu iliongozwa na ndovu mmoja ambaye alitwikwa mamlaka ya kutoa mwelekeo kwa ndovu wengine. Uongozi wa kinara wa ndovu ulidhihirika katika muktadha ambapo ndovu mjamzito alilemewa na safari. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> …Walipoenda, yule aliyekuwa mjamzito akashindwa kuendelea na safari. Wakienda hivyo akasema ameshindwa kutembea. Wakateremka. Kiongozi wao akasema, ``sasa kwa sababu tuko kwa Fisi, tutamwombea mahali pa kulala ili tumchukue tukirudi. Akaombewa mahali pa kulala kwa Fisi.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa kinaratolojia unaoshikilia kuwa matukio hupangwa kwa mfuatano wa kiusababishi (Propp, 1928). Mfano ndovu mjamzito kushindwa kutembea kuombewa mahali pa kulala kwa fisi na ndovu wengine kuendelea na safari. Kulingana na dondoo hili, inadhhirika kuwa sifa kuu ya kiongozi mzuri ni kutoa suluhisho la matatizo yanayoisibu jamii. Katika muktadha huu, ndovu anapolemewa na safari kiongozi anajitokeza kama wakala wa simulizi ambaye anaathiri ulimwengu wa ngano hii kwa kutoa mwelekeo kuhusu usuluhishaji wa tatizo lililokumba ndovu mjamzito. Kiongozi wa ndovu amejitokeza kuwa mhusika mwenye upevu wa kimawazo na ndiposa anawaelekeza ndovu wengine kukubali kumwombea ndovu mwenzao mahali pa kulala.

Uongozi unahusishwa na uwezo wa kiongozi kutimiza maslahi ya umma anaoongoza. Hii ina maana kuwa maslahi ya umma yanapewa kipaumbele na kiongozi mzuri huwa katika mstari wa mbele kupigania maslahi ya umma. Hali hii ilidhihirika katika N6. Mfano, inapobainika kuwa fisi walimla ndovu mjamzito, kinara wa ndovu alianza mikakati ya kudai kulipwa fidia ya ndovu aliyeliwa na fisi. Hii inadhihirika katika kifungu kifuatacho:

> Sasa wakarudi nyumbani. Wakapitia kwa fisi: wakaambiwa``mje mkutanoni``…Naye akaja mkutanoni. Kinara wa ndovu ndiye ameitana mkutano. Mkutano ukapangwa.`` Ndovu wetu tulipomwacha kwenu mlimfanya nini?...Wakaambiwa,``Sasa tunataka ndovu wetu.``, Wakasema,``sasa tutawapiga kwa nini?``Wakaambiwa,`` sasa ni vita tutapigana mpaka mtupatie ndovu mwenzetu``.Vita vikaanza …Fisi wakapiga ndovu kwa mijeledi. Naye ndovu akasema,``Aa! Achaneni na hawa. Wacha niwaangushie kimoja tu…waliporushiwa walikufa wote.

Kutokana na dondoo hili, ni dhahiri kuwa kiongozi anapaswa kuwa katika mstari wa mbele kutetea maslahi ya umma. Mfano, kinara wa ndovu katika N6 aliongoza ndovu wengine kukabiliana na fisi. Vita vinapochacha kinara wa ndovu aling`oa mti mmoja na kuwaangushia fisi wote ambao walikufa papo hapo. Kupitia uongozi wa kinara wa ndovu waliweza kumlipizia kisasi ndovu mwenzao aliyeliwa na fisi. Maudhui ya uongozi katika N6, ni mwafaka katika usawiri wa mwonoulimwengu wa kisiasa katika ngano za Wandia.

### 4.4.3 Haki

Dhana ya haki imekitwa kwenye falsafa ya maadili na siasa. Kiini cha haki ni udhihirisho wa ukweli kwa lengo la kuleta mabadiliko katika jamii. Matravers (2014) ameainisha haki katika vitengo vitatu; Kutendeana sawa sawa, manufaa kwa pande zote mbili na uadilifu. Haki ni kipengele cha kimsingi cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kisiasa wa jamii chenye lengo la kihakikisha usawa wa jamii. Hali hii iljitokeza katika data ya utafiti. Mfano, katika N4, Thigiti na Kanyonyo, suala la haki lilijitokeza dhahiri. Utafutaji wa haki ulizunguka kadhia ya wizi wa ndama wa Kanyonyo na Thigiti. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> Wazee wale wakasema,`` tutafanya hivi ili tujue ni nani aliyeiba ndama. ``Wewe ndiwe utakayeondoa jabali. Kina Thigiti wakaambiwa, `` twende sasa tukashuhudie mkiliondoa jabali. Naye mtu yuko ndani. Sasa, Thigiti ndiye alikuwa na shida sana kwa kuwa alitamani ndama wa Kanyonyo. Akaambiwa,`` sasa wewe ndiwe utakayeanza kwa sababu mtu yule ambaye anashukiwa ndiye huwa na shida.” Alijaribu kuvuta, akavuta. Alipovuta akachoka, akasema, ``sasa ninachoka jinsi hii na ni ndama wa Kanyonyo niliyeiba? Mtu aliye shimoni anasikia na kuandika taarifa yake.

Dondoo hili lina mshabaha na kazi ya Muriuki (1974) na Kenyatta (1938), hususan katika ubainisho wa nafasi ya baraza la wazee katika utafutaji wa haki katika jamii. Taswira sikivu ilitumika na baraza la wazee kuamua mahali pa kusikizwa kwa

maungamo ya kila mhusika baada ya kuliondoa jabali. Taswira mwendo ilihusiana na majaribio ya kuliondoa jabali, suala ambalo liliibua taswira hisi ya mhusika ambaye alichoka na kushindwa kuliondoa jabali. Thigiti aliungama kuwa ndiye aliiba ndama wa Kanyonyo. Ungamo hili lilimfanya Thigiti kuhukumiwa kifo kwa kufungiwa matawi makavu ya mgomba na kuchomwa.

Mchakato wa utafutaji wa haki ulishurutisha aliyekosewa kutoa ushahidi wake. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, dondoo lifuatalo linathibitisha haya.

> Kanyonyo naye akaambiwa na wazee,`` ingia hapo``. Kanyonyo akasukuma, akasukuma, akasukuma, akasema,`` sasa ninachoka hivi kwa sababu ndama wangu aliibiwa na Thigiti. Sitavuta tena. Aliye ndani ya shimo anaendelea kunakili yote``

Taswira sikivu ilitumika kumwelekeza Kanyonyo kuvuta jabali. Mbinu ya Takriri yaani urudiaji wa neno,`` akasukuma`` mara tatu iliibua taswira hisi ya mtu aliyechoka kupita kiasi. Taswira mwendo ilipaswa kusababisha mwondoko wa jabali na iliposhindikana Kanyonyo akaungama kuwa alichoka hivyo kwa sababu ndama wake aliibiwa na Thigiti. Kauli ya Kanyonyo iliibua hisia ya suala ambalo liliashiria ombi la kupewa haki yake.

Kilele cha utafutaji wa haki kilifikiwa mshukiwa alipoadhibiwa na aliyekosewa kufidiwa. Data ya utafiti ilithibitisha haya katika dondoo lifuatalo;

> Yule kijana alikuja… alikuja akawaambia ,`` je mnajua mimi ndiye nilikuwa mwamuzi katika kesi hii?...wewe Thigiti ulisemaje? Maandishi yako ndiyo haya, ..`` eti unachoka hivyo na ni ndama wa Kanyonyo uliiba ili uboreshe wako wawe wanene. Nawe Kanyonyo umechoka hivyo na wewe uliibiwa ndama wako kwa sababu umemtunza vizuri. Sasa ninyi amueni kesi hii. Barua yenyewe ndiyo hii. Wazee wakasoma barua na ikathibitika kwamba Thigiti ndiye mwizi. Wakati huo watu walikuwa wakiwekwa kwa mzinga au kufungiwa matawi…unawashwa moto…sasa ng`ombe wameachiwa Kanyonyo. Thigiti akachomwa…

Dondoo hili linaafiki mawazo ya Propp (1928) kwa kuelezea mchakato wa utafutaji wa ushahidi kinathari kwa njia ya mfuatano wa kiusababishi. Taswira sikivu ilitumika kudhihirisha mwamuzi wa kesi hii huku taswira uoni ikidhihirisha maandishi yaliyobeba ushahidi kuhusu wizi wa ndama. Baada ya barua kusomwa, taswira mwendo ilitekeleza wajibu wa kuonyesha harakati za kumfungia Thigiti matawi makavu ya

mgomba na kuchomwa. Haki ilipatikana pindi Kanyonyo aliporejeshewa ndama wake pamoja na ng`ombe wa Thigiti.

Mchakato mzima wa utafutaji wa haki ulimfanya kijana aliyekuwa shimoni kuwa wakala wa simulizi ambaye alibadilisha na kurahisisha mkondo wa utafutaji wa haki kwa Kanyonyo. Muktadha wa uwasilishaji ulidhihirisha mtazamo wa fanani Wanjira wa Rukenya na jamii ya Wandia kuhusu haki. Kanyonyo alipopata haki kwa kurejeshewa ng'ombe wake, mazingira ya uwasilishaji yalibadilika na kuwa ya furaha kwa kuwa haki ilipatikana.

N5, Mkutano wa Wanyama wa Porini, ilishughulikia suala la haki kama kipengele cha mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia kwa kulihusisha na utapeli wa sungura. Data ya utafiti inathibitisha haya katika dondoo lifuatalo;

> Wakakaa, walipotokezea wakaenda wakachimba kisima. Wakaambiana,`` na yeyote yule hatachimba kisima hatakunywa maji hayo… Sungura akajua kwa kuwa hakwenda kuchimba kisima,``nitatumia ujanja wangu. Hebu mimi niende nikanywe maji sababu sikushiriki uchimbaji wa kisima.``

Dondoo hili lilibainisha kuwa kulikuwa na makubaliano kati ya wanyama kuwa wanyama walioshiriki kuchimba kisima ndio waliokuwa na haki ya kunywa maji ya kisima hicho. Maafikiano hayo yalitekelezwa kupitia taswira sikivu. Hata sungura alisikia hayo lakini akaamua kutoshiriki uchimbaji wa kisima. Kwa kufanya hivyo sungura alikiuka haki ya matumizi ya maji ya kisima. Mhimili wa kinaratolojia ulioshikilia kuwa mpangilio wa matukio huzingatia mfuatano wa kiusababishi unadhihirika katika kadhia hii. Aidha suala la wakala wa simulizi ulibainika. Hapa, sungura alitumika kama wakala wa simulizi kwa kuendeleza msuko wa ngano hii kwa vitendo vyake.

Kilele cha ukiukaji wa haki kilishuhudiwa pale ambapo sungura alitumia ujanja kuchota maji ya kisima kinyume cha sheria. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> Akavaa matawi makavu ya mgomba… Matawi makavu ya mgomba yakining`nia. Hayo ndiyo alijifungia ili akienda asijulikane kwanza unajua kuwa ni mfupi. Akaenda hivyo, unajua akienda ni kama matawi yanayotembea.… Ni kama kwamba anajigaragaza, akaenda akachota maji. Wanyama wakaambiana ,`` njooni muone . Ala! Aiah! Njooni muone, majani makavu ya mgomba yanakunywa maji huku yakichota.

> Siku iliyofuata…. Ndipo akakumbuka majani ya mwaloni. Akajifunga ili aachiwe macho tu.

Utapeli wa sungura ulielezewa kinathari kwa kuzingatia mpangilio wa kimfuatano wa matukio kiusababishi Propp (1928). Mpangilio huu ulibua taswira uoni iliyohusu sungura kujibadilisha sura kwa matawi makavu ya mgomba na majani ya mwaloni. Aidha taswira mwendo ilihusisha kitendo cha sungura kujigaragaza na kuchota maji, suala ambalo liliibua taswira hisi iliyowafanya wanyama kushuku iwapo ni matawi makavu ya mgomba ama majani ya mwaloni yaliyochota maji au ni mwizi wa maji ya kisima. Suala hili lilizua taharuki miongoni mwa wanyama na suluhisho likawa wanyama kushika doria kwa zamu.

Muktadha wa utapeli wa sungura na wizi wa maji kisimani uliwanyima wanyama waliomiliki kisima haki ya kutumia maji ya kisima peke yao. Utapeli wa sungura ni ukiukaji wa haki ya wanyama. Suluhisho sharti lingepatikana. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Wazee wanne walishika doria na wakamkamata sungura. Sungura alipokamatwa alipelekwa pale ambapo alipaswa kuchomewa… Alipokamatwa alidanganya ili asipelekwe chunguni. Mke alipoenda kumshika akaponyoka na kutoroka.

Dondoo hili liliafiki mhimili unaotambua kuwa kuna njia mbalimbali za kusimulia matukio . Mfano, jitihada za kulinda haki ya matumizi ya maji ya kisima zilielezewa kwa njia ya nathari kwa kuzingatia mfuatano wa matukio kiusababishi. Kukamatwa kwa sungura, kukabidhiwa wanawake ili achomwe chunguni na hatimaye kutoroka kuliibua taswira mwendo. Muktadha wa uwasilishaji uliibua taswira hisi ambapo hata hadhira ilimhurumia sungura kwa kuwa angeteseka kutokana na ukosefu wa maji. Hata hivyo wanyama walipata haki yao kutokana na kukomeshwa kwa sungura kutumia maji ya kisima. Kutokana na misingi kuwa kiini cha haki ni udhihirisho wa kuleta mabadiliko katika jamii ni bayana kuwa udhihirisho wa haki ulitumika katika N4 na N5 kama msingi wa kuleta na kudumisha haki katika jamii.

### 4.6 Hitimisho

Uchunguzi ulibaini kuwa ngano teule zilidhihirisha mwonoulimwengu wa Wandia. Uainisho wa mwonoulimwengu wa Wandia ulikitwa kwenye makundi matatu

yafuatayo kama vile mwonoulimwengu wa kijamii, mwonoulimwengu wa kiuchumi na mwonoulimwengu wa kisiasa. Usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii ulihusisha masuala kama vile mivutano ya kijinsia, uchumba, ndoa, maadili, haki ya kijamii na tabaka. Mwonoulimwengu wa kiuchumi ulihakikiwa kwa masuala kama vile kilimo, ufugaji, biashara na kibarua. Usawiri wa mwonoulimwengu wa kisiasa ulihakikiwa kwa masuala kama vile usuluhishi wa migogoro, uongozi na haki.

# SURA YA TANO

# JINSI SAUTI YA SIMULIZI NA MTAZAMO ZINAVYOCHANGIA MWONOULIMWENGU WA KIJAMII, KIUCHUMI NA KISIASA KATIKA NGANO ZA WANDIA

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inajadili usimulizi na utazamaji wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule za Wandia. Sauti ya simulizi inarejelea wakala anayetumiwa kuwasilisha mwonoulimwengu mahususi katika ngano teule. Umakini upo katika utambuzi wa msimulizi na mwonoulimwengu mahususi anaoshughulikia (Abbott, 2002). Kwa upande mwingine mtazamo unahusu utambuzi wa chombo ambacho kinaelekeza usimulizi wa mwonoulimwengu katika ngano teule. Hivyo basi, sura hii inaangazia jinsi sauti ya simulizi na mtazamo zilitumika kuwasilisha suala la mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule.

Sauti ya simulizi na mtazamo ndizo nyenzo za kimsingi ambazo zinatumiwa na mtunzi kuwasilisha hadithi katika matini ya kisimulizi (Wafula, 2013). Bal (1997) ameelezea kuwa sauti ya simulizi na mtazamo ni nyenzo ambazo zinatumiwa na mtunzi kuchezea na kuelekeza usomi wa hadithi iliyosimuliwa katika ngano fulani. Kwa mujibu wa Currie (2010), sauti ya simulizi na mtazamo zinapaswa kuwezesha mawasiliano katika matini ya ngano. Sauti ya simulizi na mtazamo ni istilahi ambazo zina uhusiano wa karibu hivi kwamba kuna haja ya kutambua wakala anayeongea (sauti ya simulizi) na yule anayeona hadithi (mtazamaji) ili kuondoa utata katika kuelezea jinsi kitu fulani kinavyoonekana na jinsi mwonekano huo unavyosimuliwa (Bal, 1997). Ili kuondoa utata kati ya chombo ambacho kilisimulia hadithi na kile ambacho kinaelekeza usimuliaji wake, Genette (1980) aliibua dhana ya mtazamo. Ilibainika kuwa sauti ya simulizi na mtazamo ni nyenzo zinazotumiwa kuongoza usimuliaji wa hadithi inayosimuliwa katika matini yoyote ya simulizi. Kwa sababu hii sauti ya simulizi na mtazamo ni vigezo muhimu katika uhakiki wa mwonoulimwengu wa Wandia kama unavyojitokeza katika ngano teule.

## 5.2 Jinsi Sauti ya Simulizi na Mtazamo Zinavyochangia Usawiri wa Mwonoulimwengu wa Kijamii wa Wandia

Vipengele vya sauti ya simulizi na mtazamo vilitumika kusawiri mwonoulimwengu wa Wandia kupitia kwa vigezo vya maudhui ya mivutano ya kijinsia, uchumba, ndoa, malezi, maadili, haki ya kijamii na tabaka. Mivutano ya kijinsia ilijadiliwa katika sehemu ifuatayo;

### 5.2.1 Mivutano ya Kijinsia

N1 ilibainisha kuwa sauti ya simulizi na mtazamo zilitumiwa kuwasilisha dhana ya mivutano ya kijinsia. Taswira uoni kuhusu mgomo wa wasichana ilitumiwa kuongoza uhakiki wa mivutano ya kijinsia. Barobaro walilitazama suala la mivutano ya kijinsia na kubainisha mshtuko na mtamauko wao kuhusu mgomo wa wasichana. Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> Hapo zamani za kale, paliishi wasichana waliogoma kuongea wala kuolewa na wanaume. Wakasema kuwa yeyote watakayeongea naye ndiye atakayewaoa…Wasichana wamekataa kuolewa.

Dondoo hili lilidhihirisha kuwa mgomo wa wasichana ni kinyume cha mwonoulimwengu wa kijamii kuhusu uchumba na sababu kuu ya mvutano wa kijinsia. Haingewezekana msichana kuolewa na mwanamume kutokana na misingi ya kuongea naye tu. Hata hivyo barobaro waliheshimu uamuzi wao. Sauti ya barobaro ilielekezwa kwa Kabindura ambaye aliibua mbinu ya kusitisha mgomo. Barobaro walipoongea mara ya kwanza walidhihirisha utamaushi ilhali walipoongea mara ya pili walidhihirisha ushindi dhidi ya wasichana. Mabezo yao yalidhihirisha kuwa mgomo wa wasichana ulikuwa umekitwa kwenye misingi ya ujinga na kutojua. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza wingi inauliza

> Wakamwambia msichana ``ulikawia hivyo muda huo wote ukingojea Kabindura ilhali ana matege na hapendezi yeyote densini?

Furaha ya barobaro hawa ilionyesha kuwa ndoa kati ya msichana na Kabindura ilifidia makosa waliyofanyiwa na wasichana na huo ukawa mwisho wa mgomo. Usimulizi wa mtazamo wa Wandia kuhusu mivutano ya kijinsia ulizingatia misingi ya mawazo ya Propp(1928) yanayosisitiza mpangilio wa matukio kwa mfuatano maalum wa kiusababishi ambao ulijenga msuko wa hadithi. Katika muktadha wa kiuchanganuzi,

mgomo wa wasichana ulisababisha mtamauko wa barobaro ambao pia ulichochea kuzua mikakati ya kusitishwa kwa mgomo.

N1, iliangazia kaida zinazoongoza utongozaji na uchumba, suala ambalo lilidhihirisha kuwa ukiukaji wa kaida hizi ni msingi wa mivutano ya kijinsia. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

Msichana huyu- I-rere
umesalimiwa na Kabindura
Upawa na kitanda
Panda kwa kitanda
Na kitanda kimetandikwa
Na nyumba imeezekwa
Imeezekwa ndari -I-rere
Msichana huyu- I-rere

Dondoo hili lina mshabaha na mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza kuwa kuna njia mbalimbali za usimulizi wa ngano (Wamitila, 2002). Dondoo hili lilitumia wimbo kuwasilisha ujumbe. Muktadha wa uwasilishaji wa dondoo hili ulijenga taswira uoni iliyoiwezesha hadhira kuona mawazoni upawa, kitanda ambacho kilikuwa kimetandikwa na nyumba iliyoezekwa. Katika dondoo hili, Kabindura, ambaye ndiye sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza alidhihirisha kuwa anafahamu kaida zinazoongoza shughuli ya utongozaji na uchumba. Kwanza alijenga uhusiano kwa kumjulia hali na kumsalimia kisha akamsadikisha kuhusu vipengele vya msingi wa ndoa kama vile; chakula (upawa), kitanda na nyumba. Mambo haya matatu yalithibitisha utayari wa barobaro kuoa. Katika muktadha huu mwitikio wa msichana ulisababisha mvutano wa kijinsia kutokana na ukimya wa msichana na kumshurutisha Kabindura kung`oa mtama ili msichana aongee. Mtazamo wa Kabindura ni kwamba kila barobaro alipaswa kuoa pasipo kuzingatia misingi ya iwapo ana ulemavu au kasoro yoyote ile. Mtazamo huu ulisimuliwa kupitia kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza. Sauti hii ilitilia mkazo mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia unaosisitiza ulazima wa barobaro kuoa.

Mtazamo wa msichana ulidhihirisha nia yake ya kujikomboa kutokana na kudhibitiwa na utamaduni ambao ulimkweza mwanamume na kumdhalilisha mwanamke. Msichana aling`ang`ania nafasi yake japo alishindwa na hatimaye kuongea na kuolewa na Kabindura. Sauti hii ni changamoto kwa jamii iliyokwama kwenye utamaduni potovu ikumbatie mabadiliko kuhusu mahusiano ya kijinsia. Kitendo cha msichana kuolewa na Kabindura kilibatilisha mtazamo wa wasichana wenzake waliogoma na kupanga

mkutano mwingine wa kusitisha mgomo. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya:

Kuhusu mgomo wa wasichana,

> Wakaitana tena, "Njooni tusitishe mgomo." Kwa sababu …wasichana wale wote wazuri wanaolewa na *`mang`ong`oi`*.

Dondoo hili linaafiki mhimili wa nadharia ya utafiti unaodokeza kuwa mpangilio wa matukio huzingatia mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, mkutano wa wasichana, kauli ya kusitisha mgomo na wasichana wazuri kuolewa na watu wasiovutia. Wasichana walibatilisha uamuzi na kuwa wakala wa simulizi na sauti ya simulizi katika ufafanuzi wa mabadiliko haya. Mtazamo wa msichana ulijumuisha mtazamo wa wasichana katika mahusiano ya kijinsia na kuibua sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ambayo ilitumika kusimulia mwonoulimwengu wao. Kusitishwa kwa mgomo kulipokonya kiapo nguvu zake na kuzirejesha kwa utamaduni ambao uliwapendelea wanaume. Mradi barobaro walipokezwa uwezo wao upya, wasichana hawakuwa na uwezo wa kujiamulia masuala ya kijinsia lakini sauti yao ilisikika.

Mtazamo wa msimulizi ulidhihirika na kuafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza kwamba msimulizi hadhamirii kuwasimulia wasikilizaji wake tu bali huwa na mtazamo wake kuhusu masuala anayowashirikisha. Kwa kuwa msimulizi ni kiwakilishi cha jamii ya Wandia, mtazamo wake unasadikika. Msimulizi alituchorea taswira uoni ya mgomo wa wasichana pasipo kutoa msimamo wake lakini mwishoni wasichana walipositisha mgomo, mtazamo wake ulidhihirika. Msimulizi aliwasuta wasichana kwa kuzingatia masharti ya kiapo kisichojengwa kwenye mantiki yoyote na kuishia kwenye maangamizi. Sauti ya nafsi ya tatu ilitumika kusimulia mtazamo huu ambao ndio mwonoulimwengu wa jamii. Hivyo basi msimulizi alipendekeza wanaume wasimame katika nafasi yao na wadhihirishe uhodari katika mahusiano yao na wanawake.

N3 ilidhihirisha kuwa sauti ya simulizi na mtazamo zilichangia pakubwa mwonoulimwengu wa kijamii kwa misingi ya mivutano ya kijinsia. Msimulizi alichora taswira ya jinsi mtoto wa kiume amedekezwa huku mtoto wa kike akidhibitiwa na utamaduni uo huo. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Ndugu yake akirejea kutoka densini, akamwambia, `` Muya unajua kuna wanaume watatu wanaokuja hapa kunikuta unapoondoka?

> Wacha kuwa ukikawia sana ukienda uwe unarudi…Sababu hutanikuta nami sitakubali kuuawa kwa kukataa kuwafuata. Lazima niandamane nao.

Dondoo hili lilibainisha kuwa usimulizi wa nguvu za utamaduni ulizingatia mhimili wa nadharia ya utafiti unaosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi (Propp, 1928). Mfano, Muya kutahadharishwa kuhusu wanaume wanaomvizia Cinji na uwezekano wa kutwaliwa kwa nguvu ama kuuawa. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza iliyodhihirika kupitia kwa mhusika Cinji ilisimulia jinsi nguvu za kitamaduni zilivyotumiwa kumdhalilisha msichana. Udhihirisho wa nguvu za kitamaduni ulisimuliwa kwa mtazamo wa ndani kupitia kwa Cinji, ambaye alikuwa amedhibitiwa na utamaduni. Mfano, sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza iliorodhesha majukumu ya dada kwa ndugu yake kama vile; kupika, kufua na kumtunza kwa jumla. Utamaduni ulihalalisha majukumu haya. Msimulizi alitazama kitendo cha kuviziwa kwa Cinji na barobaro watatu. Mtazamo huu una mshabaha na mhimili wa nadharia ya utafiti unaoonyesha kuwa msimulizi huwa ana mtazamo wake kuhusu mambo anayosimulia hadhira. Hapa, taswira iliyochorwa na msimulizi ni ya msichana asiyekuwa na uwezo wowote kwa kuwa alidhibitiwa na utamaduni potovu. Mivutano ya kijinsia ilidhihirika katika kadhia ya barobaro kumtwaa Cinji pasipo hiari yake. Hapa, sauti ya simulizi ilitumika kusimulia nguvu za kitamaduni katika mchakato wa mahusiano ya kijinsia. Sauti hii ya simulizi ndiyo msingi wa fasiri ya mwonoulimwengu wao wa kijamii.

Cinji alitazama mivutano ya kijinsia na kuonyesha kuwa ameridhia udhibiti wa utamaduni ambao ulimdhalilisha. Mtazamo wake ni kuwa msichana akikataa kutwaliwa kwa nguvu, angeweza kuuawa. Alimwambia ndugu yake Muya kuwa yeye hangekubali kuuawa kwa kukataa kuwafuata. Cinji, ambaye aliwakilisha wasichana, alionyesha kuwa wasichana walinyimwa uwezo wa kushiriki katika maamuzi ya nani angewaoa bali walitwaliwa kwa nguvu. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya ndani na ilidhihirisha kuwa utamaduni ulipewa uwezo wa kuongoza na kutawala mawanda ya mapenzi na uchumba.

### 5.2.2 Uchumba

Sauti ya simulizi na mtazamo zilitumika kusimulia suala la uchumba katika ngano teule. N1 ilidhihirisha mtazamo wa Kabindura kuhusu uchumba. Mtazamo wake ni kwamba

kila mwanamume alipaswa kujitetea na kuchumbia msichana licha ya kuwa na kasoro za kimaumbile. Huu ndio mtazamo wa jamii ya Wandia. Sauti ya Kabindura iliposikika, ilisisitiza kutimizwa kwa vipengele vya kimsingi vinavyodhihirisha utayari wa barobaro kuoa. Dondoo hili linathibitisha madai haya;

> Msichana huyu- *I-rere*
> umesalimiwa na Kabindura
> Upawa na kitanda
> Panda kwa kitanda
> Na kitanda kimetandikwa
> Na nyumba imeezekwa
> Imeezekwa ndari -*I-rere*
> Msichana huyu- *I-rere.*

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia unaoshikilia kuwa kuna njia mbalimbali za usimuliaji wa ngano. Katika muktadha huu, utazamaji na usimulizi wa uchumba katika usawiri wa mtazamo wa kijamii wa Wandia ulitumia mbinu ya wimbo. Katika dondoo hili sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza iliibua taswira uoni ambayo ilidhihirisha uwepo wa nyumba, upawa na kitanda. Taswira hii ilitumiwa kusimulia utayari wa Kabindura kuoa kwa kutoa uhakikisho wa kuwepo kwa nyumba, chakula na malazi.

Suala la uchumba liliangaziwa na kutazamwa na mtazamaji wa ndani. Hapa Kabindura ndiye kiakisi cha mtazamo na ajenti wa simulizi. Utamaduni umeweka utaratibu ambao unaongoza mchakato wa uchumba (Waita,2003; Kenyatta, 1938). Utaratibu huu uliwapa barobaro nafasi ya kutongoza kwanza na sio kinyume. Kutenda kinyume cha utaratibu huu kulisababisha adhabu. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti katika kifungu kifuatacho;

> Mimi nilipata wangu. Njooni muone. Niliwaambia nitapata mkabishana nami. Njooni sasa. Barobaro wakakubali kwenda kumwona msichana…Wakamwambia msichana, ``ulikawia hivyo muda huo wote ukimngojea Kabindura ilhali ana matege na hata hapendezi yeyote densini.

Dondoo hili lilizingatia mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza mpangilio wa mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, Kabindura alipata mke, akawaalika barobaro waje washuhudie, kubezwa kwa wasichana na udhihirisho wa kuwa Kabindura ana matege. Kabindura, ambaye aliwakilisha sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza alisisitiza mtazamo wa jamii kuwa kila barobaro alipaswa kuoa pasipo

kuzingatia misingi ya iwapo ana kasoro za kimaumbile au la. Aidha, sauti ya simulizi ya ndani iliyowakilishwa na barobaro ilidhihirisha dhihaka kwa msichana aliyeshiriki mgomo wa wasichana na hatima yake ikawa kuolewa na Kabindura. Mtazamo wa Wandia kuhusu suala hili ulisimuliwa na kubainishwa kwa kutumia sauti ya simulizi ya ndani.

Sauti ya simulizi kutoka nje ilibainisha kuwa barobaro wana wajibu wa kujitetea na kutongoza msichana na mambo yalipowawia magumu, wangeweza kutumia mbinu yoyote mradi msichana akubali kutongozwa. Mathalan, kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> Msichana akamwambia Kabindura, `` wacha kung`oa mtama wetu. Njoo uniambie unachotaka kwa kuwa sasa unakosea.

Dondoo hili liliibua taswira uoni ambayo ilichora picha ya Kabindura aking`oa mtama hadi msichana akamrai asiendelee kung`oa. Kabindura alijitokeza kama sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na mwenye mtazamo wa ndani kuhusu umuhimu wa barobaro kuanzisha mchakato wa uchumba. Hii ndiyo sababu Kabindura aling`oa mtama ili kumshurutisha msichana akubali kuongea ili mwishowe amuoe.

Densi za usiku zilisawiriwa kuwa mazingira mwafaka ya kutongozana na kuchumbiana katika N3. Ngano hii ina mshabaha na kazi ya Waita (2021), ambapo ameeleza kuwa densi za usiku zilikuwa mazingira mwafaka ya kutongozana na kuchumbiana. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti katika kifungu kifuatacho;

> Mvulana alikuwa ameenda densini msichana akabaki nyumbani…Mvulana alikuwa akienda kuimba nyimbo zilizokuwa zikiimbwa zamani na wavulana na wasichana. Msichana hakuwa akishiriki nyimbo ili asiache nyumba hivyo. …Ndugu yake akirejea kutoka densini akamwambia, ``Muya unajua kuna wanaume watatu wanaokuja hapa kunikuta unapoondoka? Wacha kuwa ukikawia sana. Ukienda uwe unarudi.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa kinaratolojia kwa kufuata mpangilio wa matukio kwa mfuatano wa kiusababishi. Mfano, mvulana kwenda densini, msichana kubaki nyumbani na msichana kumtahadharisha Muya. Usimulizi na utazamaji wa uchumba uliibua taswira mwendo. Taswira hii ilidhihirisha jinsi wavulana kwa wasichana walishiriki densi. Taswira uoni iliunda picha ya kimawazo ya Wavulana pamoja na

wasichana densini. Dondoo hili lilibainisha kuwa kivutio kikuu kwa Muya kilikuwa wasichana. Densi na nyimbo za usiku zilimzuzua Muya mpaka akasahau wajibu wake wa kumlinda dada yake Cinji. Hapa kupitia kwa macho ya msimulizi, tunaonyeshwa uwezo wa densi za usiku kwa barobaro na mwono huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu.

Ngano hii pia ilionyesha kuwa kulikuwa na baadhi ya wasichana ambao hawakupewa nafasi ya kuchumbiwa kutokana na nguvu za kitamaduni. Wasichana kama hawa walinyimwa nafasi ya kudhihirisha uwezo wao wa kudhibiti hisia na kujichagulia wachumba. Sauti za simulizi ya nafsi ya kwanza na ya tatu zilitumika kusimulia suala hili. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ilitumika kuonyesha jinsi msichana hakuwa na hiari ya kujichagulia mchumba. Angetwaliwa kwa nguvu na akikataa kutwaliwa angeuawa. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya:

> Sababu hutanikuta. Nami sitakubali kuuawa kwa  kukataa kuwafuata.
> lazima niandamane nao.

Dondoo hili lilibainisha kuwa msichana hakupewa nafasi ya kujuana na kuchumbiana na mume mtarajiwa kutokana na shinikizo la mila na utamaduni.  Hapa, msichana amesawiriwa kama wakala wa simulizi kwa kutofanya chochote ili kujikwamua kutokana na dhuluma ya aina hii.

### 5.2.3 Ndoa

Sauti ya simulizi na mtazamo zilitumiwa kama vipengele vya usawiri wa mwonoulimwemgu wa kijamii wa Wandia kwa kuongozwa na kigezo cha ndoa. Mfano, katika N1, barobaro waliduwaa kwa kuwa walishindwa kuoa wasichana kutokana na athari za mgomo wa wasichana. Barobaro walionyesha kutoridhika kwao na sauti yao ilisikika katika mabishano yao na Kabindura. Sauti ya barobaro ilidhihirika walipomwahidi Kabindura ndama, fahali na mbuzi watano. Sauti ya simulizi kutoka nje, ilionyesha msisitizo wa sauti ya barobaro kuhusu ahadi yao kwa Kabindura. Uzito wa suala la ndoa ulijitokeza katika muktadha wa kuwekeana dau kati ya Kabindura na barobaro watatu kama ilivyojitokeza katika dondoo lifuatalo.

> Kabindura akasema, ``sasa kwa sababu wamekasirishwa na barobaro, mimi nitaoa wasichana hao wanaogoma. ``Na nikiwaoa mtanipatia nini? Kabindura akaambiwa, ``nitakupatia ndama``. Mwenzake akajitolea, ``

> Nitakupatia mbuzi watano. Na kwa sababu walikuwa watatu, ``nitakupatia fahali`

Kabindura alijitokeza kama wakala wa simulizi ambaye alitenda kinyume cha matarajio ya barobaro ambao walitamauka kutokana na mgomo wa wasichana wa kutoongea na wanaume. Barobaro nao walidhihirika kuwa wakala wa simulizi kwa kumwahidi Kabindura ng`ombe na mbuzi iwapo angefaulu kumwoa msichana aliyegoma. Mtazamo wa barobaro hawa ulidhihirika kutokana na kujitolea kwao kumshawishi Kabindura kumwoa msichana mrembo ili watumie nafasi hiyo kuchochea kusitishwa kwa mgomo.

Kwa mujibu wa barobaro, wanaume wenye nguvu, afya na haiba ndio walikuwa na nafasi nzuri ya kuoa wanawake warembo. Data ya utafiti ilithibitisha mtazamo huu kupitia swali la balagha katika dondoo lifuatalo;

> "Sasa unajua nitaoa mmoja wa wasichana wale waliogoma? Nawe utaoaje? Una matege. Hata huvutii yeyote densini, hata wasichana hawaongei na wewe".

Dondoo hili liliafiki mhimili wa mpangilio wa mfuatano wa matukio kiusababishi.. Mfano, azma ya Kabindura kumwoa msichana ilifuatwa na kudhihakiwa na barobaro. Dondoo hili liliibua taswira uoni iliyotazamisha hadhira na hali halisi ya Kabindura ya kuwa na matege na kutovutia wasichana. Kauli ya barobaro hawa ilidhihirisha mwonoulimwengu potovu ambao ulisimuliwa kupitia kwa sauti ya simulizi ya ndani. Ndoa iliyojengwa kwenye misingi ya haiba na uwezo wa kucheza densi ni dhana potovu. Kabindura alilitazama suala la ndoa na mtazamo wake ulipinga mtazamo wa barobaro kuhusiana na dhana ya ndoa. Mtazamo wa Kabindura kuhusu ndoa ni mtazamo wa ndani na ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya kutoka ndani. Hatimaye Kabindura alifanikiwa kumwoa msichana baada ya kung`oa mtama hadi ikambidi msichana kuongea naye na hatimaye kuolewa na Kabindura.

Muktadha huu ulithibitisha kuwa kiapo cha wasichana kilikuwa na nguvu ambazo ziliwawezesha kudumisha ukimya. Kiapo hiki hakikukitwa kwenye mantiki yoyote na kiliwaingiza katika maangamizi. Ilibainika kuwa kiapo cha Kudumisha ukimya kilikuwa na nguvu na ndicho kilichowezesha wasichana kuendelea kuwatesa barobaro. Hata hivyo, Kabindura alipoanza kung`oa mtama, msichana aliongea. Msichana

alipodumisha ukimya, alihodhi nguvu nyingi ambazo ziliogofya barobaro. Hata hivyo alipoongea na kumrai Kabindura amwoe, Kabindura alimpokonya nguvu zile na kuchukua nafasi ya kuwa mwokozi wa barobaro ambao walikuwa wamekata tamaa. Muktadha huu ulimfanya Kabindura wakala wa simulizi ambaye alirejeshea barobaro nguvu na uwezo wa kuoa tena. Mathalan, barobaro walipomtembelea Kabindura na Kuthibitisha kuwa amemwoa msichana mrembo, walimbeza mno. Mabezo haya yalichochea wasichana wengine kusitisha mgomo. Huu ni urejesho wa nguvu kwa barobaro. Ilibainika kuwa huu ndio mtazamo wa jamii ya Wandia kuhusu ndoa.

Msimulizi alitazama dhana ya *`mang`ong`oi`* na kubainisha kuwa kila mwanamume alitarajiwa na jamii kuoa. Mtazamo huu ulisimuliwa kupitia kwa sauti ya simulizi ya kutoka nje iliyoonyesha kuwa *`mang`ong`oi`* walitafutiwa wasichana na kuletewa nyumbani. Sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu inaelezea kuwa;

> Hata wale ambao hawakuwa sawa walipelekewa msichana. Msichana angekamatwa na wanaume watano na akiingia huko hangetoka anakuwa mke wa huko.

Usimulizi na utazamaji wa suala la ndoa katika dondoo hili ulizingatia mhimili wa mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, barobaro kuletewa wasichana, msichana kutwaliwa kwa nguvu na kupelekewa barobaro. Dondoo hili liliibua taswira uoni. Hadhira iliweza kuona mawazoni msichana akibebwa hobelahobela mabegani mwa barobaro. Taswira hii ilionyesha kudhibitiwa kwa wasichana na utamaduni ambao uliwakandamiza. Mtazamo wa jamii ya Wandia kuhusu ndoa ulithibitisha kuwa ndoa ni suala nyeti ambalo wakati mwingine lilihusisha jamii nzima. Jamii ilijitwika jukumu la kumtafuta msichana, kumtwaa na kumpelekea *`mang`oing`oi`* pasipo hiari yake. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya:

> Ndio, sasa ingebidi apelekewe, atetewe ama aletewe. Sababu watu walikuwa wakiletewa msichana, na mwanamume akakubali. Waliletewa msichana hadi nyumbani. Angekamatwa na barobaro watano.Msichana kama huyu mzuri, anakamatwa na barobaro watano. Hadi kwa barobaro huyu na kuambiwa, “Mfungie sasa.” Nawe ukiingia humo. Humo hutatoka. Na ukipelekwa nyakati hizo zetu hungetoka huko. Umekuwa mwanamke wa huko.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa mfuatano wa matukio kiusababishi (Propp, 1928). Mfano, msichana kutongozwa kwa niaba ya barobaro, kutwaliwa, kupelekewa barobaro, kufungiwa kwa barobaro na kuwa mke wa barobaro. Taswira mwendo

ilijumlisha msichana kukamatwa na barobaro na kupelekwa kwa mume pasipo hiari yake. Muktadha huu uliibua taswira uoni ambayo ilionyesha picha ya msichana akitwaliwa. Utwaaji wa msichana kwa lazima na kumpelekea mwanamume ni idhibati kwamba kulikwa na ulazima wa kila barobaro kuoa. Sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu ilitumika kusimulia mwonoulimwengu wa jamii kuhusu suala nyeti la kulazimisha wasichana kuolewa. Sauti hii inasadikika kwa kuwa ni sauti ya msimulizi ambaye ni kiwakilishi cha tajriba ya utamaduni wa Wandia kuhusu suala la ndoa.

Mtazamo wa jamii ya Wandia kuhusu ndoa ulibainisha kuwa ndoa ni suala linalohusisha jamii nzima kwa jumla. Mtazamo huu ulishurutisha ukoo kumchangia mwanamume maskini mbuzi mmoja mmoja na kumlipia mahari. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> … Hata akiwa na ulemavu wa aina yoyote, sharti angeoa. Hata watu walikuwa. wakilipiwa mahari na ukoo nyakati hizo. Iwapo mtu hakuwa na kitu. Iwapo ni *`mang`ong`oi`* watu wangechangia kila mtu mbuzi mmoja mmoja.

Dondoo hili linaafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia uliobainisha kuwa msimulizi huwa na mtazamo wake kuhusu mambo anayoishirikisha hadhira. Dondoo hili lilibainisha mtazamo wa msimulizi. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Sauti hii ilibainika kuwa sauti ya wakala wa utamaduni wa Wandia. Hivyo basi sauti hii ilisababisha kusadikika kwa mtazamo wa kijamii wa Wandia kuhusu ndoa na kuthibitisha fasiri ya mwonoulimwengu wa Wandia wa kijamii kwa kuongozwa na kipengele cha ndoa.

Sauti ya simulizi na mtazamo zilitumiwa kusawiri ndoa za lazima katika N3. Msingi wa ndoa za lazima ulikitwa kwenye utamaduni wa jamii (Kenyatta, 1938; Waita, 2003). Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Haya! Huku Muya akaambiwa, ``utanitafuta wewe! Na njia nitakayopitia nitakuelekeza. Nitabeba vitu vyote; nibebe mtama, fiwi, njegere, maharagwe na wimbi. Nitabeba chochote kitakachopatikana ili ile njia utakayopitia ukinitafuta uione ikiwa imeota mimea hiyo. Sababu hutanikuta nami sitakubali kuuawa kwa kukataa kuwafuata. Lazima niandamane nao.

Dondoo hili lilithibitisha kuwa suala la ndoa za lazima lilitazamwa kwa macho ya Cinji ambaye ndiye kiakisi cha mtazamo wa ndani. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na kubainisha kuwa Cinji hakuwa na pingamizi yoyoye kuhusu kutwaliwa kwake. Cinji alijitokeza kama wakala wa simulizi kwa kutochukua hatua yoyote ya kupambana dhidi ya udhalimu huu. Mtazamo huu uliafiki mtazamo kuhusu ndoa katika N1 unaoshikilia kuwa wasichana wangetwaliwa kwa nguvu na kupelekewa wanaume ambao hawakuwa na uwezo wa kujitetea wala kutongoza wasichana.

Sauti ya simulizi na mtazamo katika N1 na N3 ni nyenzo madhubuti ambazo zilitumiwa kutazama na kusimulia suala la ndoa kama kipengele cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia.  Ndoa ilijitokeza kama taasisi muhimu na msingi wa usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia.

### 5.2.4 Maadili

Suala la maadili kama kipengele cha usawiri wa mwonoulimwengu wa wandia lilitazamwa na kusimuliwa katika N1, N2 na N5. N1 ilibainisha kuwa ukweli na uaminifu ndio msingi wa maadili wa Wandia. Data ya utafiti ilibainisha kuwa maadili yalishurutisha mtu kutimiza ahadi. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Mimi nitaoa wasichana hao wanaogoma. Na nikiwaoa mtanimpatia nini?
> Kabindura akaambiwa “nitakupatia ng’ombe” mwenzake akajitolea “nitakupatia mbuzi watano” … Hapo ndipo kabindura aliahidiwa ng’ombe, ndama, fahali na mbuzi watano na wale barobaro.

Suala la uaminifu kama kibainishi cha maadili ya wandia lilitazamwa na msimulizi kwa macho ya Kabindura. Hapa Kabindura ndiye wakala wa simulizi ambaye mtazamo wake ulibainisha kuwa kuwekeana dau ni uthibitisho wa uaminifu na aliyeahidi hakuwa na budi kutimiza. Suala la uaminifu liliendelezwa katika dhana ya mgomo wa wasichana dhidi ya kuongea na wanaume. Msingi wa kiapo cha mgomo huu ulikuwa msichana akiongea na barobaro angeolewa naye papo hapo. Suala hili lilitazamwa kwa mtazamo wa ndani kwa macho ya msichana na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika kifungu kifuatacho;

> Akapakuliwa chakula, akaambiwa, “sasa kwa sababu tulisema mtu tutakayeenda naye ni yule tutakuwa tumeongea naye. Sasa kwa sababu nimeongea nawe. Twende sasa ukanioe”.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya utafiti kwa kuzingatia mpangilio wa mfuatano wa matukio kiusababishi. Dondoo hili liliibua taswira mwonjo iliyohusishwa na upakuaji wa chakula. Taswira hii ilionyesha kukubalika kwa Kabindura. Uaminifu kwa kiapo cha mgomo wa wasichana ulitazamwa kwa miwani ya msichana na kubainisha kuwa maadili yaliyohusiana na kiapo yalishurutisha mtu kutimiza masharti ya kiapo kwa vyoyote vile. Hii ndiyo sababu msichana alimrai Kabindura amuoe kwa kuwa aliongea naye. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ilitumika kusimulia mtazamo huu. Hapa msukumo wa masharti ya kiapo ulimfanya msichana wakala wa simulizi aliyeathiri ulimwengu wa ngano hii na kuendeleza msuko wake.

Msimulizi alitazama suala la maadili kwa kulihusisha na uzingativu wa miiko ya Wandia katika N2. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya: -

> Ukila *uura* huo wa nguchiro, hakuna jambo jema utakalopata. La! Ndiyo sababu alikuwa akipangusa na kulitupa kwa sababu *uura* haupaswi kuliwa na binadamu. Ulikuwa ukiliwa na watu walafi.

Dondoo hili liliibua taswira uoni iliyohusisha msichana kupangusa `*uura*` ulipomwangukia midomoni. `*Uura*` ulitumika kiistiari kuashiria chanzo cha mikosi. Miiko ya jamii ya Wandia ilitazamwa kwa mtazamo wa nje na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Mtazamo wa msimulizi na Wandia kwa jumla ni kuwa miiko haina budi kuzingatiwa. Hii ndiyo sababu msimulizi alihusisha ulaji wa *uura* na chanzo cha mikosi katika maisha.

Utazamaji na usimulizi wa maadili kama kipengele cha usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia katika N5 ulihusishwa na mshikamano wa kijamii. Muktadha huu ulithibitisha kuwa wanajamii walishirikiana takriban katika mambo yote. Ushirika huu ndio msingi wa maadili ya jamii. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> Sungura, akajua ya kuwa hakwenda kuchimba kisima, “nitatumia ujanja wangu…” wazee wanne walishika doria. Wakamkamata sungura. Sungura alipokamatwa alipelekwa pale ambapo alipaswa kuchomewa.

Taswira uoni ilitumika kuchora picha ya washika doria wakimkamata sungura. Dondoo hili lina mshabaha na mawazo ya Hogan (2013) yanayoonyesha kwamba naratolojia inahusu hadithi na diskosi. Hadithi katika muktadha huu ni ukiukaji wa maadili uliotekelezwa na sungura ilhali diskosi ni usimulizi wa ukiukaji huu kinathari. Suala la ukiukaji wa maadili lilitazamwa kwa mtazamo wa ndani na nje na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na ya tatu. Mtazamo wa Wandia ni kwamba kila mwanajamii anapaswa kuchangia miradi yoyote ya maendeleo na akisusia, anyimwe haki ya kufaidika kutokana na mradi huo.

N6, Ndovu na Fisi, ilibainisha kuwa maadili ya jamii yamekitwa kwenye uhusiano wa kidugu kati ya familia ya ndovu na fisi. Uhusiano huu umekita mzizi hivi kwamba ndovu walikuwa radhi kumwacha ndovu mjamzito nyikani mwa fisi wakitarajia angetunzwa lakini matokeo yake yakawa tanzia. N6, ilithibitisha kuwa ukiushi wa kanuni za maadili ya kijamii unaweza kusababisha maafa katika jamii. Mfano, dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Watoto wa ndovu walitoroka. Wale waliokuwa tumboni. Wakaponyoka. Wakatoroka wakamwacha mama yao akiliwa… walipomwacha akiliwa, watoto wakatoroka wakaenda kuita ndovu wengine.

Dondoo hili linaafiki mhimili wa kinaratolojia unaoshikilia kuwa usimuliaji wa matukio hupangwa kwa mfuatano wa kiusababishi. Mfano, kuponyoka na kutoroka kwa watoto wa ndovu, kumwacha mama akiliwa na fisi na kuwafahamisha ndovu wengine. Maelezo haya yaliibua taswira mwendo hivi kwamba hadhira iliweza kuona mawazoni watoto wa ndovu wakikimbia. Katika dondoo hili watoto wa ndovu ndio wakala wa simulizi ambao kutoroka kwao kuliathiri ulimwengu wa ngano hii. Uwakala wa watoto wa ndovu ulidhihirika katika mchakato wa kuwajulisha ndovu wengine kuhusu tanzia ya mama yao kuliwa na fisi.

Maadili yanahusishwa na uwajibikaji, suala ambalo linashurutisha wanajamii kuwajibikia matendo yao. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Ndovu hawa mlienda kukaa
> Mkamwacha mama nyikani mwa fisi
> Mtoto wa fisi akilia
> Niume uwayo wa ndovu

Kila kukicha asubuhi ni;
Ii, Ii! Uwayo, uwayo wa ndovu
Ikifika jioni ni;
Ii! Ii! Uwayo, uwayo wa ndovu.

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya utafiti unaosisitiza kuwa kuna njia mbalimbali za kusimulia matukio. Hapa, kupotoka kimaadili kwa ndovu kulisimuliwa kwa njia ya wimbo ambao unaashiria kuwa kukawia kwaondiko kulisababisha kuliwa kwa ndovu mjamzito. Watoto wa ndovu waliwasuta ndovu wengine kwa sababu walimwacha mama yao nyikani mwa fisi huku wakifahamu kuwa fisi ni walafi. Taswira sikivu ilitumika kufahamisha ndovu wengine kuhusu tanzia ya kuliwa kwa ndovu mjamzito na kuwachochea kulipiza kisasi. Wimbo huu ulitoa taswira ya jinsi fisi na aila yake walikaidi maadili ya kijamii na kusambaratisha mshikamano wa jamii. Katika wimbo huu ulafi wa fisi unawapelekea kuuma uwayo wa ndovu hadi wakamla akakwisha.

N6, ilithibitisha kuwa, maadili yanayotawala mahusiano ya kijamii yametazamwa na kusimuliwa kwa sauti ya nafsi ya kwanza na ya tatu. Mtazamo wa msimulizi ni kuwa ukiushi wa maadili ya kijamii yanaweza kusababisha maafa. Mfano, data ya utafiti, imethibitisha haya katika wimbo ufuatao.

Ndovu hawa mlienda kukaa,
Mkamwacha mama nyikani mwa fisi
Mtoto wa fisi akilia
Niume uwayo wa ndovu
Ii! ii ! uwayo, uwayo wa ndovu
Ikifika jioni ni;
Ii! Ii! Uwayo, uwayo wa ndovu.

Katika dondoo hili, mhimili wa nadharia ya utafiti unaosisitiza kuwa kuna njia mbalimbali za usimuliaji wa matukio ulijipenyeza. Katika muktadha huu usimulizi na utazamaji wa ukiushi wa maadili umetumia njia ya wimbo. Katika wimbo huu, maadili yanayotawala mahusiano ya kijamii yalitazamwa na kubainishwa kuwa yamekiukwa na fisi na familia yake kwa kumla ndovu mjamzito. Katika wimbo huu watoto wawili wa ndovu waliokuwa tumboni na kufanikiwa kutoroka ndio wakala wa simulizi ambao walitoa taarifa kuhusu mauaji ya mama yao, suala ambalo ni kinyume cha maadili ya jamii. Taarifa hii ilitumika kama msingi wa mwanzo wa kutafuta haki ya ndovu aliyeuliwa. Mtazamo wa wandia ni kwamba mauaji hayafai kutekelezwa na yeyote na

iwapo yametekelezwa, wauaji hawana budi kuadhibiwa. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza.

### 5.2.5 Haki ya Kijamii

Suala la haki ya kijamii kama kigezo cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii lilitazamwa na kusimuliwa katika N1, N2 na N3. Utazamaji na usimulizi wa haki ya kijamii katika N1 ulikitwa kwenye vipengele viwili; mgomo wa wasichana na unyanyapaa dhidi ya walemavu. Kipengele cha mgomo kilitazamwa kwa mtazamo wa nje na wa ndani. Aidha, sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu na ya kwanza zilitumika kusimulia mtazamo huu. Data ya utafiti inathibitisha madai haya katika dondoo lifuatalo;

> Hapo zamani za kale paliishi wasichana waliogoma kutoongea wala kuolewa na wanaume.'Wakasema kuwa barobaro yeyote watakayeongea naye ndiye atakayewaoa. Naye Kabindura akabishana na barobaro. Alipobishana nao akawaambia,`` mimi kwa sababu mnakataa kwenda kuongea na wasichana hao na wamegoma hawataki kuolewa. Nitamwoa mmoja wa wasichana hao wamegoma."

Mgomo wa Wasichana wa kutoongea wala kuolewa na wanaume ulitazamwa kwa mtazamo wa nje na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Wasichana ndio wakala wa simulizi kwa kuathiri ulimwengu wa ngano hii. Mgomo huu ni kinaya katika muktadha wa kijamii wa Wandia ambapo suala la uchumba na ndoa lilichangamkiwa na kusisimua jamii (Kenyatta, 1938; Waita, 2003). Muktadha wa uwasilishaji uliibua taswira hisi ya dhihaka dhidi ya mgomo huu.

Utazamaji wa kadhia ya mgomo wa wasichana kwa macho ya Kabindura yaani mtazamo wa ndani uliibua taswira ya ulazima wa kila barobaro kuoa katika jamii ya Wandia pasipo kujali misingi ya kasoro za maumbile. Mawazo haya yana mshabaha na kazi ya Kenyatta (1938) na Waita (2003). Falsafa hii ya kitamaduni ilimfanya Kabindura kuapa kwamba angemwoa mmoja wa wasichana walioshiriki mgomo. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza. Taswira uoni, sikivu, na hisi ndizo taswira ambazo ziliibua hali ya utamaushi miongoni mwa barobaro. Mgomo huu uliwanyima barobaro haki ya kijamii ya kutongoza, kuwachumbia na kuwaoa wasichana.

Suala la unyanyapaa dhidi ya walemavu lilitazamwa kwa mtazamo wa ndani hasa kwa macho ya barobaro. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika kifungu kifuatacho;

> …sasa unajua nitaoa mmoja wa wasichana waliogoma.`` Nawe utaoa aje? Una matege. Hata huvutii yeyote densini, hata wasichana hawaongei na wewe``. Akaulizwa,`` sasa utaoaje? "Nitaoa msichana mmoja wa hao wanaogoma."

Suala la ulemavu lilitazamwa kwa macho ya barobaro na kudhihirisha unyanyapaa dhidi ya walemavu kama vile Kabindura. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na kuibua taswira uoni iliyowezesha hadhira kuona picha ya mtu mwenye matege. Taswira uoni iliathiri hisia na kuibua taswira hisi iliyoonyesha jinsi walemavu walitengwa na kudhihakiwa na jamii. Unyanyapaa uliwapokonya walemavu haki ya kijamii ya kutongoza, kuchumbia na kuoa. Mbinu ya takriri iliyothibitishwa na urudiaji wa neno `utaoaje` ilidhamiriwa kusisitiza unyanyapaa dhidi ya walemavu.

Dondoo hili lilibainisha mtazamo wa Kabindura kuhusu uchumba na ndoa katika jamii ya Wandia. Mtazamo huu ulishikilia kuwa kila barobaro ana haki ya kuoa na kumnyima nafasi hiyo ni sawa na kumpokonya haki yake ya kijamii. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ambapo Kabindura aliapa kumwoa msichana mmoja miongoni mwa wale waliogoma pasipo kujali hali yake ya maumbile. Unyanyapaa dhidi ya walemavu uliendelezwa na barobaro pamoja na wasichana. Barobaro walionyesha mtazamo wao kuhusu walemavu katika dondoo lifuatalo;

> Wakamwambia msichana, ulikawia hivyo muda huo wote ukimngojea Kabindura ilhali ana matege na hata hapendezi yeyote densini?

Dondoo hili lilibainisha kuwa walemavu waliowakilishwa na Kabindura walitengwa katika miktadha ya kijamii kama vile densini ambapo hangecheza na msichana yeyote. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ilidhihirisha dhihaka dhidi ya Kabindura hadi wakashangaa kwa nini msichana alikawia muda huo wote hatimaye aolewe na Kabindura. Dhihaka ya aina hii ni kuwahini walemavu haki yao ya kijamii.

Mtazamo wa jamii kuhusu walemavu ulisababisha kusitishwa kwa mgomo wa wasichana. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> Sasa akaambiwa amefanya vizuri. Kuhusu mgomo wa wasichana, wakaitana tena,`` Njooni tusitishe mgomo kwa sababu… wasichana wale wote wazuri ndio wanaolewa na mang`ong`oi…. Barobaro wasio hali wala fasili, wasiovutia, wasioweza hata kujitetea.

Kauli mbiu ya wasichana ya kusitisha mgomo iliashiria kilele cha unyanyapaa dhidi ya walemavu. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ilibainisha mtazamo wa wasichana kuwa walemavu hawapaswi kuoa wasichana wazuri. Sadfa ilisababisha wasichana wazuri kuolewa na wanaume wasiovutia na ikabidi mgomo usitishwe. Kusitishwa kwa mgomo kuliwarejeshea barobaro uwezo wao wa kutongoza, kuchumbia na kuoa wasichana. Hivyo basi barobaro walirejeshewa haki ya kijamii.

Haki ya kijamii ilitazamwa na kusimuliwa kwa kuambatanishwa na tuzo ama adhabu kutegemea tabia ya mtu binafsi katika N2. Hivyo basi haki ya kijamii ilitegemea wajibu wa mtu binafsi. kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> …Akipita hapo ndipo anaitwa,``msichana huyu, njoo unile ukinipondaponda na unaona kuwa tunajila. Akasema, sili vijilavyo``. Ndio hizo ni fiwi kwa sababu ametoka kwa njegere. Sasa amekuja kwa uji. Sasa amekuja kwa fiwi. Ametoka kwa `uura`

Dondoo hili lilibainisha kuwa ufahamu wa uzingativu wa maadili ya jamii kama msingi wa kubainisha mtu aliyestahili ama asiyestahili kupewa haki ya kijamii ulitazamwa na kusimuliwa. Ufahamu huu ulitazamwa kwa mtazamo wa nje na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Taswira mwonjo na taswira uoni zilitumika kama kishawishi cha kuvutia Wacuka kwenye majaribu lakini Wacuka alidhibiti nafsi yake na kushinda majaribu hayo.

Haki ya kijamii ilijumlisha utuzaji mtu kwa kuzingatia maadili ya jamii na kuadhibu mtu kutokana na ukiukaji wa maadili. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> Kondoo wangekatwa mkia na kisha kukatwakatwa vipande vidogo vidogo. Vipande hivyo vingekatwa vidogo vidogo na kukaangwa jikoni. Vipande hivyo vingeletwa kwa sahani… sasa ukiwa na kipande kimoja naye mwenyeji ana vipande viwili, ukiwa na viwili mwenyeji ana vitatu. Yule akiwa na vinne, nawe una vitatu. Vipande vilipokwisha wakalala. Sasa umemaliza mtihani. Wameenda kulala. Asubuhi aende afunguliwe ghala kama hili; lina mapambo, lina mikufu. Akaambiwa. Jaribu… jipambe kwa chochote unachotaka. Vitu vyote.

Utazamaji na usimulizi wa ushindi wa Wacuka ulizingatia msingi wa mawazo ya Propp (1928) unaoshikilia kuwa matukio hupangwa kwa mfuatano wa kiusababishi. Mtazamo wa nje na usimulizi wa nafsi ya tatu kuhusu udhibiti nafsi ziliibua taswira ya jinsi Wacuka alinga`ng`ana kula vipande vichache kuliko mwenyeji ili asidhihirishe ulafi. Hatimaye Wacuka alituzwa kwa mapambo ya kila namna. Muktadha wa uwasilishaji ulibainisha wazi mtazamo wa fanani Wanjira wa Rukenya kuhusu haki ya kijamii kwa Wacuka aliyeshinda majaribu yote.

Aidha, N2, ilishughulikia mtazamo na usimulizi wa adhabu kwa wanajamii waliokaidi maadili ya kijamii. Adhabu ni haki ya kijamii kwa mujibu wa jamii ya Wandia. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika dondoo lifuatalo;

> Msichana akaambiwa,`` hii ndiyo sababu ulitunukiwa maganda. Iwapo `uura` wenyewe ulipokuangukia ulikula… sasa iwapo uliuramba na ukaende ukila chakula… ndiyo nilikuwa nikila chakula na kunywa uji. ``Ndio sababu ulipewa maganda.. maganda ni msichana asiyeweza kudhibiti hisia zake. Na amefanya mapenzi na kupata mtoto.

Dondoo hili lilidhihirisha kuwa adhabu kama kipengele cha haki ya kijamii ilitazamwa kwa mtazamo wa ndani na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza. Muktadha wa uwasilishaji ulibainisha mtazamo wa msimulizi kwa kukadiria jinsi alivyochangamka hasa alipoelezea adhabu ya vazi la maganda kwa Kamwagirwa kutokana na ukiukaji wa maadili ya jamii. Sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu ilifafanua zaidi kuwa maganda ni jazanda iliyoashiria msichana ambaye alipata mtoto nje ya ndoa. Mtazamo wa fanani Wanjira wa Rukenya kuhusu adhabu unasadikika kwa kuwa yeye ni kiwakilishi cha jamii ya Wandia. Mtazamo huu ulibainisha kuwa adhabu aliyopewa Kamwagirwa ni stahiki yake. Hiyo ni haki ya kijamii.

Utazamaji na usimulizi wa suala la adhabu kama sehemu ya haki ya kijamii uliendelezwa katika N3, Muya na Dada yake Cinji. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya;

> …Siku moja, Muya alipotoka densini akakuta hakuna mtu. Akakaa, akakaa. Akaathiriwa na funza. Akaathiriwa na njaa. Akasema , ``sasa dada yangu angekuwa hapa ningekuwa nikishiba kama zamani? Ningekuwa nimetolewa funza hawa. Sasa nitatolewa na nani? Sasa nitafanya nini? Sasa nitafanya nini? Sasa nitaamka niende kumtafuta kupitia njia aliyopitia.

Adhabu ilitazamwa kwa mtazamo wa nje na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Adhabu hii ilielezewa kinaratolojia kwa kuzingatia mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, Kutwaliwa kwa Cinji kulimsababishia Muya madhara kama vile kutekenywa na funza pamoja na njaa. Mtazamo wa msimulizi ni kuwa Muya alistahiki kuadhibiwa ndiposa akapewa haki ya kijamii kulingana na matendo yake. Utazamaji na usimulizi wa dondoo hapo juu ulidhihirisha taswira mwono inayotoa picha kamili ya adhabu aliyopata Muya. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa haki ya kijamii ni kipengele cha kimsingi ambacho kilitumiwa kusawiri mwonoulimwengu wa kijamii katika ngano teule.

### 5.2.6 Tabaka

Utazamaji na usimulizi wa tabaka kama kipengele cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii ulijitokeza katika N1 na N3. Kwa mujibu wa Weber (1947), kuwa na mali ama kukosa mali ni pande mbili za utabaka. Katika N1, utazamaji wa utabaka kwa misingi ya kigezo cha mali ulidhihirika. Suala hili lilitazamwa kwa macho ya msimulizi ambaye ni kiwakilishi cha jamii ya Wandia na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> … Hata watu walikuwa wakilipiwa mahari na ukoo iwapo mtu ni maskini. Ndiyo iwapo mtu hana chochote…. Watu wanachanga kila mtu mbuzi mmoja mmoja … Ndiyo yule hana mbuzi angetoa shilingi thelathini, ndizo zilikuwa zikununua mbuzi,

Dondoo hili lilithibitisha mtazamo wa jamii kuhusu uhusiano kati ya tabaka la juu na tabaka la chini. Kitendo cha wanajamii kuchangia barobaro maskini mbuzi ili aoe ni ithibati ya jinsi jamii ya Wandia ilijali maskini. N1 ilijumlisha vibarua katika tabaka la chini huku waajiri wao wakiwekwa kwenye tabaka la juu. Suala hili lilitazamwa na kusimuliwa katika dondoo lifiuatalo;

> Tena mnataka asiende kuwa `ndurua` kwa wenyewe kuajiriwa… akienda kwa wenyewe kuajiriwa kazi huyo ndiye aliitwa `ndũrua`.

Mtazamo wa Wandia kuhusu vibarua ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu na kuonyesha jinsi Wandia walichukia dhana ya mtu kuwa kibarua kwa wenyewe. Taswira uoni katika dondoo hili iliibua taswira hisi ya mateso dhidi ya vibarua, suala ambalo lilichochea jamii kuwaepusha na masaibu ya maisha ya kibarua. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu.

Utazamaji na usimulizi wa matabaka ulihusisha uhusiano kati ya waajiri na waajiriwa katika N3. Uhusiano huu uliafiki msingi wa nadharia ya Umaksi ambapo mabwanyenye hudhulumu waajiriwa. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Cuuaaii! Ndege wa shamba hili
> Paeni
> Hamfahamu maskini na matajiri
> Sawa na Wacinji wetu
> Anayenilalisha kwenye majivu
> Na ninapokula, nalia kwenye kigae
> Aaai! Cuuaaii!
> Paeni

Usimulizi wa mtazamo kuhusu utabaka ulitumia mtindo wa maghani na hivyo basi kuafiki mhimili wa kinaratolojia unaoshikilia kuwa kuna jinsi mbalimbali za kusimulia matukio. Mtazamo huu wa ndani ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na kubainisha kuwa kuna uhusiano mbaya kati ya mabwanyenye na waajiriwa. Dondoo hili lilikashifu uwepo wa matabaka katika jamii. Jazanda ya ndege wasiotambua tofauti kitabaka wanapovamia mashamba yao unaashiria usawa wa binadamu katika jamii. Dondoo hili lilisawiri mtazamo wa Wandia kuhusu uhusiano kati ya mabwanyenye na waajiriwa. Uhusiano huu ulitazamwa kwa mtazamo wa ndani na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza iliyowakilishwa na Muya. Aidha, mikinzano kati ya tabaka la juu na la chini ilitazamwa na kusimuliwa katika dondoo hapo juu. Kwa mujibu wa Muya, ambaye ana tajriba ya kudhulumiwa, mabwanyenye waliwalaza waajiriwa kwenye majivu na kuwapakulia chakula kwenye kigae badala ya sahani. Usimulizi wa mtazamo wa Muya kuhusu utabaka uliibua taswira sikivu Muya alipoamuru ndege wa shamba hilo wapae na kulalamikia uhusiano kati ya maskini na matajiri. Data ya utafiti katika N1 na N3 ilibainisha kuwa utabaka ni kigezo muhimu cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kijamii wa Wandia.

### 5.3 Jinsi Sauti ya Simulizi na Mtazamo Zinavyochangia Mwonoulimwengu wa Kiuchumi wa Wandia

Tumeshataja katika sura ya nne kuwa kilimo, ufugaji, kibarua na biashara ndizo shughuli ambazo zilitumika katika kusawiri mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia. Sehemu hii ilihakiki jinsi sauti ya simulizi na mtazamo zinavyochangia fasiri ya mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia. Uhakiki wa kimaudhui uliofanywa

katika ngano teule ulikitwa kwenye misingi ya mchango wa sauti ya simulizi na mtazamo katika kufanikisha maudhui ya kilimo, ufugaji, kibarua na biashara.

### 5.3.1 Kilimo

Kilimo ni kitega uchumi muhimu ambacho kinahakikishia jamii utoshelevu wa chakula. Mfano, Katika N1, Kabindura, sauti ya simulizi na mtazamo zilidhihirisha kuwa, kilimo ndicho uti wa mgongo wa mfumo wa kiuchumi wa Wandia. Hali hii ilidhihirishwa na data ya utafiti katika dondoo lifuatalo;

> … ndipo Kabindura akakuta msichana akiwinga mtama usiliwe na ndege. Akaenda. Hata hakuongea na msichana huyo. Alienda akaanza kung`oa mtama upande ambapo msichana hakuwa huku akiimba. Msichana akamwambia Kabindura,``wacha kung`oa mtama wetu. Njoo uniambie unachotaka."

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya utafiti unaoshikilia kuwa kuna njia mbalimbali za usimuliaji wa hadithi. Matukio katika dondoo hili yalisimuliwa kwa njia ya nathari. Taswira uoni ilifanikisha usimulizi na utazamaji wa kilimo kwa kuchora picha ya msichana anayewinga ndege ulingoni. Aidha taswira uoni ya Kabindura aking`oa mtama ilibainika wazi. Msichana aliongea kutokana na shinikizo la utambuzi wa nafasi ya kilimo katika jamii ya Wandia. Katika dondoo hili, Kabindura alijitokeza kuwa wakala wa simulizi aliyeendeleza mtazamo wa msimulizi pamoja na Wandia kuhusu kilimo. Kabindura alielewa fika nafasi ya kilimo katika fasiri ya mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia ndiposa akaamua kung`oa mtama akiwa na lengo la kumzindua msichana aongee. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu ambapo mtazamo wa msimulizi na Wandia kwa jumla ulibainishwa.

Sauti ya simulizi na mtazamo zilitumiwa kusawiri mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia katika N3. Kulingana na N3, kilimo ni chanzo cha utoshelevu wa chakula katika jamii. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Haya, wakakaa Muya akiambiwa ``utanitafuta wewe! Na njia nitakayopitia nitakuelekeza. Nitabeba vitu vyote; nibebe mtama, fiwi, njegere, maharagwe na wimbi. Nitabeba chochote kitakachopatikana ili njia utakayopitia uione ikiwa imeota mimea hii."

Cinji ndiye wakala wa simulizi ambaye alidhihirisha ufahamu wa misimu. Hii ndiyo sababu alitapakaza mbegu za kila namna ili mvua ikinyesha kisha mbegu ziote mimea hiyo itumike na Muya kama kielekezi cha alikopelekwa. Kwa upande mwingine uwepo wa aina mbalimbali za mbegu ni ithibati ya kuwepo kwa kilimo cha mimea izaayo mbegu hizo. Sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu ilitumiwa kusimulia mtazamo wa Wandia kuhusu nafasi ya kilimo katika fasiri ya mwonoulimwengu wao.

N3 ilihusisha kilimo na matabaka.Tabaka ni mgawanyiko wa jamii katika vikundi kwa misingi ya cheo, elimu na mali (Weber, 1947). Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, maghani ya Muya ya kuwinga ndege unathibitisha madai haya;

> Cuuaaii! Ndege wa shamba hili
> Paeni!
> Hamfahamu maskini na tajiri
> Sawa na Wacinji wetu, anayenipakulia kigaeni
> Nikilala, hulalia majivu

Dondoo hili liliafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia unaoshikilia kuwa kuna njia mbalimbali za usimuliaji wa hadithi. Utazamaji na usimulizi wa kilimo kama kibainishi cha utabaka katika dondoo hili ulitumia njia ya maghani. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ilitumia mtindo wa maghani kusawiri mtazamo wa jamii kuwa kilmo kinaweza kuwa kibainishi cha matabaka katika jamii. Muya aliwasuta ndege kwa kuwa walipokuwa wakila mtama hawakutofautisha kati ya shamba la maskini na matajiri, suala ambalo lilionyesha utambulisho wa matabaka katika jamii ya Wandia.Utazamaji na usimulizi wa suala la kilimo katika N1 na N3 ulibainisha kuwa kilimo ni kipengele muhimu katika usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia.

### 5.3.2 Ufugaji

Sauti ya simulizi na mtazamo zilitumiwa kuendeleza suala la ufugaji kama mojawapo ya fasiri ya mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia katika ngano teule. Mfano, Katika N1, thamani ya ng`ombe na mbuzi katika jamii ya Wandia ilibainishwa kupitia sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika dondoo lifuatalo;

> Sasa, Kabindura akasema, ``sasa kwa sababu wamekasirishwa na barobaro mimi nitaoa wasichana hao wanaogoma. Na nikiwaoa mtanipatia nini?``Kabindura akaambiwa,``nitakupatia ndama``,

> mwenzake akajitolea, ``nitakupatia mbuzi watano.``Na kwa sababu walikuwa watatu,``nitakupatia fahali. ``

Usimulizi wa matukio katika dondoo hili ulipenyeza mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza kuwa kuna jinsi mbalimbali za usimuliaji wa hadithi. Matukio katika dondoo hili yalisimuliwa kwa njia ya nathari. Dondoo hili lilibainisha kuwa thamani ya mifugo ilikitwa kwenye misingi ya kuwekeana dau. Hapa barobaro watatu ndio wakala wa simulizi waliotumiwa kubainisha dhana ya thamani ya ufugaji katika jamii ya Wandia.

Aidha, thamani ya mifugo ilijitokeza katika dhana ya ulipaji wa mahari. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Ndiyo. Hata watu walikuwa wanalipiwa mahari na ukoo. Iwapo mtu ni masikini. Ndiyo iwapo mtu hana chochote…Watu wangechanga kila mtu mbuzi mmoja mmoja.

Kifungu hiki kilibainisha kuwa umiliki wa mbuzi ulikuwa umeambatanishwa na ulipaji wa mahari. Hii ndiyo sababu hata wanakijiji walihusishwa katika mchakato wa maskini hohehahe kupata mke.

Sauti ya simulizi katika N2, ilithibitisha kuwa ufugaji wa kondoo ulikuwa shughuli muhimu ya kiuchumi katika jamii ya Wandia. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Kondoo wangekatwa mkia na kisha kukatwa vipande vidogo vidogo na kukaangwa jikoni. Vipande hivyo vingekatwa vidogo vidogo kisha vikaletwa kwa sahani.

Usimulizi wa dondoo hili uliibua taswira uoni iliyochora picha ya kondoo bila mkia na vipande vidogo vidogo vya nyama ya mkia wa kondoo vikiwa kwa sahani. Uoni wa vipande vya mkia wa kondoo katika sahani ulizua taswira mwonjo na taswira hii ilitumiwa kutathmini ulafi au udhibiti nafsi wa Wacuka. Katika dondoo hili, mwenyeji ndiye wakala wa simulizi ambaye alidhihirisha umuhimu wa ufugaji wa kondoo kwa kuuambatanisha na kukirimu wageni.

N3 ilifungamanisha usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi na utambuzi wa ufugaji kama chanzo cha ajira. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> …Akaenda. Akaenda, akakuta boma akapewa kazi. Alipopewa kazi ikawa kwamba kazi yake ni kuchunga mifugo. Akachunga mifugo kwa muda…

Taswira mwendo ilitumika kukadiria mwendo mrefu uliobainishwa kwa takriri ya urudiaji wa neno `akaenda` mara mbili. Taswira hii ilionyesha kuwa mifugo walimilikiwa na matajiri ambao hawakupatikana mahali pamoja. Sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu ilitumiwa kusimulia suala la ufugaji na kuonyesha mtazamo wa msimulizi kuwa ufugaji ni chanzo cha ajira. Hii ndiyo sababu Muya aliajiriwa kuchunga ng`ombe. Hata hivyo Muya hakutunzwa vizuri na akaishia kuathiriwa na funza. Mtazamo wa nafsi ya nje ulitumika kubeza kazi ya kibarua.

Sauti ya simulizi na mtazamo katika N4 ziliusawiri ufugaji kama kitega uchumi muhimu ambacho kiliweza kusababisha utangamano ama uhasama wa kijamii. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika kifungu kifuatacho;

> …Sasa Thigiti wakaishi pamoja na Kanyonyo. Kila mmoja alikuwa na ng`ombe wake. Ng`ombe hao walipoanza kuzaa, ng`ombe wa Kanyonyo akazaa, naye wa Thigiti akazaa pia. Mtu aliyekuwa na shida nyingi sana ni Thigiti kwa sababu alitamani mali ya Kanyonyo kwa sababu aliona Kanyonyo alikuwa ametunza ng`ombe wake vizuri ilhali wake hawakuwa wamenona.

Mhimili wa nadharia ya utafiti unaosisitiza kuwa kuna njia mbalimbali za kusimulia hadithi ulijipenyeza katika dondoo hili. Njia ya nathari ilitumika kusimulia matukio. Taswira uoni ilitumika kuchora picha ya jinsi Kanyonyo na Thigiti waliishi maisha ya ujima. Aidha, taswira ya ng`ombe wa Kanyonyo walionona na wale wa Thigiti waliokondeana ilibainika wazi. Thigiti ndiye wakala wa simulizi kwa sababu matendo yake yaliathiri ulimwengu wa hadithi hasa kipengele cha ujima na kusambaratisha uhusiano wake na Kanyonyo. N4 ilibainisha kuwa ufugaji ulichukuliwa kama kipengele muhimu cha usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia kutokana na misingi kuwa kina uwezo wa kudumisha au kusambaratisha mshikamano wa kijamii.Utazamaji na usimulizi wa suala la ufugaji katika N1, N2, N3 na N4 ulitambua nafasi ya ufugaji katika usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia.

### 5.3.3 Biashara

Dhana ya biashara ilitazamwa kwa kina katika N1. Biashara ilitumiwa kama kipengele muhimu cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia. Dhana ya biashara ilijitokeza katika taswira ya ukadiriaji wa thamani ya mbuzi. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Na iwapo mtu hana chochote na ni king`ong`oi, watu wangechanga kila mtu mbuzi mmoja mmoja… ndiyo yule ambaye hana mbuzi angetoa shilingi thelathini, ndizo zilikuwa zikununua mbuzi…ndiyo. Wewe utoe thelathini iwapo huna mbuzi. Mtu mwenye mbuzi atoe mbuzi…walikuwa rahisi sababu ungeuza debe ya mtama.

Katika dondoo hili, sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu, ilitambua biashara ya uuzaji wa mbuzi. Hii ndiyo sababu, iwapo mwanajamii hangeweza kumudu mbuzi mmoja, ingembidi kuchanga shilingi thelathini ambazo zilikuwa thamani ya mbuzi mmoja.

Sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu pia ilisimulia biashara ya mtama. Hapa, msimulizi alibainisha kuwa debe ya mtama iligharimu shilingi thelathini sawia na mbuzi mmoja. Mtazamo wa msimulizi na Wandia kwa jumla ni kwamba biashara ni mhimili mkuu wa usawiri wa mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu.

## 5.4 Jinsi Sauti ya Simulizi na Mtazamo Zinavyochangia Usawiri wa Mwonwoulimwengu wa Kisiasa Katika Ngano Teule

Sauti ya simulizi na mtazamo ni nyenzo ambazo zilitumika kutazama na kusimulia mwonoulimwengu wa kisiasa katika baadhi ya ngano teule. Uhakiki wa kimaudhui wa data ya uhakiki ulithibitisha kuwa masuala yaliyoelezea fasiri ya mwonoulimwengu wa kisiasa ni kama vile; usuluhisi wa migogoro, uongozi na haki. Usulihisi wa migogoro umejadiliwa katika sehemu inayofuata.

### 5.4.1 Usuluhishi wa Migogoro

Suala la usuluhishi wa migogoro lilitazamwa na kusimuliwa katika N4. Msimulizi, ambaye ni mwenye mtazamo wa nje, alibainisha kuwa usuluhishi wa migogoro ya kijamii ni kigezo muhimu cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia. Hali hii iljitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Alipobadilisha ndama, Kanyonyo akamwambia Thigiti,``wewe unakosea. Unakosea kwa sababu ulibadilisha ndama. Ulichukua ndama wangu, tutaenda kwa baraza la wazee.

Dondoo hili lilibainisha kuwa Thigiti ndiye wakala wa simulizi ambaye aliendeleza msuko wa simulizi hii kwa kubadilisha ndama wa Kanyonyo. Vivyo hivyo Kanyonyo ni wakala wa simulizi kwa kuchukua hatua ya kumshtaki Thigiti kwa baraza la wazee. Mashtaka haya yaliathiri ulimwengu wa ngano hii na kuendeleza msuko wake. Muktadha huu una mshabaha na kazi ya Leakey (1977) na Kenyatta (1938) zinazoelezea kuwa kesi ziliendeshewa nyanjani.

Mashtaka haya yalisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu na kubainisha mtazamo wa jamii kuhusu usuluhishi wa migogoro katika jamii. Sauti ya simulizi ya kutoka nje ilibainisha dhima ya baraza la wazee katika usuluhishaji wa migogoro ya kijamii. Badala ya kuchukua sheria mkononi, Kanyonyo alienda kumshtaki Thigiti kwa baraza la wazee. Baraza hili lilianzisha mchakato wa kusikilizwa kwa kesi. Msimulizi alieleza kuwa kesi ilisikizwa uwanjani juu ya jabali lililofunika shimo alimokuwa barobaro. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Tutaenda kwa baraza la wazee, baraza hili litaamulia kesi kule uwanjani. Kule uwanjani kulikuwa kumechimbwa shimo. Ndani ya shimo hilo mliwekwa kijana na wazee wa baraza.

Umuhimu wa baraza la wazee ni kuhakikisha kuwa sera za utafutaji wa haki zilifuatwa ili kuhakikishia wanajamii haki kwa mujibu wa sheria. Hivyo basi, kuwepo kwa haki katika jamii kulipunguza migogoro ya kijamii na matokeo yake yakawa utangamano wa kijamii. Huu ndio mtazamo wa Wandia na fasiri ya mwonoulimwengu wao wa kisiasa kwa misingi ya kipengele cha usuluhishi wa migogoro.

Mtazamo wa Wandia kuhusu washukiwa ulibainisha kuwa mshukiwa huwa hana kosa mpaka ithibitike kuwa amekosea. Dhana hii ina mshabaha na kauli ya kikatiba inayoshikilia kuwa mshukiwa hana hatia mpaka ithibitike kuwa amekosea (Katiba Mpya ya Kenya 2010: Sehemu ya 50. Ibara ya 2a). Hii ndiyo sababu ilibidi kesi isikizwe ili kutafuta ithibati madhubuti za kuwezesha maamuzi ya kesi yaliyokitwa kwenye haki na kweli. Mtazamo huu unaoana na maoni ya Magesa (1998) anapodai kuwa usuluhishi

wa migogoro ya kijamii ulishurutisha waamuzi kusikiza pande zote mbili na hata mashahidi na kisha kuamua kesi.

Hatua ya tatu ya usuluhishi wa mgogoro ni kusikizwa kwa kesi. Sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu ilisimulia suala hili na kubainisha mtazamo wa Wandia kuhusu umuhimu wa kusikizwa kwa kesi. Mathalan, Kesi iliendeshwa juu ya shimo lililofunikwa kwa jabali. Baraza la wazee liliamuru Thigiti na Kanyonyo kuvuta jabali kwa zamu. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Alijaribu, akavuta, akavuta, alipovuta akachoka, akasema,"sasa ninachoka jinsi hii na ni ndama wa Kanyonyo niliyeiba?" Naye mtu aliye shimoni anasikiza na kuandika taarifa yake. Zamu ya Kanyonyo ilipofika aliamrishwa kulivuta na kuondoa jabali kutoka hapo. Alijaribu kuondoa akashindwa na papo hapo akasema. "sasa si ninachoka hivi kwa sababu ndama wangu aliibiwa na Thigiti? Sitavuta tena"

Barobaro aliyekuwa shimoni alinakili maungamo hayo na yakatumiwa kama ushahidi madhubuti wakati wa maamuzi ya kesi. Muktadha huu ulimfanya barobaro aliyekuwa shimoni wakala wa simulizi kwa kuwa maandishi yake yaliathiri mkondo wa maamuzi ya kesi. Thigiti alipatikana na makosa ya wizi wa ndama wa Kanyonyo.

Mchakato wa usuluhishi wa migogoro ni maamuzi ya kesi. Hatua hii ilihusisha barobaro aliyetoka shimoni akiwa na maandishi kuhusu maungamo ya Thigiti na Kanyonyo. Kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> Wewe Thigiti ulisemaje? Maandishi yako ndiyo haya, eti unachoka hivyo na ni ndama wa Kanyonyo uliiba ili aboreshe ng'ombe wako wawe wanono. Nawe Kanyonyo unachoka hivyo na ni wewe uliibiwa ndama wako kwa sababu umemtunza vizuri.

Maandishi haya yalitumika kama msingi wa kuongoza uamuzi wa kesi hii. Uamuzi huu ambao ulibainisha kuwa Thigiti ndiye mwizi pia ulipendekeza hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi ya Thigiti. Hukumu ya kifo ilitolewa kwa Thigiti na akauawa kwa kufungiwa matawi makavu ya mgomba na kuwashwa moto. Kanyonyo akarudishiwa ndama wake.

Mtazamo wa msimulizi na ambao ndio mtazamo wa jamii ni kwamba kosa la wizi ni kosa la jinai na adhabu yake ni kifo. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Sauti hii ndiyo sauti ya jamii iliyoashiria mtazamo wa jamii ya Wandia

kuhusu usuluhishi wa migogoro ya kijamii. Madhali ngano za Wandia zilitokana na tajiriba ya Wandia, inadhihirika kuwa mbinu za usuluhishi wa migogoro ambazo zilirejelewa ni baadhi ya fasiri ya mwonoulimwengu wao wa kisiasa. Sababu ni kuwa usuluhishi wa migogoro katika jamii ni hakikisho la umoja, amani na utangamano. Masuala haya ndio msingi wa maendeleo katika jamii

Sauti ya simulizi na mtazamo zilitumiwa kusawiri mgogoro baina ya wanyama wenye pembe na sungura katika N5. Kiini cha mgogoro huu ni ulaghai wa sungura uliotokana na kususia kuchimba kisima lakini akaapa kutumia maji ya kisima hicho. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika kifungu kifuatacho;

> Sungura akajua kuwa kwa kuwa hakwenda kuchimba kisima, ``nitatumia ujanja wangu. Hebu mimi niende nikanywe maji sababu sikushiriki uchimbaji wa kisima``, Akavaa majani makavu ya mgomba… "Njooni muone! Aia! Aia! Majani makavu ya mgomba yanakunywa maji huku yakichota``

Dondoo hili lilidhihirisha kuwa sungura ndiye wakala wa simulizi ambaye kususia kwake kushirikiana na wanyama wengine katika uchimbaji wa kisima kulichangia mgogoro huu kwa kiasi kikubwa. Sungura aliendeleza maudhui ya ulaghai na kuibua mtazamo wa jamii kuhusu walaghai katika kupalilia migogoro ya kijamii. Msimulizi alipotazama, alisawiri taswira ya ushirikiano wa wanyama katika uchimbaji wa kisima na kwa upande mwingine alisawiri ukaidi na ubinafsi wa Sungura. Mtazamo wa msimulizi ni kwamba sungura alistahiki kutengwa na jamii kwa kukosa kushirikiana na wanyama wengine. Hapa, tunaisikia sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu ikisimulia mtazamo huu ambao ni kielelezo cha mtazamo wa tajriba ya Wandia. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinaendeleza mgogoro huu;

> Siku iliyofuata akajua hangevaa majani makavu ya mgomba. "Nitajibadilisha kwa kitu kingine nisije kujulikana." Ndipo akakumbuka matawi ya mwaloni…akajifunga ili aachiwe macho tu… ndiyo sababu akigaragara nayo yanaimba jinsi anavyoenda.

Sungura aliendelea kuchukua nafasi ya wakala wa simulizi na kuendeleza msuko wa ngano hii kwa kujifungia matawi ya mwaloni ili asitambulike kwa urahisi. Kuchota maji kwa sungura ndiko kulipalilia mwendelezo wa mgogoro huu na kushurutisha wanyama kuanza kushika doria. Hali hii inathibitishwa katika dondoo lifuatalo;

> Wazee wanne walishika doria na wakamkamata sungura. Sungura alipokamatwa alipelekwa pale ambapo alipaswa kuchomewa…

> Alipokamatwa ndipo alidanganya ili asipelekwe chunguni… sasa wazee wakampokeza sungura kwa wanawake… wakaambiwa wamweke vizuri ili asitoroke…mke alipoenda kumshika sungura na ni mnyama mwenye utelezi kwa sababu ya manyoya…akaponyoka akatoroka.

Dondoo hili lilibainisha kuwa wazee wanne walioshika doria ndio wakala wa simulizi. Katika muktadha huu wazee wanne walikuwa na lengo la kuhakikisha kuwa utapeli wa sungura umekomeshwa. Sungura aliendelea kuchangia mwendelezo wa msuko kwa kuwa wakala wa simulizi aliyethubutu kuchota maji kinyume cha sheria. Sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu iliendeleza usimulizi wa mgogoro huu kwa siku ya pili. Sungura alijifunga matawi ya mwaloni na kuimba huku akichota maji. Siku hiyo Sungura alikamatwa na wazee wanne kabla ya kuchota maji. Mchakato wa usuluhishi wa mgogoro huu ulishurutisha Sungura kuhukumiwa kifo kwa kutumbukizwa kwenye chungu chenye maji yaliyotokota. Japo sungura aliweza kuponyoka na kutoroka hakurudi tena kuchota maji na mgogoro huu ukasuluhishwa hivyo. Uhakiki ulibainisha kuwa wanyama walioshiriki kuchimba kisima ndio wenye nguvu na uwezo wa kudhibiti matumizi ya maji ya kisima hicho. Isitoshe nguvu hizi zilipokezwa wanyama wenyewe na kuwapa haki miliki ya kisima. Haki hii ya matumizi ya maji ya kisima ilibainisha mipaka ya wanyama wenye haki ya kutumia kisima. Hapa mtazamo wa msimulizi ni kwamba mtu yeyote hana budi kushirikiana na wanajamii wenzake katika jitihada za kutatua matatizo ya kijamii ili asitengwe na jamii kama alivyotengwa sungura. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu.

N6 ilibainisha kuwa, suala la usuluhishi wa migogoro ni kipengele muhimu cha fasiri ya mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> Fisi akikaakaa, mtoto akasema
> Ihi! Ihi! Ihi!Ihi!, akaulizwa na mama yake, ``unataka nini?,`` ``ninataka kuuma uwayo wa ndovu mafuta yachirizike ta!
> Mtoto mwingine akasema,
> ``Ehe! Ehe! Ehe!Ehe!``
> Akaulizwa,`` unataka nini?``
> Ninataka kuuma uwayo wa ndovu mafuta yachirizike ta!
> Naye mume akasema
> ``Ehe!Ehe!Ehe!Ehe!``
> Akaulizwa ,``unataka nini?``
> Ninataka kuuma uwayo wa ndovu mafuta yachirizike ta!
> Naye mke akaiga, ``Ehe! Ehe!Ehe!Ehe!``
> Akaulizwa, `` unataka nini?``

Ninataka kuuma uwayo wa ndovu mafuta yachirizike ta!

Katika dondoo hili, fisi, mkewe na wana wao wawili ndio wakala wa simulizi wanaoendeleza mgogoro. Chanzo cha mgogoro huu ni dhuluma aliyotendewa ndovu mjamzito na familia ya fisi. Suala la dhuluma limetazamwa na kusimuliwa na ndilo msingi wa mgogoro huu. Tanzia ya kifo cha ndovu ilizua taharuki na mtafaruku baina ya familia ya ndovu na fisi. Data ya utafiti inathibitisha madai haya katika dondoo lifuatalo;

Wale watoto wa ndovu waliokuwa tumboni mwa mama yao walitoroka
Wakachomoka, wakatoroka na kumwacha mama yao akiliwa.

Katika dondoo hili, udhalimu wa fisi umesimuliwa kupitia kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Sauti hii inabainisha mtazamo wa nje ambao unasisitiza kuwa dhuluma ni kinyume cha haki na anayedhulumu hana budi kuadhibiwa. Suala la dhuluma limeendelezwa na watoto wa ndovu kupitia wimbo ufuatao;

Ndovu hawa mlienda kukawia
Mlienda kukawia na msirudi
Mkamwacha mama nyikani mwa fisi
Mtoto wa fisi akilia,`` niume uwayo wa ndovu``
Kukicha asubuhi, ni Ii! Ii!,uwayo,uwayo wa ndovu
Ikifika jioni ni Ii!Ii!uwayo, uwayo wa ndovu

Katika dondoo hili, mtindo wa wimbo ulitumiwa kuchora taswira ya dhuluma aliotendewa ndovu mjamzito na fisi. Dondoo hili lilibainisha kuwa, watoto wawili wa ndovu ndio wakala wa simulizi kwa kuwa kutoroka kwao na kuwapasha ujumbe ndovu wengine ndiko kulikoanzisha mchakato wa utafutaji wa haki na ulipizaji wa kisasi dhidi ya fisi. Katika wimbo huu, watoto wa ndovu wanawalaumu ndovu wengine kwa kukawia kurudi na kuwapa fisi nafasi ya kumla mama yao mjamzito. Muktadha huu hivyo basi unawafanya ndovu wengine wakala wa simulizi.

Mtazamo wa msimulizi na ambao ndio mtazamo wa jamii ni kwamba kosa la mauaji ni kosa la jinai na adhabu yake ni kifo. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Sauti hii ndiyo sauti ya jamii na inaashiria mtazamo wa jamii ya Wandia kuhusu usuluhishi wa migogoro ya kijamii. Madhali ngano za Wandia zinatokana na tajiriba ya Wandia, ni dhahiri kuwa mbinu za usuluhishi wa migogoro ambazo zimerejelewa ni baadhi ya fasiri ya mwonoulimwengu wao wa kisiasa. Sababu

ni kuwa usuluhishi wa migogoro katika jamii ni hakikisho la umoja, amani na utangamano. Masuala haya ndio msingi wa maendeleo katika jamii

### 5.4.2 Uongozi

Sauti ya simulizi na mtazamo zilitumika kusawiri suala la uongozi katika baadhi ya hadithi teule. Muktadha wa kiuhakiki ulibainisha kuwa sauti ya simulizi na mtazamo ndizo nyenzo ambazo zilitumika kusawiri mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia. Mfano;N5 ilitambulisha sifa za uongozi bora. Kifungu kifuatacho kinathibitisha madai haya;

> "….. Njooni tusemezane. Tutasema hivi, kichaka kitachomwa na sasa mnyama yeyote ambaye hatakuwa amekatwa pembe hatapata mahali pa kutorokea. Sasa tutatafuta mafundi na watu wa kuchimba mashimo ili kitakapochomeka tupate mahali pa kutorokea."

Dondoo hili lilibainisha kuwa paa ndiye wakala wa simulizi kwa kushawishi wanyama wakatwe pembe na kuchimba mashimo ya kujificha. Kitendo hiki kiliendeleza msuko wa N5. Paa alitazama suala la uongozi na mtazamo wake kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza. Paa alipotazama, alidhihirisha sifa za uongozi bora. Paa alitwikwa mamlaka ya kuongoza wanyama wengine porini. Uongozi bora ulihakikishia watawaliwa usalama wao. Mtazamo wa paa ni kuwa kiongozi bora alipogundua hatari iliyowakabili watawaliwa, alipaswa kuwatahadharisha ili waweze kuepuka au kukabiliana na hatari hiyo. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ilisimulia tahadhari kuhusu hatari ya kuchomwa kwa kichaka. Isitoshe, sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ilipendekeza hatua za kujitanzua kutokana na janga hili. Sauti hii ya simulizi ilisimulia mtazamo kuwa uongozi bora ulijumuisha sio tu kutahadharisha wanajamii kuhusu hatari bali kupendekeza mikakati ya kupambana na kushinda majanga ya kijamii kama alivyofanya Paa. Mathalan, Paa alipendekeza mhanga na nungunungu wapewe kibarua cha kuchimba mashimo ili kichaka kikichomeka waweze kujificha humo.

Utazamaji wa Paa kuhusu uongozi ulisisitiza kushirikisha umma katika mwono wa kiongozi. Mojawapo wa mwono wa kiongozi ulihusiana na miradi ya maendeleo ya kijamii. Kupitia mtazamo wa ndani, ilibainika kuwa kufaulu kwa miradi ya maendeleo ya kijamii kulitegemea kiwango cha uhusishaji wa jamii. Mathalan; Paa alipofahamu kuwa baada ya kichaka kuwashwa moto mito yote ingekauka, alipendekeza kuchimbwa kwa kisima. Kifungu kifuatacho kinadhibitisha haya;

> Wakakaa mashimoni. Sasa walipoendelea kukaa mashimoni si moto ulizimika? Wakatoka. Sasa wakaambiana ``tuliafikiana kuwa tutakapotoka mashimoni tutachimba kisima”.

Mwono wa paa, ulimfanya wakala wa simulizi kwa kushawishi wanyama kuchimba kisima na kuendeleza msuko wa simulizi hii. Paa aliwashirikisha wanyama wote katika uchimbaji wa kisima na jitihada zao zikafanikiwa. Mtazamo huu ulishikilia kuwa jamii ilibidi kushirikishwa katika miradi ya maendeleo. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya ndani kupitia kwa kiongozi Paa. Msimulizi ambaye aliwakilisha mtazamaji wa nje na sauti simulizi ya nje alitazama suala la uongozi. Msimulizi aliichora taswira ya kiongozi bora. Baadhi ya taswira hizi ni kama vile; kuwa kiongozi mwenye maono kuhusu maendeleo ya jamii kwa jumla, kutahadharisha umma kuhusu hatari inayoikabili jamii na kupendekeza mikakati ya kuepuka maangamizi pamoja na kulinda rasilimali za jamii. Mtazamo wa nje ulimsawiri Paa kama kiongozi mwenye madaraka yaliyomwezesha kutoa maamuzi kwa niaba ya jamii au kushirikisha jamii katika kuyafikia maamuzi hayo.

N6, Ndovu na Fisi, ilitumia taswira kueleza dhana ya uongozi mzuri na uongozi mbaya. Data ya utafiti imethitisha na kusawiri uongozi bora katika kifungu kifuatacho;

> Wakaanza safari. Wakaenda, wakaenda. Walipoenda yule aliyekuwa mjamzito akashindwa kuendelea na safari. Wakienda hivyo akasema ameshindwa na kutembea. Wakateremka. Kiongozi wao akasema, `` sasa kwa sababu tuko kwa fisi tutamwombea mahali pa kulala. Akaambiwa akae hapo.

Katika kifungu hiki, kiongozi wao amejitokeza kuwa wakala wa simulizi ambaye alipendekeza suluhisho la tatizo la ndovu mjamzito la kushindwa kutembea kwa kumwombea mahali pa kulala. Mtazamo wa ndovu ni kuwa uongozi bora unahakikisha kuwa umezingatia maslahi ya umma kama alivyofanya kinara wa ndovu. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza.

Mchakato wa kudai fidia kwa ndovu mjamzito aliyeliwa na fisi ulidhihirisha uongozi bora ambao ulijali maslahi ya wote. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya;

> Wakaja. Mkutano ukapangwa.
> Ii! Ndovu mwenzetu tulipomwacha kwenu mlifanya nini?

> ``Tulimla`` ,`` Ni watoto waliomla! Sisi hata hatukujua alivyofanyiwa kwa sababu ni watoto waliomla tulipowaacha hapo… Wakaambiwa ,`` sasa ni vita! Vita vikaanza”. Fisi wakapiga ndovu kwa mijeledi.

Usimulizi na utazamaji wa suala la uongozi katika dondoo hili ulizingatia mfuatano wa matukio kiusababishi.Mfano, kupanga mkutano, majibizano kati ya fisi na ndovu na mwishowe vita. Usimulizi na utazamaji wa matukio katika dondoo hili ulizua taswira uoni ambayo iliiwezesha hadhira kuunda picha ya majibizano na vita baina ya ndovu na fisi hasa fisi wakitumia mijeledi. Uongozi mbaya unakosa kuwajibikia matendo ya mtu binafsi au jamii. Kwa mfano fisi alipotakiwa kueleza kwa nini walimla ndovu mjamzito, fisi alihepa swahili hilo kwa kudai kuwa ni watoto waliomla na kwamba yeye na mkewe hawakushiriki. Mtazamo wa msimulizi ni kwamba kiongozi anapaswa kuwajibikia matendo yake na ya jamii kwa jumla. Mtazamo huu umesimuliwa kwa sauti ya simulizi ya kutoka nje.

Kwa upande mwingine sauti ya simulizi na mtazamo zilitumiwa kusawiri uongozi mbaya katika N6. Uongozi mbaya ulidhihirika kutokana na fisi kushindwa kuongoza familia yake vizuri. Hali hii ilijitokeza katika data ya utafiti. Mfano, kifungu kifuatacho kinathibitisha haya;

> …Mtoto wa Fisi akilia.
> Niume uwayo wa Ndovu.
> Kukicha asubuhi,
> Ii! Ii!Uwayo wa ndovu
> Sasa anataka asubuhi aume na jioni aume.
> Ndiposa anaambiwa Ii! Ii!...
> Aume Ndovu
> Je? Kuna wakati ambapo hataki?

Katika dondoo hili mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi umejipenyeza. Mfano, kilio cha mtoto kinafuatwa na kuomba idhini ya kuuma uwayo wa ndovu. Taswira uoni iliiwezesha hadhira kuumba picha mawazoni ya mtoto wa fisi akilia na kuuma uwayo wa ndovu. Katika dondoo hili, mapuuza ya fisi yalimfanya wakala wa simulizi ambaye alisababisha kuliwa kwa ndovu mjamzito. Katika kutazama na kusimulia uongozi mbaya, sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu ilitumika kuonyesha jinsi fisi alishindwa kudhibiti mkewe na watoto wake. Watoto wa fisi na mama yao walipoomba idhini ya kuuma wayo wa ndovu, anawaidhinisha.

Mwishowe hata fisi mwenyewe akashiriki uovu wa kumla ndovu mjamzito. Hapa uongozi wa fisi umekosa lengo na mwelekeo. Hivyo basi huu ni uongozi mbaya.

Aidha, usimulizi na utazamaji wa uongozi mbaya ulibainisha kuwa uongozi wa aina hii haukadirii matokeo ya kadhia yenye hatari na hivyo kuhatarisha maisha ya umma. Data ya utafiti imethibitisha haya katika kifungu kifuatacho;

> Haya! Wakaambiwa, “sasa tunataka ndovu mwenzetu.”, wakaambiwa,``sasa ni vita! Sasa ni vita tutapigana mpaka mtupatie ndovu mwenzetu. Vita vikaanza. Fisi wakapiga ndovu kwa mijeledi… naye ndovu akasema, “Aa! Achaneni na hao! Wacha niwaangushie kimoja tu!...” wakang`oa mti mzima. waliporushiwa walikufa wote.

Dondoo hili limeafiki mhimili wa nadharia ya naratolojia unaosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi. Mfano, vita kupangwa, fisi kupiga ndovu kwa mijeledi, ndovu kung`oa mti na kurushia fisi na kuwaua wote. Aidha, mhimili wa nadharia ya utafiti unaotambua uwepo wa njia mbalimbali za usimuliaji wa hadithi umejipenyeza kwa kutumia maelezo ya kinathari. Taswira uoni iliwezesha hadhira kuona mawazoni picha ya mandhari hatari ya vita baina ya ndovu na fisi. Aidha, taswira ya upumbavu wa fisi ilibainika wazi kutokana na fisi kuwapiga ndovu kwa mijeledi. Hiki ni kinaya. Sauti ya simulizi ya nje ilisimulia mtazamo kwamba uongozi mbaya haukadirii matokeo ya kadhia yenye hatari kama vile vita. Hatima yake ni maangamizi ya jamii. Mtazamo wa msimulizi ni kwamba kiongozi anapaswa kuwajibikia matendo yake na ya jamii kwa jumla. Mtazamo huu umesimuliwa kwa sauti ya simulizi ya kutoka nje. Mtazamo wa msimulizi ulidhihirisha kuwa makosa ya jinai yanapaswa kukabiliwa kwa vyovyote vile. N6, ilitoa adhabu ya kifo kwa fisi wote walioshiriki unyama wa kumla ndovu mjamzito. Kifo cha fisi na aila yake ni fidia ya kifo cha ndovu mjamzito na uhakikisho kuwa unyama kama huo haungeweza kutendeka tena.

### 5.4.3 Haki

Suala la haki lilitazamwa katika N4 na N5. Mfano, katika N4, suala la haki lilitazamwa na kusimuliwa na hasa linahusu wizi wa ndama wa Kanyonyo uliotekelezwa na Thigiti. Dondoo lifuatalo linathibitisha madai haya;

> Wale wazee wakasema, `` tutafanya hivi ili tujue ni nani aliyeiba ndama. Wewe ndiwe utakayeondoa jabali. Kina Thigiti wakaambiwa, `` sasa twende, sasa tukashuhudie mkiliondoa jabali. Naye mtu yuko ndani.

> Sasa Thigiti ndiye alikuwa na shida sana kwa kuwa alitamani ndama wa Kanyonyo. Akaambiwa, sasa wewe ndiwe utakayeanzia kwa sababu mtu yule ambaye anashukiwa ndiye huwa na shida.Alijaribu, akavuta, akavuta, alipovuta akachoka akasema,``sasa ninachoka jinsi hii na ni ndama wa Kanyonyo niliyeiba… Aaaai! Sitavuta tena sababu ninachoka bure. Mimi ndiye mwizi  wa ndama wa mwenyewe.``Kanyonyo naye akaambiwa na wazee,``ingia hapo``. Kanyonyo akasukuma, akasukuma, akasukuma akasema,``sasa ninachoka hivi kwa sababu ndama wangu aliibiwa na Thigiti. Sitavuta tena!.``Aliye ndani ya shimo anaendelea kuandika.

Nafasi ya baraza la wazee ilitazamwa kwa macho ya mtazamaji  wa ndani. Wazee wa baraza ndio wakala wa simulizi ambao kwa kutumia mtazamo wa ndani waliendesha kesi juu ya jabali. Utazamaji huu ulijumlisha kuamrisha Thigiti na Kanyonyo kuvuta jabali ili kushinikiza ungamo. Utazamaji huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza iliyowakilishwa  na wazee. Aidha, mtazamo wa nje uliohusishwa na Fanani ulidhihirika. Mtazamo huu uliibua taswira kuwa uvutaji wa jabali ni adhabu kali iliyotazamiwa kushinikiza ungamo. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Barobaro aliyekuwa shimoni alichukua nafasi ya wakala wa simulizi  na mchakato wa utafutaji wa haki ulitarajiwa kubadilika pindi tu barobaro akianza kutekeleza wajibu wake na kuweka wazi ushahidi. Taswira uoni pamoja na taswira mwendo zilizotokana na kitendo cha usukumaji wa  jabali ziliibua taswira ya adhabu kali. Kinaya ni kwamba mbinu hii ya utafutaji wa haki kwanza inamtesa Kanyonyo kwa kumshirikisha  katika usukumaji wa jabali kabla ya kumfidia baada ya ukweli kujulikana.

Hukumu huwa kilele cha mchakato wa utafutaji wa haki. Hukumu inaweza kumweka mshukiwa kwenye lawama au kumwondolea lawama. Hali hii ilithibitika  katika data ya utafiti. Mfano, hukumu ya kesi kati ya Kanyonyo na Thigiti ilitazamwa na kusimuliwa kupitia sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza  katika dondoo lifuatalo:

> Yule kijana alikuja… alikuja akawaambia,`` Je, mnajua mimi ndiye nilikuwa  mwamuzi katika kesi hii?``Wewe Thigiti ulisemaje? Maandishi yako ndiyo haya, eti unachoka hivyo na ni ndama wa Kanyonyo uliiba ili uboreshe wako wawe wanene.  Nawe  Kanyonyo unachoka hivyo na ni wewe uliibiwa ndama wako kwa sababu umemtunza vizuri. Sasa ninyi amueni kesi hii.” Wazee wakasoma barua. Ilithibitika kwamba Thigiti ndiye mwizi. Wakati huo watu walikuwa wakiwekwa kwa mzinga au kufungiwa matawi makavu ya mgomba… unawashwa moto…. Sasa ng`ombe wameachiwa Kanyonyo, Thigiti akachomwa.

Dondoo hili lilithibitisha kuwa barobaro aliyekuwa shimoni ndiye wakala wa simulizi na sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza iliyotumika kusimulia mchakato mzima wa kutekeleza hukumu iliyokitwa kwenye haki. Mtazamo wa ndani ulitumika kubainisha ukweli kwa kuweka bayana ushahidi, suala ambalo lilidhihirisha mtazamo wa Wandia kuhusu umuhimu wa ushahidi na ukweli katika kutoa hukumu zilizokitwa kwenye haki pasipo mapendeleo. Mchakato mzima wa utafutaji wa ushahidi na hukumu ulisimuliwa kwa kuzingatia misingi ya mawazo ya Propp (1928) inayosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi. Sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu inayowakilishwa na Fanani ilitumiwa kusimulia mtazamo wa Fanani Wanjira wa Rukenya kuhusu uhalifu na haki. Mtazamo wa jamii hii ni kwamba mwizi alipaswa kufa. Muktadha wa uwasilishaji ulizua msisimko kutoka kwa Fanani Wanjira wa Rukenya na kubainisha kuwa kifo cha Thigiti kilitokana na hukumu ya haki. Aidha Kanyonyo alipewa haki kwa kurejeshewa ndama wake pamoja na ng`ombe wa Thigiti kama fidia. Mtazamo wa msimulizi na Wandia ulibainika wazi katika wimbo wa `Kaguru`;

> *Kaguru* lalia mtu
> *Kaguru* lalia mtu
> Mwizi hana mwenyewe
> Mchawi hana mwenyewe

Muktadha wa usimulizi uliibua taswira ya mtu mpweke, yaani uovu wa mwizi ulishurutisha kutoungwa mkono na mwanajamii yeyote. Hivyo basi hana budi kukabaliana na mkono mrefu wa sheria. Wimbo huu uliafiki mhimili wa kinaratolojia unaoshikilia kuwa kuna njia nyingi za uwasilishaji wa matukio.

Suala la haki kama kipengele cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kisiasa lilitazamwa kwa macho ya sungura katika N5. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya ndani na ya nje. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika dondoo lifuatalo:

> Wakakaa. Wakaenda wakachimba kisima. Wakaambiana,``na yeyote yule hatachimba kisima hatakunywa maji hayo.. sungura akajua kwa kuwa hakwenda kuchimba kisima,``nitatumia ujanja wangu, hebu niende nikanywe maji sababu sikushiriki uchimbaji wa kisima."

Dondoo hili lilibainisha kuwa taswira sikivu ilitumika kuweka wazi masharti ya matumizi ya maji ya kisima kwa wanyama walioshiriki uchimbaji wa kisima pekee. Kwa upande mwingine wale waliosusia walinyimwa haki ya kutumia maji hayo. Muktadha wa kupata haki na kunyima haki uliibua mtazamo wa Wandia kuhusu

ushirika wa kijamii. Mtazamo huu ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na kuibua dhana ya kushirikisha wanyama katika maamuzi hayo. Sheria ya haki ya matumizi ya maji ililenga haki ya matumizi ya maji ya kisima kwa walioshiriki kuchimba kisima pekee na ilipovunjwa na sungura, mchakato wa kumkomesha ukaanza kama njia ya kudumisha haki ya matumizi ya maji kwa wanyama waliostahili. Usimulizi wa mtazamo huu ulizingatia mantiki ya mhimili wa kinaratolojia uliosisitiza mfuatano wa matukio kiusababishi (Propp, 1928). Usimulizi umethibitisha kuwa sungura ndiye wakala wa simulizi kwa kunywa maji kinyume cha sheria ya haki ya matumizi ya maji ya kisima.

Ukiukaji wa haki ya kutumia maji ya kisima ulitazamwa kwa macho ya fanani na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika dondoo lifuatalo;

> Akavaa majani matawi.
> Matawi yakining`ng`inia.
> Hayo ndiyo alijifunga ili akienda asijulikane kwanza unajua ni mfupi.
> Akienda hivyo, unajua akienda ni kama matawi yanayotembea… Ni kama kwamba anajigaragaza akienda kuchota maji.
> Wanyama wakaambiana, ``Njooni muone. Ala! Aiah!
> Njooni muone matawi yanakunywa maji huku yakichota.
> Siku iliyofuata ndipo akakumbuka matawi ya mwaloni. Akajifungia ili aachiwe macho tu.

Utapeli wa sungura ulitazamwa kwa mtazamo wa nje na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Usimulizi uliibua taswira uoni iliyobainisha uovu wa sungura kutokana na ukiukaji wa haki ya utumiaji wa maji ya kisima kwa mujibu wa sheria za wanyama. Uovu huu ulisisitizwa kwa matumizi ya uradidi uliohusu urudiaji wa kifungu `njooni muone` na kuibua taswira uoni. Taswira hii ilionyesha kinaya cha sungura kuchota maji kinyume cha sheria. Huu ni ukiukaji wa haki. Usimulizi wa ukiukaji huu wa haki ya matumizi ya maji ya kisima ulisimuliwa kwa kuzingatia mantiki ya Propp (1928) ya mfuatano wa matukio kiusababishi. Mikakati ya kumkomesha sungura kunyemelea maji ya kisima na kuwapokonya wanyama wengine haki yao ilitazamwa kwa macho ya Fanani na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Data ya utafiti ilithibitisha madai haya katika kifungu kifuatacho;

> Wazee wanne walimkamata sungura… sungura alipokamatwa alipelekwa pale ambapo alipaswa kuchomewa…alipokamatwa ndipo

> alipodanganya ili asipelekwe chunguni. Mke alipoenda kumshika, sungura akaponyoka na kutoroka.

Dondoo hili lilibainisha mtazamo wa Wandia kwamba mtu hana haki ya kufaidi jasho la wengine. Aidha mhusika akijitenga na jamii hapaswi kuhurumiwa kwa vyovyote vile. Mtazamo wa nje ulitumika kutazama mikakati ya kukomesha utapeli wa sungura na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu. Mtazamo huu ulisadikika kwa sababu fanani ni kiwakilishi cha jamii. Dondoo hili lilibainisha kuwa taswira mwendo, taswira uoni na taswira hisi zilitumika kuibua taharuki iliyosababishwa na hatari iliyomkabili sungura kutokana na kukamatwa kwake.

Kwa mujibu wa N6, Ndovu na Fisi , mtazamo kuhusu haki kama kipengele cha usawiri wa mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza . Data ya utafiti imethibitisha madai haya katika dondoo lifuatalo:

> Watoto wakaimba
> Ndovu hawa mlienda kukaa
> Mlienda kukaa na msirudi
> Mkamwacha mama nyikani mwa fisi
> Mtoto wa fisi akilia
> Niume uwayo wa ndovu
> Kukicha asubuhi ni
> Ii!ii! Uwayo, uwayo wa ndovu

Katika dondoo hili watoto wa ndovu walikasirishwa na dhuluma aliyotendewa mama yao na fisi hadi wakatunga wimbo wenye motifu ya dhuluma. Uwasilishaji wa wimbo huu kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza unaafiki mhimili wa kinaratolojia unaoshikilia kuwa kuna jinsi mbalimbali za kusimulia matukio. Matumizi ya wimbo yalidhamiriwa kunata na kuathiri hisia za ndovu na kuwachochea kuanza mchakato wa kutafuta haki ya mama yao aliyeliwa na fisi. Mtazamo wa ndani ulitumika kutazama suala la dhuluma na kusimuliwa kwa sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza.

Utazamaji na usimulizi wa mchakato wa utafutaji wa haki ya ndovu aliyeliwa na fisi ulizua taharuki. Mchakato huu ulipochukua mkondo wa vita baina ya ndovu na fisi ulisababisha mauaji ya fisi wote. Data ya utafiti inathibitisha madai haya:

> Haya wakaambiwa,``sasa tunataka ndovu wetu. Wakasema, sasa tutawapiga kwa nini? Wakaambiwa sasa ni vita. Sasa ni vita tutapigana mpaka mtupatie ndovu mwenzetu. Vita vikaanza. Fisi wakapiga ndovu

> kwa mijeledi… walienda wakang`oa mti wakaja nao ukiwa hivi…Waliporushiwa walikufa wote.

Katika dondoo hili taswira sikivu ilitumika kuandaa pande zote mbili kwa vita. Taswira hii iliibua taharuki ambayo ilionyesha mtazamo wa Wandia kuhusu utafutaji wa haki kwa kutumia nyenzo ya vita. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza ilitumika kusimulia mtazamo huu. Kifo cha fisi ni jazanda iliyoonyesha fidia kwa kifo cha ndovu. Jazanda hii inaonyesha mtazamo wa Wandia kuhusu dhuluma na vifo vya fisi wote vinaashiria kuondolewa kwa dhuluma katika jamii na mwanzo wa jamii mpya.

## 5.5 Hitimisho

Uchunguzi ulibaini kuwa sauti ya simulizi na mtazamo ni nyenzo mbili muhimu ambazo zilitumika kusawiri mwonoulimwengu wa Wandia wa kijamii, kiuchumi na kisiasa katika ngano teule. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na ya tatu ni nyenzo ambazo zilitumiwa kusimulia mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule. Halikadhalika, mtazamo wa nafsi ya kwanza na ya tatu ndiyo mitazamo ambayo ilitumiwa kuchunjia habari kuhusu mwonoulimwengu wa Wandia.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Muhtasari

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule. Huu ulikuwa utafiti wa fasihi simulizi uliohusisha kushiriki uwasilishaji wa ngano teule na Wanjira Wa Rukenya, unukuzi wa ngano teule kwa lahaja ya Kindia, kutafsiri ngano teule kwa Kiswahili Sanifu, kusoma na kuhakiki matini za ngano teule na kuwasilisha matokeo ya uchunguzi kwa kuyapanga katika sura. Sura ya Kwanza ilijadili: Usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti ambayo yalilenga usawiri wa mwonoulimwengu na mchango wa sauti ya simulizi na mtazamo katika usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, machukulio, maelezo ya istilahi na vifupisho.

Sura ya Pili ilihusu mwauo wa maandishi ambao ni: Dhana ya mwonoulimwengu, sauti ya simulizi, mtazamo, historia fupi ya Wandia, mfumo wa maisha wa jamii ya Wandia, utamaduni wa Wandia, ngano, ngano za Wandia, historia fupi ya Fanani Wanjira wa Rukenya, usawiri wa wahusika katika ngano na msingi wa kinadharia.

Sura ya Tatu ilihusu mbinu za utafiti. Katika sura hii, vipengele vifuatavyo vilijadiliwa: Mahali pa utafiti, mpangilio wa utafiti, uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, maadili ya utafiti, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

Sura ya Nne na ya Tano zilihusu uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Sura ya nne ilijadili shughuli mbalimbali zilizotumika kusawiria mwonoulimwengu wa Wandia kijamii, kiuchumi na kisiasa na kutambua shughuli zifuatazo: Mivutano ya kijinsia, uchumba, ndoa, malezi, kudhibiti hisia na maadili zilitumika kusawiria mwonoulimwengu wa kijamii; kilimo, ufugaji, kibarua, uhunzi na biashara ni shughuli zilizotumika kufafanulia mwonoulimwengu wa kiuchumi na; usuluhishi wa migogoro na uongozi ni shughuli zinazotumika kusawiri mwonoulimwengu wa kisiasa.

Sura ya Tano ilijadili matumizi ya nyenzo za sauti ya simulizi na mtazamo katika usawiri wa mwonoulimwengu wa Wandia. Katika sura hii, masuala yaliyojadiliwa

katika sura ya nne yalichunguzwa kwa kina kwa kutumia kigezo cha mtazamo ambao ulisimuliwa kwa sauti ya simulizi. Mtazamo wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu ndiyo mitazamo ambayo ilitumika kuhakiki mwonoulimwengu wa Wandia. Aidha sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na sauti ya simulizi ya nafsi ya tatu ndizo sauti za simulizi ambazo zilitumika kusimulia mitazamo pamoja na mwonoulimwengu wa Wandia. Sura ya sita ni muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

**6.2 Hitimisho**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya naratolojia. Nadharia hii iliteuliwa kwa sababu ya vipengele vya kimsingi katika kuyachunguza masuala ya usimulizi, sauti ya simulizi na mtazamo. Vigezo hivi vilikuwa mihimili mikuu katika utafiti huu. Uchunguzi wa madhumuni ya kwanza ulibaini kuwa ngano teule zilisheheni shughuli mbalimbali zinazotumiwa kusawiri mwonoulimwengu wa Wandia kama vile: Mwonoulimwengu wa kijamii uliofafanuliwa kwa vipengele kama vile mivutano ya kijinsia, uchumba, ndoa, malezi, kudhibiti nafsi, maadili, haki ya kijamii na tabaka. Masuala ya kilimo, ufugaji, uhunzi, biashara na kibarua yalitumika kuelezea mwonoulimwengu wa kiuchumi wa Wandia. Mwonoulimwengu wa kisiasa wa Wandia ulifafanuliwa kwa vipengele vya usuluhishi wa migogoro, uongozi na haki.

Uchunguzi wa madhumuni ya pili ulitambua kuwa ngano teule zilitumia sauti ya simulizi na mtazamo kusawiria mwonoulimwengu wa Wandia. Sauti ya simulizi ya nafsi ya kwanza na ya nafsi ya tatu ndizo sauti ambazo zilitumika kusimulia mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule. Kwa upande mwingine, mtazamo wa ndani na wa nje ndiyo mitazamo ambayo ilitumika kutazamia shughuli zote zilizotumika kusawiria mwonoulimwengu wa Wandia. Matokeo ya utafiti huu, yalibainisha kuwa watunzi wa ngano teule walidhihirisha misimamo yao ya kiitikadi kuhusu suala la mwonoulimwengu wa Wandia kupitia kwa matumizi ya sauti ya simulizi na mtazamo. Aidha sauti ya simulizi na mtazamo ni mbinu mbili zinazokamilishana na zilisaidia usimulizi wa usawiri wa suala la mwonoulimwengu wa Wandia katika ngano teule. Kupitia sauti ya simulizi suala la mwonoulimwengu wa Wandia katika kila ngano teule lilibainishwa. Kwa upande mwingine kupitia kwa mtazamo, suala la mwonoulimwengu wa Wandia lilichujwa kwa kuona wahusika na vitendo vyao kwa miwani ya mtazamo.

Matokeo haya yanatazamiwa kumsaidia msomaji kuulewa muundo wa ngano teule kwa kuzingatia kigezo cha usimulizi na kuuelewa ujumbe unaowasilishwa katika simulizi. Utafiti utafaidi jamii ya wasomi kuelewa zaidi dhana ya usimulizi na nafasi yake katika kuchanganua masuala mazito ya kijamii kama vile mwonoulimwengu. Utafiti utaonyesha jinsi nyingine ya kuchanganua ngano kwa kutumia nadharia ya naratolojia mbali na mbinu zingine kama zile za kimtindo, kimaudhui na za lugha. Aidha, matokeo katika utafiti huu yataongeza marejeleo katika uwanja wa fasihi simulizi na kutumika na watafiti wa baadaye.

**6.3 Mapendekezo**

Utafiti huu ulishughulikia jinsi mwonoulimwengu wa Wandia unavyodhihirika katika ngano teule. Kwa kuwa kipengele cha ngano tu ndicho kilitumika kutafitia mwonoulimwengu huo, utafiti zaidi unapaswa kufanywa kuchunguzia mwonoulimwengu wa Wandia kupitia tanzu nyingine za fasihi simulizi kama vile; nyimbo, vitendawili, semi, miviga na ushairi ili kubainisha jinsi mwonoulimwengu wa Wandia unavyojitokeza katika vipera hivyo**.** Utafiti zaidi unaweza kufanywa kubainisha mwonoulimwengu wa jamii pana ya Agikuyu kupitia tanzu za fasihi simulizi. Aidha utafiti unaweza kufanywa ili kulinganisha mwonoulimwengu wa Wandia na mwonoulimwengu wa jamii nyingine za kiafrika. Nadharia ya naratolojia ilitumiwa kuchanganua na kusawiri mwonoumlimwengu wa Wandia katika ngano teule. Mapendekezo ni kwamba tafiti zaidi zifanywe kwa kutumia nadharia zingine tofauti na nadharia ya naratolojia.

## MAREJELEO


Abbott, H. (2002). *The Cambridge Introduction to Narratives*, Cambridge University Press.

Abrams, M. (1999). *A Glossary of Literary Terms* (Seventh Edition) San Antonio: Earl Mcpeek

Akivaga, S. & Odaga, B. (1982). *Oral Literature: A School Certificate Course*, Heinemann Educational Books (E.A) Ltd.

American Psychological Association (APA) (2020). Guidelines for referencing and Essay writing (7th Edition), Southern institute of Technology.

Arege, T. (2012). *Narration in Swahili Narrative Poetry: An Analysis of Utenzi Wa Rasi 'LGhuli*, (An Unpublished Ph.D. Thesis), University of Nairobi

Aristotle (1961) Aristotle's Poetics. New York, Hill and Wang

Bal, M. (1997). *Introduction to the Theory of Narratives* (3rd Edition) University of Toronto Press.

Bal, M. (1999), *Narratology: Introduction to the Theory of Narratives*. (Second Edition) University of Toronto Press, London.

Bauman, R. (1986) *Story Perfomance and Event: Contextual Studies of Oral Narrative*: Cambridge University Press.\

Benson T. (1964) *Kikuyu- English Dictionary*, Clarendon Press.

Bruner, E.M. (1984). Introduction: The Opening Up of Anthropology. In S. Platter and E.M Bruner (Eds), *Text, play and story: The Construction and Reconstruction of Self and Society- 1983 Proceedings of The American Ethnological society* (PP 1-16). Princeton, NJ: American Ethnological society.

Chesaina, C. (1994). Images of Women in African Oral Literature: A Case Study of Kalenjin and Maasai Oral Narratives, In Bukenya, A. et al (eds), Understanding Oral Literature, Nairobi University Press;Nairobi

Chimerah, R. (1990). *The Implications of the selected works of Ngugi in The Educational Thinking and Practices of Kenya*. Xerographic process on acid Free Paper Literature, Culture Education.

Churchil, L. (1982) The Teaching of Ethics and Moral Values in Teaching: Some Contemporary confusions. *The Journal of Higher Education* 53(3) (296-306/ 1981 749)

Cohan, S. & Linda, S. (1988). *Telling stories: A Theoretical Analysis of Narrative Fiction*. Routledge.

County Government of Kirinyaga (2023) Kirinyaga County Integrated Development Plan 2023-2027.

Currie G. (2010) Narratives and Narrators: A Philosophy of Stories. Oxford University Press, Oxford.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse*, Cornell University Press, Ithaca

Government of Kenya (GoK). The Constitution of Kenya 2010. Nairobi: Government Printer

Habib, M. (2011). *Literary Criticism from Plato to the Present: An Introduction*.Malden M.A: Wiley –Blackwell

Hogan, P. (2013). *Narrative Discourse: Authors and Narrators in Literature. Film and Art.* The Ohio State University Press.

Jahn, M. (2005). *A Guide to the Theory of Narrative. Part III of Poems, Plays and Prose: A guide to the Theory of Literary Genres*, University of Cologne.

Kabira W. (1983). *The Oral Artist*. Heinemann Educational Books (EA) Limited, Nairobi.

Kabira, W. (1993). Images of Women in Gikuyu Literature. (Unpublished Ph.D. Thesis), University of Nairobi.

Kabira, W. (1994). Gender and Politics of Control. An Overview of Images of Women in Kikuyu Oral Narrative. In Bukenya et al (eds) *Understanding Oral Literature*, Nairobi University Press.

Kabira, & Mutahi (1988). *Gikuyu Oral Literature*, East African Educational Publishers.

Kabira, & Waita (2010). *Reclaiming my Dreams*: *Oral Narratives by Wanjira Wa Rukenya.* Nairobi University Press.

Kawia, S. (2015). Kuchunguza Usawiri Chanya wa Mwanamke Katika Vitendawili vya Jamii ya Wanyiha (Tasnifu ya uzamili isiyo chapishwa) ; Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Keen, S. (2003). *Narrative Form*, Palgrave Macmillan

Kenyatta, J. (1938). *Facing Mount Kenya:* Heinmann Educational Books (EA) Limited.

King`ei, K. & Ndalu. A. (2013). *Kamusi Ya Methali Za Kiswahili*, East African Educational Publishers.

Kloepfer,R (1967). *Die Theorie der Literarischen Ubersetzung* (Munchen: Fink).1978 "Consommation ou Creation Litteraire; Critique de quelque de.base' *Oeuvres et Critiques* II,2,39-50

Koltko-Rivera, M. E. (2004) The Psychology of Worldviews. *Review of General Psychology* 8(1):3-58. Available from https://doi.org/10.1037/1089-2680.8.1.3.

Kothari, C. (2009). *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Age International.

Kraft, C. H. (1999) Culture, Worldview and Contextualization. *In Perspectives on the World Movement. 3d. ed.* Ralph D.W. and Stephen C.H. eds.pp.384-391. Pasadena: William Carey Library.

Kurka, R. (2004) Comments on Worldview. *In Global Civilization, Ancient world: Reader. 3rd ed. Vol.1* William L.Osborne and Ralph D.W. eds.11A. Pasadena: William Carey Library.

Leakey, L. (1977 a). *The Southern Kikuyu Before 1903*. VOL. I Academic Press.

Leakey, L. (1977 b). *The Southern Kikuyu Before 1903. VOL 3*. Academic Press.

Magesa, L. (1998). Eds, *African Religion: The Moral Traditions of Abundant Life*, Paulines Publications Africa.

Matravers, D. (2014) Justice and Punishment: The Rationale of Coersion (unpublished Ph.D. Thesis) London school of Economics and Political Science.

Mbiti, J. (1969). *African Religion and Philosophy,* Heinemann Kenya Ltd.

Miriti, K. (2016). *Mwonoulimwengu katika Methali za Wamuthambi,(Tasnifu ya uzamili* (M.A) (isiyochapishwa), Chuo kikuu cha Chuka.

Miruka,O.S.(1994) *Encounter with Oral Literature.* East African Educational Publishers.

Miruka, O. S. (1999). *Studying Oral Literature.* Acacia stanlex Publishers.

Msanjila, M. (1992). The Genesis of Theory: The Case Study of Kenyan Oral Literature. In Okombo and Nandwa (1992), *Reflections on Theories and Methods in Oral Literature*. Kenya Oral Literature Association (KOLA), UON.

Mugambi,A. & Waita,N. (2016). The Power of Technique and Device in African Narratives: A Case Study of Kikuyu Community in Kenya, Narratives Performance with Special Reference to Wanjira wa Rukenya: A Renown Artist. *International Journal of Current Research*, 8(06)33962-33973.

Mugenda,O.M & Mugenda, A.G.(2003). *Research Methods,* Acts Press.

Munene, W. (1995). *Mutaarani Mugikuyu [Mshauri Mkikuyu]*. East African Educational Publishers Ltd.

